ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais.
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu.
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa.
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa.
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.

10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa.
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa.
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi.
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole.
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae.
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 12 Aprili, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Spika, (Mhe. Pandu Ameir Kificho) Alisoma Dua.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwa idhini yako na kwa ruhusa yako, naomba kuweka mezani hotuba ya kuwasilisha taarifa ya ziara ya Rais wa China Mhe. XI Jinping nchini Tanzania tarehe 24 na 25 Machi, 2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mambo mengine ni lazima upate mafunzo maalum, XI Jinping. Sasa hii ndio yenyewe hasa. Mhe. Waziri tunakushukuru. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Waziri wa (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani, hotuba ya ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala ya mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba ya ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2011/2012. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala: Mhe. Spika, baada ya furaha kubwa ya Wajumbe kwa taarifa ya XI Jinping, sasa na mimi naomba kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwasilisha mezani hotuba ya ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2012/2013. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 76

Uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kura

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-
Daftari la kudumu la wapiga kura Zanzibar limeanzishwa na Tume ya Uchaguzi (ZEC) ili kurahisisha suala zima la uchaguzi nchini. Mara tu baada ya kuanzishwa daftari hili Tume hiyo iliahidi kuliweka wazi kila baada ya muda kwa ajili ya kuingiza wapiga kura wapya ambao wameshatimiza umri wa kupiga kura yaani miaka 18, sambamba na kuwatoa wale wote ambao aidha wamefariki, wamehama au kupoteza sifa za kuwa wapiga kura.

Je, zoezi hili limefanyika mara ngapi tangu daftari hili lianzishwe.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli tangu kuanzishwa rasmi kwa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Zanzibar hapo Novemba, 2004. Tume iliahidi kuliweka wazi daftari kila baada ya muda kwa ajili ya kuingiza wapiga kura wapya ambao wana sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa sheria. Tangu mwaka huo hadi hivi sasa kazi za uandikishaji wa wapiga kura wapya zimefanyika mara mbili kama ifutavyo:-

- Awamu ya kwanza ya uandikishaji ulifanyika sambamba na zoezi la ubadilishaji wa shahada za zamani (zilizotolewa mwaka 2004 na 2005) za wapiga kura. Zoezi hili lilianza tena tarehe 6 Julai, 2009 hadi tarehe 14 Februari, 2010

- Awamu ya Pili ya uandikishaji wa wapiga kura wapya ambayo pia ilifanyika sambamba na zoezi la ubadilishaji wa shahada za zamani za wapiga kura ilifanyika kuanzia tarehe 1 Machi 2010 hadi tarehe 5 Mei 2010.

Mhe. Spika, hivi sasa Tume imo katika hatua za kuanza kazi ya uandikishaji wapiga kura waliotimiza sifa kwa mujibu wa sheria. Kazi hii inafanyika kwa mashirikiano na ndugu zetu wa UNDP ambao wametusaidia fedha shilingi 756,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi hiyo, ambapo tayari wametoa

milioni 480 na SMZ imetenga milioni 350 na tayari wametoa milioni 339. Kwa hivyo, utekelezaji wa shughuli hii utafanyika kama ulivyopangwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ambaye pia ni mpiga kura wangu Mhe. Mohamed Aboud, naomba niulize swali moja dogo sana kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba limefanyiwa uhakiki mara mbili hili daftari tangu lianzishwe, na kwa kuwa katika uandishi wa daftari hili vyama vya siasa vilishirikishwa katika kuwekewa mawakala katika uandishi wake.

Je, katika kulifanyia uhakiki daftari hili ule utaratibu wa kuwashirikisha vyama vya siasa kupeleka mawakala wake katika zoezi hili upo au ndio ulimalizika katika uandishi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, nia na madhumuni makubwa ya Tume ya uchaguzi ni kufanya uchaguzi utakaokidhi haja, utakaotenda haki kwa wahusika wote na wadau wote, na kuhakikisha kwamba vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi huo vinaridhika na hatua zote zinazochukuliwa. Kwa hivyo, kila jambo jema ambalo litapelekea kufanya kazi vizuri, basi tume ya uchaguzi italipa kipaumbele na kuliwekea maanani ili tutekeleze uchaguzi wetu vizuri.

Hivi sasa Mhe. Spika, tumo katika hatua za mwisho kufanya marekebisho ya sheria na kanuni za uchaguzi ili ziendane na matakwa ya wadau, ziendane na mapendekezo yaliyotolewa na taasisi za uangalizi wa uchaguzi na zikidhi haja kwa ajili ya kuendesha uchaguzi huru na wa haki.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa kipindi ni kikubwa bado daftari hili halijaendelezwa na kuna wananchi wengi ambao wameshafikia umri, na waziri anasema kwamba wako katika matayarisho ili waendelee kuandikisha katika daftari la kudumu.

Sasa namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa wako katika matayarisho ya mwisho. Je, Tume ya Uchaguzi imejipanga vipi kuwaelimisha wananchi, ili kushiriki vizuri katika zoezi hilo pindi muda utakapofika.

Je, kwa kuwa vituo vya uandikishaji daftari kwa kipindi kilichopita linajulikana, litakuwa ni vile vile au vitaongezwa vituo vyengine vya uandikishaji wa daftari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, tutahakikisha kwamba Tume ya uchaguzi inachukua kila hatua kuelimisha wananchi juu ya suala zima la daftari la kudumu la wapiga kura na kuwaelimisha wananchi haki zao, ili waweze wote kuandikishwa usiwepo usumbufu.

Kwa sasa utaratibu wa vituo ni ule ule, lakini ikionekana kwamba kuna uhitaji wa kufanya vyenginevyo, basi tutafanya hivyo ili kurahisisha zoezi hili lifanyike vizuri kwa usalama na kwa utulivu mkubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii leo asubuhi kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba kwa kuwa wapo vijana wanaoingia katika rika la kutimia umri wa kupiga kura na bado hawajaelewa umuhimu wa daftari la kupiga kura, pamoja na kujiandikisha.

Je, Mhe. Spika, tume imejitayarishaje kutoa elimu kwa vijana hao kuhusu umuhimu huo wa daftari la kupiga kura.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ni wajibu wa Tume kuelimisha wananchi wote, wakiwemo wale vijana wapya ambao wanahitaji kupata elimu hiyo, ili waweze kuelewa umuhimu wa daftari la kudumu la wapiga kura. Kwa hivyo, namuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tume imejipanga na elimu itatolewa, zoezi hili litakwenda vizuri na kila mwananchi atapata haki yale.

Nam. 80

Uingizaji wa Dawa za Kulevya Nchini

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Kwa kuwa dawa za kulevya zimeshaathiri vijana wetu wengi na hadi leo hii vijana wanaendelea kujitumbukiza katika janga hilo jambo ambalo linarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Na kwa kuwa dawa hizi lazima ziingizwe nchini ndio vijana waweze kuzitumia.

(a) Je, ni kesi ngapi za waingizaji unga zimepelekwa Mahakamani kwa kipindi cha mwaka 2012/2013

(b) Ni watuhumiwa wangapi wako rumande na wangapi wameshahukumiwa kwa kosa hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kabla ya kujibu swali la Mhe. Mwakilishi, naomba nikubaliane naye kwamba kweli uingizaji wa dawa haramu za kulevya na matumizi ya dawa hizo kunachangia kwa kiasi kikubwa katika kudumaza maendeleo ya taifa letu, na mustakbali mzuri wa vijana ambao siku zote tumekuwa tukieleza kwamba vijana ni msingi mkuu wa taifa la leo na la kesho.

Mhe. Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 80 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013 jumla ya kesi sita (6) za waingizaji wa dawa za kulevya zimeripotiwa, zilizowahusisha wanaume watano na mwanamke mmoja. Aidha, watuhumiwa wanne niliowataja hapo juu, kati ya hao (6) wako rumande na kesi zao zinaendelea na wawili tayari wameshahukumiwa. Hukumu mbili tayari zimeshatolewa.

Mhe. Spika, napenda kuchukua nafasi hii kwa mara nyengine tena, kwa kufanya hivyo kuviomba vyombo vya dola, vilivyopewa jukumu la udhibiti wa dawa za kulevya, kuongeza kasi ya utekelezaji wa kazi zao za udhibiti ili kunusuru vijana wetu wasizidi kuangamia na janga hili la matumizi ya dawa za kulevya. Ushirikiano wa wananchi kuondosha muhali, kutoa taarifa na ushahidi, ni silaha tosha ya kusaidia katika kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya janga hili. Pia naviomba sana vyombo vya sheria kuwa waadilifu katika kufikia maamuzi, yasiyo na shaka katika utekelezaji wa majukumu yao.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali moja dogo sana la nyongeza. Kwa kuwa Zanzibar kesi zilizokamatwa ni (6) tu, na kwa kuwa usambazaji wa unga wa kulevya katika nchi ni kubwa, ukilinganisha na kesi (6) tu ambazo zimekamatwa.

(b) Je, Mhe. Waziri utakubaliana na mimi kwamba serikali haiko makini katika kudhibiti uingiaji wa dawa za kulevya katika nchi.

(c) Kwa kuwa kuna manung'uniko mitaani, kwamba baadhi ya wawekezaji wanajishughulisha sana, hususan katika nyanja hizi za mahoteli, wanajihusisha sana na masuala haya ya unga wa kulevya. Je, serikali imefanya utafiti wa kina na kuona hili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, katika swali lake mama Mhe. Saleh Nassor Juma alitaka kujua ni kesi ngapi

zilizoripotiwa kwa mwaka 2012/2013. Kesi za wanaokamatwa na unga wa kulevya ni nyingi, sio (6) tu Mhe. Spika.

Kwa hivyo, hii taarifa tuliyomletea ni kama alivyoiomba yeye ya mwaka 2012/2013. Naomba nikiri kwamba vita vya kupigana na waingizaji wa dawa za kulevya ni vigumu, hasa ukizingatia suala zima la kwamba nchi yetu ni kisiwa, na kisiwa hiki kina bandari nyingi ambazo si rasmi, au kwa lugha nyengine tunaziita njia za panya, ambazo uwezekano wa kuingizwa dawa kutoka baharini labda ni mkubwa mno. Lakini vyombo vya dola vinajitahidi sana.

Kuhusu suala la pili. Mhe. Spika, naomba sana kama kuna taarifa kama hizi, basi ni vizuri sana ziripotiwe katika vyombo vya dola ili ziweze kufanyiwa kazi. Ofisi yangu hadi hivi sasa haijapokea taarifa yoyote ya aina hiyo. Kama tutaipokea sisi tutaipeleka kunakohusika ili kuzifanyia kazi.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika majibu yake amesema kwamba, kwenye mwaka 2012/2013 kesi (6) zimeripotiwa, naomba anisaidie majibu.

(b) Je, kati ya hizo kesi (6) ni raia wa nchi gani ambao wamethibitishwa kuhusika na dawa hizo.

(c) Wizara imefanya uchunguzi ili kubaini ni raia wa nchi gani, ambao wanatumia mlango wa Zanzibar kupitisha dawa za kulevya.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kati ya watuhumiwa (6), watuhumiwa (5) ni Watanzania na mtuhumiwa mmoja ni raia wa kigeni. Kwa hivi, sasa siko katika *position* ya kumwambia uraia wake.

Suala hili la kuweza kufanya utafiti labda kujua ni raia wa nchi gani, ndio hasa wanaoitumia bandari na uwanja wa ndege wetu katika usafirishaji wa dawa za kulevya. Naomba suala hili nilifanyie utafiti na tumletee kwa maandishi.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Waziri. Mhe. Spika, ili kuwanusuru vijana wetu kutumia dawa za kulevya kumeanzishwa *Sober House*. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, ni *Sober House* ngapi zimeanzishwa mpaka hivi sasa. Pia Wizara imewasaidiaje vijana hao ili kujitegemea kimaisha na kuondokana na kutumia dawa za kulevya

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, mpaka hivi sasa katika visiwa vya Unguja na Pemba, kuna *Sober House* ambazo zimeanzishwa na ambazo ofisi yangu inazitambua jumla yake ni 9.

Vile vile Mhe. Mjumbe alitaka kujua serikali inazisaidia vipi *Sober House* hizi. Mhe. Spika, kuanzia bajeti ya mwaka juzi 2011/2012 na bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa mara ya kwanza serikali imeanza kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuzisaidia kwa kiasi fulani *Sober House.*

Mhe. Spika, bajeti ya mwaka 2011/2012 *Sober House* zilipatiwa jumla ya shilingi milioni 10 na kwa bajeti ya mwaka 2012/2013 *Sober House* hizi zimepatiwa jumla ya shilingi milioni 15. Kiasi hiki ni kidogo mno kifedha kutokana na mahitaji na shughuli zinazofanyika *Sober House* hizo.

Hata hivyo, msaada wa serikali haupo tu kifedha. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tume ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ikishirikiana na Kitengo cha Ukimwi cha Wizara ya Afya, kinafanya juhudi ya kuwasaidia kupima afya zao vijana hawa ambao wako katika *Sober House*, kwa ajili ya kutambua kama wameambukizwa maradhi hasa ya homa ya ini au maradhi ya ukimwi na kuweza kuanzisha tiba, ili kuwa pamoja wawe wanatibiwa afya zao pamoja na kuacha dawa za kulevya.

Mhe. Spika, pia katika *Sober House* hizi, ofisi yangu imewasaidia baadhi ya *Sober House*, kuweza kuandika miradi na kuomba fedha kwa ajili ya kuweza kujiendesha wao wenyewe. Mfano, katika *Sober House* iliyoko Wete Pemba kwa kushirikiana na Shirika la UNODC la Umoja wa Mataifa, linalohusika na shughuli za dawa za kulevya. Wanategemea kupata fedha hivi karibu za kuanzisha mradi wa ng'ombe wa kuzalisha maziwa na juhudi kama hizo zinaendelea katika *Sober House* nyengine.

Nam. 60

Matibabu kwa Wanaomwagiwa Tindikali

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Zanzibar kumekuwepo na matukio ya watu kumwagiwa tindikali na baadae kusafirishwa nje ya nchi kwa matibabu, wakati tuna hospitali yetu ya Taifa ya Mnazi Mmoja. Kwa nini wagonjwa wa aina hiyo wasitibiwe hapa hapa Zanzibar.

(a) Kama hakuna madaktari wenye uwezo wa kutibu magonjwa ya aina hiyo, ni lini wataanza kupatikana hapa Zanzibar.

(b) Kwa kuwa matukio ya kumwagiwa watu tindikali yamekuwa yakijitokeza kila mara, serikali ina mpango gani wa kuwapatia mafunzo nje ya nchi madaktari wake, ili kupunguza gharama za matibabu kufanyika nje ya nchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako kwanza nilikuwa nina ombi kwako. Naomba Mhe Spika, waandishi wetu wa habari wawe wanaandika kile ambacho tunakisema katika Baraza na sio kuandika vitu ambavyo ni vya kupotosha taarifa zile tunazozisema. Waandike vile ambavyo ninavizungumza na vilivyoko kwenye Hansard.

Mhe. Spika, nisingependa kitokee kitendo kilichotokea tarehe 04/04/2013, kwa kuandika maneno ambayo sikusema.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi

TAARIFA

Mhe. Spika: Labda usubiri kidogo Mhe. Naibu Waziri wa Afya. Ni kweli kabisa waandishi wa habari wanapaswa kabisa kuchukua taarifa sahihi zinazotoka katika Baraza hili. Kutofanya hivyo, kwa kweli itakuwa ni kulikosea Baraza. Ilivyo Baraza lina haki ya kumuita mhariri na akaweza kujibu kwa nini akatoa taarifa ambazo si sahihi.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwatahadharisha ndugu zetu waandishi wa habari mbali mbali, wa vyombo vyote ambao wanapata nafasi ya kuja hapa au wale ambao wanapeana taarifa zinazohusu Baraza, wanapaswa kabisa kutoa taarifa sahihi ambazo zinatokana na Baraza hili. Kama wana wasi wasi wanaweza kufuatilia Hansard za Baraza hili, ili wakapata taarifa sahihi ambazo zimetoka hapa. Hiyo ni lazima kufanya hivyo. Nashukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 60 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kabla sijatoa jawabu naomba nitoe maelezo kidogo. Matokeo ya kihalifu ya watu kumwagiwa tindikali hapa Zanzibar ni ya kinyama na umeanza kuwa ni mtindo ambao una dhamira maalum, kuwafanyia watu maalum. Sababu ya kufanya hivyo hao wanaofanya wanazijua wao wenyewe. Lakini wafahamu kwamba wana dhima kwa kuwadhulumu wengine. Kama

jambo analofanya mlengwa huridhiki nalo huna sababu ya kuchukua hukumu mikononi, kwani vyombo vya sheria vipo.

Mhe. Spika, mapendekezo ya Mhe. Mwakilishi ya kuanza kutengeneza utaratibu maalum na kuandaa madaktari kwa ajili ya kazi hiyo ya matukio ya kihalifu, kufanya hivyo ni kuhalalisha hayo yanayotendeka.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya huwa inaandaa fani za madaktari kulingana na mahitaji makubwa ambayo yana ushahidi wa takwimu za maradhi yaliopo nchini na sio matukio.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, hiki chombo ni kizito cha wananchi. Kauli aliyoitoa Mhe. Naibu Waziri wa Afya hivi sasa haikuridhisha. Kifungu cha 59(8) (a) kutumia lugha ya kashfa

Mhe. Spika: Hebu, Mhe. Jaku Hashim. Juu ya nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhalalisha. Mimi nimeleta swali sikuja kuhalalisha hapa. Alipokuwa akijibu alisema kwamba mapendekezo ya Mwakilishi ya kuanza kutengeneza utaratibu maalum, wa kuandaa madaktari kwa ajili ya kazi hiyo ni matukio ya kuhalalisha. Mimi nimeleta swali sikuja kuhalalisha hapa.

Mhe. Spika: Msikilize majibu yake Mhe. Naibu Waziri, halafu kama kuna swali la nyongeza utauliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: *Hewallah*.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Afya, anza upya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nashukuru kwa kuingilia kati. Mhe. Spika, pindipo tukio kama hilo likijitokeza cha muhimu ni ule msaada wa mwanzo atakaopewa mhanga wa tukio hilo huko katika jamii.

Msaada anaotakiwa kupewa mtu katika jamii akimwagiwa tindikali ni kama huu ufuatao.

1. Kummwagia maji mengi iwezekanavyo ili kupunguza nguvu ya tindikali isizidi kumuathiri mlengwa.
2. Kuchana na kumvua nguo zilizomwagikiwa haraka iwezekanavyo, ili zising’ang’anie mwilini na kumsitiri mhanga kwa kumfunika nguo

nyepesi. Kama kanga, kitenge, seruni na kadhalika kitakachopatikana karibu.

3. Pia kumkimbiza mhanga hospitali akapate huduma ya kwanza na dawa za kupunguza maumivu.

Mhe. Spika, tukifanya hivyo, tutakuwa tumemtibu mgonjwa kwa asilimia kubwa. Baada ya hapo hatua za matibabu zitafuatia kulingana na madhara yaliyompata muathirika wa tukio hilo na kama itabidi kusafirishwa atasafirishwa. Kwani kuokoa maisha ya binadamu ni gharama hata kama hakusafirishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Spika. Kwanza kabla sijauliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, hii dhana iliyokuja juzi niliuliza swali mimi, Mhe. Naibu Waziri akawa anapiga kelele kuhusu dawa za ukimwi kutowepo. Hili suala tulilizungumza kama Kamati na nikamwambia kamati ilipotembelea maabara kule Maruhubi dawa za ukimwi hazipo. Kamati hiyo hapo shahidi, Mhe. Hija Hassan Hija yupo, Mhe. Ashura Sharif Ali yupo na wengine wapo.

Kwa hivyo, asimtupie lawama mwandishi, kama kuzungumza tumezungumza Kamati na swali la nyongeza niliuliza mimi, kwamba dawa hiyo ilipotembelea Kamati hamna.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hilo ndio nyongeza lako au sio. *(Vicheko/Makofi)*

UFAFANUZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, labda nitoe ufafanuzi kuhusiana na hili. Kweli kabisa kwamba kulikuwa na taarifa ambayo kwa mujibu wa *hansard* zetu na namna ilivyoripotiwa kwenye gazeti haikuwa sahihi, baadhi ya maelezo yaliomo kwenye gazeti wala hayakuzungumzwa na Mhe. Naibu Waziri. Sasa tukamuita ndugu yetu huyu na wala haina haja ya kumtaja, ili asawazishe hiyo taarifa kwa ajili ya kuendana na kwa mujibu wa taarifa ilivyotoka hapa Barazani.

Kwa hivyo, inavyoonekana ile taarifa kwamba kuna mtu labda amempa na hakuchukua usahihi wa ile iliyotoka Barazani. Matokeo yake taarifa iliyotoka Barazani ambayo iko kwenye *hansard* na taarifa iliyotokeza kwenye gazeti ni vitu viwili tofauti.

Waheshimiwa Wajumbe, tulichukua hatua kwa kumuita mhusika huyo, ili asawazishe taarifa hiyo iendane kwa mujibu wa zile taratibu na vile ilivyojitokeza ndani

Nam.69

Kilimo cha Matunda na Mboga Mboga

Mhe. Asha Abdu Haji – Aliuliza:-

Kilimo cha mboga mboga na matunda kwa hivi sasa kimekuwa ni muhimu sana hasa kutokana na mahitaji makubwa katika Biashara ya Utalii. Aidha wakulima wa mboga mboga na matunda wamejenga matumaini ya kupata mapato makubwa yatakayowasaidia kutatua matatizo yao ya maisha ya kila siku.

Ni ukweli ulio wazi kuwa wakulima wetu hutumia muda wao mwingi na nguvu kubwa katika kilimo hicho, lakini matokeo yake hawafikii lengo kwa sababu ya kupata mafanikio madogo kutokana na kufanya kazi hiyo bila ya ujuzi na maelekezo kutoka katika Kitengo cha Wataalamu wa Kilimo cha Mboga Mboga na Matunda.

(a) Je, wizara yako ina wataalamu wangapi wa mboga mboga na matunda.

(b) Je, wataalamu hao wamegaiwa vipi katika wilaya zetu na majimbo yetu.

(c) Je, ni kweli wataalamu hao wanafanya kazi zao katika maeneo waliyopangiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inao wataalamu 158 kwa mazao ya mboga mboga na matunda na mazao mengine ya chakula.

(b) Wataalamu hao wamegawika kwa shehia na wilaya katika fani tofauti za kilimo na wala sio mboga mboga peke yake. Hata hivyo kutokana na uhaba wa mabwana shamba katika baadhi ya maeneo, Bwana shamba mmoja anahudumia zaidi ya Shehia moja.

(c) Mhe. Spika, wataalamu wanapangiwa maeneo katika Shehia, Wilaya na Mikoa na wanakuwa chini ya Uongozi wa Serikali za Wilaya na Shehia na kwa hivyo taasisi hizo zinatakiwa kufuatilia utendaji wa kazi zao. Wizara ya

Kilimo kwa upande wake ina jukumu la kusimamia utendaji wa wataalam wake katika ngazi zote na inafanya hivyo kutokana na muundo wake wa kuwa na Maafisa wa Kilimo wa Mikoa na Wilaya, ambao ndio wanaoratibu mipango ya utendaji kazi wa wataalamu hao, na kuhakikisha wanatekeleza kazi wanazopangiwa.

Wataalam hao kwa upande wao wanawajibika kufuatilia kazi zao za kila siku na kutoa ripoti ya kazi zao kama walivyopangiwa. Kwa utaratibu huo Wizara inatarajia kila mtaalam anafanya wajibu wake.

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Kwa kuwa kuna malalamiko ya wataalamu, yaani Mabwana shamba hawapatiwi mafunzo. Je, wizara yako haioni kuwa inawanyima haki zao za msingi.

(b) Kuna Mabwana shamba wangapi katika Wilaya ya Kusini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, malalamiko nathubutu kusema ndio mafanikio ya kazi. Hivi sasa upo mradi wa *TAP*, ambao unafadhiliwa na *USA* lengo lake ni kusaidia kutoa mafunzo kwa Mabwana shamba. Mhe. Spika, hivi sasa ninavyozungumza ni kwamba tangu tarehe 8 kuna Mabwana shamba kama 25 ambao wako Mansoon kwa ajili ya kupatiwa mafunzo. Kwa hivyo, wizara yangu inatoa mafunzo kwa wataalamu hao.

Mhe. Spika, Wilaya ya Kusini ina Mabwana shamba 21.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri. Kwa kuwa kilimo cha mboga mboga ni muhimu sana kwa Sekta ya Utalii na kwa kuwa thamani ya soko kubwa la mboga mboga hizo ni mboga zinazotumia mbolea isiyokuwa ya *chemicals*.

Je, serikali ina mpango gani wa kuwaelimisha na kuwahamasisha wajasiriamali kutumia mbolea zisizokuwa za *chemicals*.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Mabwana Shamba Darasa inatoa taaluma ya kutumia mbolea hizi zisizo na *chemicals* na madarasa haya yanafanya kazi kwa kila sehemu kwa ajili ya kutoa taaluma hii. Vile vile wakulima wameshajihika sana kupitia mradi huu wa *Farmer School*.

Kwa hivyo, tumo tunatoa taaluma kwa kupitia madarasa haya na wananchi wameelimika vya kutosha, ndio maana hivi sasa utakuta wafugaji kama vile ng'ombe au kuku mbolea inakuwa adimu haipatikani, ambapo zamani ulikuwa ukienda kwa wafugaji wa kuku au ng'ombe mbolea ipo nyingi. Kwa maana hiyo, hili linatoa taaluma vya kutosha.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante na mimi kunipa nafasi moja ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein amekuwa akishajihisha na kuwaomba vijana kujiendeleza katika kujikwamua kiuchumi kwa kujishughulisha na masuala haya ya kilimo. Kwa mfano, kuna vijana wa Kikundi cha ZASOZA ambao wapo pale Tunguu.

Je, wizara inawatambua vijana hawa na kama inawatambua ni juhudi au msaada gani wametoa kuwapelekea wataalamu, ili kuweza kujiendeleza na Kilimo chao cha Mboga mboga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, hicho kikundi sikukisikia jina lake na kiko wapi.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, hebu elezea vizuri hicho kikundi chenyewe.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante nimesema kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein amekuwa akishajihisha na kuwataka vijana kujikwamua kiuchumi kwa kujishughulisha na masuala haya ya kilimo hususan mambo haya ya mboga mboga. Katika maeneo ya Tunguu kuna vijana wanaitwa ZASOZA wamejikusanya na wanajishughulisha na masuala haya ya Kilimo cha Mboga mboga.

Je, wizara inawatambua vijana hawa na kama inawatambua ni msaada gani ambao wamewapa katika masuala ya kuwapatia wataalamu, ili kuweza kulima kilimo cha kisasa cha mboga mboga.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kikundi hicho kilichopo Tunguu tunajua kwamba vipo vikundi vingi, lakini kikundi hichi cha ZASOZA kipo na tunakijua. Lakini *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda taarifa zake nitamletea kwa maandishi. *(Makofi)*

Nam. 37

Kuchukuliwa Hatua Watendaji Wasio Waaminifu

Mhe. Hija Hassan Hija Aliuliza:-

Mara kadhaa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wamekuwa wakikemea na kuionesha wazi serikali juu ya wizi wa fedha na mali za umma unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waaminifu kwa taifa. Kwa kuwa pamoja na juhudi za serikali kuwaahidi wananchi kuwa ipo tayari kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria watendaji wasio waaminifu, imeonekana wazi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haina nia ya dhati na ndio maana vitendo hivyo vinaendelea siku hadi siku.

(a) Je, serikali inayo taarifa kuwa upo upotevu wa fedha katika Idara ya Ujenzi ndani ya Wizara ya Ardhi.

(b) Kama upotevu upo ni kiasi gani kilichopotea na ni nani waliohusika na upotevu huo na wamechukuliwa hatua gani.

(c) Zipo taarifa kuwa Mtendaji mmoja aliyehusika amekuwa na tabia hizo kwa muda mrefu na aliwahi kupoteza zaidi ya milioni 38 za mradi wa *MACEMP* na adhabu yake akahamishiwa Idara hiyo ya Ujenzi. Je, huko sio kulindana.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 kama hivi ifuatavyo:-

Kwanza naomba kutoa maelezo mafupi juu ya hoja ya Mhe. Mwakilishi kwamba mara kadhaa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar wamekuwa wakikemea na kuonesha wazi serikali juu wizi wa fedha za umma unaofanywa na baadhi ya watendaji wasio waaminifu kwa taifa.

Napenda kueleza kwamba suala la upotevu wa fedha katika Taasisi yangu ya Idara ya Ujenzi, serikali ililigundua wenyewe kupitia kwa Mkaguzi Mkuu na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali na Mashirika na ndipo tulipolitolea taarifa polisi. Mhe. Spika, hakuna Mjumbe au mtu mwengine ambaye aliligundua suala hili na kuliletea taarifa.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye vifungu (a), (b), (c) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Kwa kuwa suala la upotevu wa fedha za Idara ya Ujenzi lipo polisi kwa uchunguzi wa kisheria, hivyo itakuwa si sahihi kutoa maelezo yake kabla ya uchunguzi haujakamilika. Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kupitia kwako Mhe. Spika, wawe wastahamilivu mpaka uchunguzi wa polisi utakapokamilika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nimemsikiliza Mhe. Waziri kwa makini na inaelekea anajaribu kukinga hoja hii isizungumzwe kwa sababu iko polisi, lakini naomba nimuulize kama ifuatavyo.

Kwa kweli mimi ni miongoni mwa watu ambapo nimeziona *documents* ambazo zimethibitishwa na idara yake kwamba upo wizi. *Documents* hizo zikiwemo *cheque* za kughushi na *voucher* ambazo zilizofuatiliwa mpaka benki na kuthibitishwa kwamba idara hii imepoteza fedha hizo.

(a) Wizi huu ulipogunduliwa hadi sasa ni kipindi gani.

(b) Kwa kuwa idara imethibitisha kupitia *cheque* za kughushi, *bank statement* kwamba watendaji wa idara hii ndio walioghushi fedha, hivi bado kunahitajika uchunguzi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, swali la mwisho sikulisikia.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, swali la mwisho rudia kidogo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, swali la mwisho ni kwamba kwa kuwa idara yake imethibitisha, kwa maana Idara ya Fedha, yaani *cashier* na mhasibu wake wameghushi *cheque* na imefuatilia mpaka benki na imepatikana *bank statement*, kwamba wametoa fedha kinyume na utaratibu. Kwa hivyo, namuuliza bado ushahidi wote huu kunahitajika uchunguzi.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ameuliza ni muda gani tangu imegunduliwa hii taarifa. Kwa kweli hivi sasa inafika miezi 6 tangu ilipogunduliwa hii taarifa na mimi nimesikitishwa vile vile kama mnavyosikitishwa nyinyi kutokana na upotevu.

Mhe. Spika, kweli baada ya wizara kupata wasi wasi wa *accounts* zake kwamba ukipeleka *cheque* unaambiwa fedha hamna wakati hesabu ilioko kule ndani inaonesha kwamba fedha zimo. Kutokana na hali hiyo, hapo ndipo tulipochukua hatua ya kumtaka Mkaguzi Mkuu afanye uchunguzi na kwa bahati Mkaguzi Mkuu anafanya uchunguzi na akagundua kwamba zipo dalili za kuwa wizi upo na ndio maana sikutaka niseme kiasi gani, kwa sababu

unaweza kutaja zipo milioni 60 na kule zikazidi na ukampa nafasi mshtakiwa kuja kusema kwamba mbona wizara ilisema kiasi hichi na nyinyi munaniambia kiasi hichi.

Kwa hivyo, kwa kuwa kuna dalili basi polisi imekwenda ndani kuchunguza suala hili, ili kujua hasa fedha zenyewe ni kiasi gani na yeye amezungumza wahusika ni wawili, lakini wanaweza kuwa zaidi ya wawili na pengine kuna mshikamano mkubwa wa kusababisha matatizo haya, kwa maana hiyo ndio maana tunawaachia polisi watumalizie kazi hii.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Spika, kwa kuwa serikali imekiri kwamba kuna wizi uliofanyikana katika idara hiyo iliyotajwa na kwa kuwa Baraza letu hili halizuiliki kujadili suala lilioko polisi, isipokuwa huzuilika tu jambo ambalo liko Mahakamani.

Vile vile hatua hizi kuna maana mbili, yaani kuna suala la mambo ya kijinai ambazo ndizo hizo zilioko polisi na mahakamani, pia kuna hatua za kinidhamu, yaani serikali wajibu wake ni kuchukua hatua za kinidhamu.

(a) Ni muda gani tangu suala hilo litambulike kuanzia pale lilipotambulika limechukua muda gani.

(b) Wizara imechukua hatua gani za kinidhamu dhidi ya hao waliohusika na kadhia hiyo.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nimesema kwamba tangu suala hili limeonekana inafika miezi 6 sasa, lakini hatujapata jibu kutoka polisi. Lakini hata hivyo napenda kumfahamisha kwamba hatua za kinidhamu tayari tumeshachukua, kwa sababu hawa ambao walionekana wazi wazi tumewasimamisha kazi na hawapo kazini.

Nam. 43

Matengenezo ya Barabara

Mhe. Salim Abdalla Hamad Aliuliza:-

Mhe. Spika, kabla ya kuomba kujibiwa swali langu Nam. 43 lenye vifungu (a) na (b) kutanguliza shukurani kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kwa kuona umuhimu wa kuwaondolea shida wananchi kwa kuwatengenezea

barabara zao, ili zihudumie vizuri pamoja na kuwawezesha kupeleka karafuu zao vituoni.

Baada ya maelezo hayo, Mhe. Spika naomba swali langu Nam. 43 lenye vifungu (a) na (b) lijibiwe.

Katika msimu wa uchumaji wa karafuu, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ilitoa fedha nyingi kwa matengenezo ya barabara zilizokuwa katika hali mbaya, ili wananchi waweze kupeleka karafuu zao vituoni. Huu ulikuwa ni msaada mkubwa kwa wananchi.

(a) Ni sababu zipi zilizozifanya barabara zile zisiendelezwe alau kutiwa kifusi baada ya msaada mkubwa huu kutoka Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

(b) Kwa wizara kuziachia barabara zile kurudia hali yake ya zamani baada ya kufanyiwa matengenezo, si kuitia hasara serikali na kuwakatisha tamaa wananchi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kwamba katika mwaka 2012 katika Jimbo la Mtambwe kulikuwa na matatizo makubwa sana ya barabara. Aidha serikali kwa kulithamini hilo na kutokana na hali mbaya ya barabara za ndani katika maeneo kadhaa jimboni humu na kutokana na ufinyu wa bajeti wa halmashauri husika.

Kutokana na hali hiyo, ndipo Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ikatoa ushirikiano stahiki kwa kuipatia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano mchango wa gharama za mafuta, kwa ajili ya kuinusuru hali hiyo, vifaa na wataalamu walishiriki kikamilifu na kuziwezesha barabara hizo kadhaa kupitika bila ya usumbufu. Barabara hizo za Makongeni – Mkanjuni, Chanjaani na Kele.

Sasa katika kujikinga na jambo kama hili lisijirejee tena mwakani, basi mambo ya msingi yamezingatiwa ikiwa pamoja na kuitaka halmashauri husika kutenga fedha zitakazokidhi matengenezo yanayostahiki ikiwa ni kuziwekea kifusi cha kudumu cha muda mrefu zaidi.

Mhe. Spika, hivyo ni dhahiri kwamba sababu ya msingi iliyopelekea kutowekwa kifusi barabara hizo husika kulitokana na ukosefu wa fedha kutoka katika halmashauri husika.

(b) Mhe. Spika, matarajio yetu ni kuona kwamba halmashari husika watatenga fedha na gharama stahiki. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano ikiwa ni pamoja na vifaa, mafundi kwa ajili ya matengenezo hayo kwa barabara zote zilizomo katika jimbo hilo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata jibu la kuridhika kwa swali langu. Lakini Mhe. Spika, naomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, ninavyoelewa ni kuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina Mfuko Maalum wa Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, ambao hutumika kwa kutengenezea barabara takriban katika nchi yetu. Vile vile kwa sababu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tayari imeshasaidia kuzifanyia *grading* barabara hizi.

(c) Ni kwa sababu ipi hasa iliyofanya ikawa tena wizara haikuendeleza.

(d) Mhe. Waziri ameeleza kuhusu halmashauri na kutoza fedha kwa habari ya mambo mengine. Lakini Mhe. Spika, ikiwa barabara ndogo tu kutoka pale Uondwe mpaka Nyali nilipokwenda Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ajili ya kuomba msaada wa kutia kifusi, basi ilibidi tutoe shilingi milioni 23.

Je, masikini hawa waliopo katika nchi hii wana uwezo gani wa kutoa milioni za fedha na kuweza kutia kifusi barabara zao, wakati wizara ipo na tunaipitishia bajeti ya kutosha kwa ajili ya kufanya kazi hiyo na kama hakuna wanakwenda kutafuta misaada popote pale kama wizara nyengine zinavyofanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, napenda tena kulikumbusha Baraza lako tukufu pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi kwamba majukumu ya msingi ya kujenga barabara hizi za ndani ni majukumu ya Halmashauri pamoja na viongozi husika wa majimbo. Wizara yetu ya Miundombinu na Mawasiliano iko tayari kutoa kila aina ya ushirikiano ikiwa pamoja na vifaa na mafundi.

Hivyo basi sababu anayoieleza Mhe. Mwakilishi kusema kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko wameshaanza, kwa nini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano isikamilishe zoezi hilo.

Mhe. Spika, majibu ni kwamba kwenye bajeti yetu sisi hatuna fedha za kufanya ukarabati huo, isipokuwa kilichopo sisi tupo tayari kutoa kila aina ya ushirikiano kwa kuwapa vifaa na mafundi. Kwa kweli tungekuwa na fedha kwa mujibu wa bajeti yetu basi tusingeona tabu wala shida kukamilisha miradi hiyo.

Tunachoendelea kuwasisitiza viongozi wenzetu kwamba tuendelee kuzikamata halmashauri zetu kwa kutambua kwamba wao ni wa bia na washirika wakubwa katika kuleta maendeleo hasa ya barabara vijijini.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba akubaliane na rai ya serikali kuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iendelee na zoezi la kuratibu barabara kubwa na barabara hizi ndogo ziendelee kuratibiwa na halmashauri zetu.

Aidha tutaendelea kuwaomba wenzetu wa Mfuko wa Barabara pamoja na kuwa na madhumuni yao makubwa ya kuendeleza barabara kubwa, lakini tutawaomba kadri hali inavyoruhusu kusaidia barabara ndogo hizi, ili kuondosha changamoto ya usumbufu ya usafiri kwa wananchi wetu walioko vijijini.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Barabara ya Wete – Chakechake kupitia njia kongwe imechimbika sana na barabara hii tulishuhudia ikitiwa viraka kwa ajili ipitike, lakini baadaye kwa muda mfupi walisitisha kutia viraka kwa sababu kuna azma ya kujengwa.

Je, barabara hii ile azma ya kujengwa ipo na kama ipo lini itaanza kujengwa.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru sana na kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake, isipokuwa tupo wawili basi tunasaidiana.

Ni kweli njia ya Chake – Wete tayari iko katika mchakato wa kujengwa upya kwa mkataba na mkandarasi maalum, lakini mchakato wake bado haujakamilika. Mhe. Spika, mwanzo ilionekana kwamba usitishwe utengenezaji ule wa kutia viraka, ili kuondoa ile gharama ya ziada ambayo ingefanyika mara ya pili inakuja kuchimbuliwa.

Mhe. Spika, napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba kulitokezea matatizo ya kuharibika kwa mitambo miwili ya lami na uchimbuaji kokoto, kwa sababu ya umeme. Kwa kweli mashine zote mbili hizi zilikuwa zikitumia majenereta ambayo yalifeli kwa kipindi kimoja.

Kwa hivyo, utaratibu wa kupeleka umeme katika Kware ya Vitongoji tayari umeshakamilika na mitambo yote miwili hivi sasa inafanya kazi, kwa maana hiyo ile njia ya Wete – Chakechake itaendelea kufanyiwa matengenezo ya kutiwa viraka mpaka hapo ukandarasi utakapokamilika.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na kwanza namshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Mhe. Spika, serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kuboresha miundombinu ya barabara ya Kijichi Jimbo la Bububu.

Kwa kweli imefanyiwa miundombinu ya misingi pembeni ya barabara hiyo, lakini cha kusikitisha zaidi misingi hiyo imeachwa hivyo hivyo kwa muda mrefu. Je, Mhe. Naibu Waziri wizara yako ina mpango gani wa kumaliza misingi hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, samahani huku mwisho sikusikia vizuri.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, ni hivi njia ya Kijichi kuna misingi ile ambayo imetengenezwa, lakini imeachwa. Je, wizara yako ina mpango gani kuitengeneza misingi hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, katika mradi wetu wa pili chini ya Mfuko wa Barabara tulikuwa na maeneo ambayo tunaita *sport chronic*, kwamba yale maeneo ambayo barabara ilikuwa ina kawaida ya kutuwama maji na kuchimbuka likiwemo Kituo cha Polisi Mfenesini, eneo la Bububu baada ya Kituo cha Polisi na Maeneo mengine. Kwa hivyo, tulichokubaliana na wenzetu wa Mfuko wa Barabara ni kutafuta namna ya kuondoa maji ndipo ikaja hiyo dhana ya kuchimba michirizi.

Mhe. Spika, ninachomuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba zoezi lile halijakamilika na ni jambo ambalo ni endelevu. Kwa mfano, hivi sasa ukipita eneo la Bububu tayari tumeshapanusuru, barabara ya Kijichi tunakwenda nayo na tunahakikisha kwamba mitaro ile inakamilika kuchukua maji kuyapeleka baharini, ili kunusuru barabara zetu kama tulivyokusudia.

Mhe. Spika: Mhe. Naibu Waziri, tunakushukuru. Waheshimiwa Wajumbe kabla ya kuendelea nimeombwa kuna wageni pale niwatambulishe kwenu,

wageni hawa wako watatu nao ni wageni wanaohusiana na Kampuni ya *Synchronal Waste Management Corporation Limited*. Kampuni hii inahusiana na usindikaji wa taka kwa ajili ya kuzalisha umeme. Baada ya kazi nzuri sana mlioifanya Waheshimiwa Wajumbe kupitisha ule mswada wa *ZURA* sasa watu wanajitokeza ili kufanya utafiti juu ya njia nyengine mbadala ya kuzalisha umeme.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amewatafuta ndugu zetu hawa ili waje kwa mazungumzo na hatimaye kufanya huo utafiti juu ya masuala ya usindikaji wa taka kwa ajili ya kuzalisha umeme. Kwa hivyo, naomba niwatambulishe kwenu wageni wetu hawa watatu waliofika nao ni:

1. Mikel Olivia, huyu ni mgeni kutoka Afrika ya Kusini ambaye yeye ni *director* wa *Synchronal South Africa.*
2. Seif Olivia , vile vile ni kutoka Afrika ya Kusini naye ni Mkurugenzi pia wa Shirika hilo la *Synchronal*.
3. *Engineer* Johns Tyuku Mbuji, huyu ni Mtanzania yeye ni Mkurugenzi wa Shirika hilo kutkoa hapa *Tanzania Synchronal, Tanzania Limited* Tanzania.

Kwa hivyo, ndugu wageni wetu *you are most welcome to our house to see what is going on here, you are most welcome.* Waheshimiwa Wajumbe hao ndio wageni wetu ambao wamefika kuja kuona shughuli zetu na wametaka muwatambue na tunawakaribisha sana Waheshimiwa Wajumbe. Karibuni sana, ahsanteni sana.

KAULI YA SERIKALI

Taarifa ya Ziara ya Rais wa China Mhe. Xi Jinping

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, Kanuni za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012 katika kanuni ya 43 na 44 zinazungumzia vitu viwili, kanuni ya 43 inazungumzia Kauli za Serikali na kanuni ya 44 inazungumzia Taarifa ya Serikali. Mhe. Spika, kuna taratibu tofauti zinazoongoza shughuli hizo mbili, sasa nimenyanyuka kuhusiana na utaratibu Mhe. Spika, kwa sababu Taarifa ya Serikali inaruhusu kujadiliwa hata kama ni kwa muda mfuli utakaouweka lakini inaruhusu kujadiliwa na kwa suala hili ambalo liko mbele yetu nadhani Wajumbe wengi wana shauku kubwa ya kulichangia kuliko kuuliza maswali ambao ndio utaratibu wa Kauli za Serikali.

Mhe. Spika, nimetaka nisimame kuhusu utaratibu na kuomba muongozo wako kwa sababu kwa mujibu wa *order paper* tuliyopewa leo katika Hati za Kuwasilisha Mezani kumetajwa Hotuba ya Kuwasilisha Taarifa ya Ziara ya Rais wa China, Mhe. Xi Jinping nchini Tanzania tarehe 24-25 Machi, 2013. Lakini ukija ukurasa wa tano wa *order paper* pale juu kuna Kauli ya Serikali kama ni kichwa cha maneno, lakini maelezo yanayofuata chini yake bado yanasema Taarifa ya Ziara ya Rais wa China Mhe. Xi Jinping nchini Tazania tarehe 24 hadi 25 Machi, 2013.

Sasa Mhe. Spika, nimeona nizitaje hizo tupate muongozo wako, kwa sababu kama ni taarifa kama inavyojieleza yenyewe ukiondoa haya maelezo kwamba yamekuwa chini ya kifungu cha Kauli ya Serikali, Wajumbe wako tungependa hata kama ni kwa muda wa saa moja kupata nafasi hata kama kila Mjumbe utampa dakika tano tano kuchangia kuliko kuuliza maswali kutokana na umuhimu wa taarifa hii ambayo imesemwa.

Pia ningeomba Mhe. Spika, kwa sababu kwa jumla kanuni ya sita(6) fasili ya pili inatoa mamlaka na naomba niisome inasema, "Spika ataongoza kila kikao cha Baraza na ndiye mwenye mamlaka ya kuamua kwa mujibu wa sharti ya kanuni hizi mambo yanayoweza kuzungumzwa ndani ya Baraza", basi utumie mamlaka yako hayo kubadilisha hii kama alivyokusudia Mhe. Waziri katika maelezo yake kwamba hii ni taarifa sio kauli ya serikali utupe nafasi japo muda mdogo tuweze kujadili. Naomba muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe Spika: Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Waziri aliombwa wakati fulani wakati tunachangia miswada mbali mbali na kama sikusahau nadhani alikuwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ndiye aliyeuliza jambo hili. Pia hata kwenye maswali na majibu likajitokeza tena suala hili kwamba, hivi serikali haitupi taarifa yote kuhusu ujio wa Mhe Rais wa China aliyekuja hapa Tanzania? Hivi kuna jambo gani ambalo sisi kama Zanzibar tumekubaliana naye ili tuweze kujua sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, inaelekea pengine zilipatikana taarifa kupitia kwa vyombo mbali mbali vya habari kwamba Rais wa Zanzibar alipata muda maalum akifuatana na baadhi ya mawaziri wake kuzungumza mambo mbali mbali yanayohusu maendeleo ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Waziri baada ya jambo hili kujitokeza humu ndani katika michango fulani na pia kwenye maswali akaona ni muhimu basi serikali itoe kauli yake juu ya ujio wa Rais yule na mambo ambayo yamezungumzwa. Mimi nadhani kufikia pahala tujadili kitu ambacho pengine hata mikataba haijatiwa saini sasa hiyo nayo itakuwa ni jambo ambalo sijui tunakusudia kufanya *pre-emption, I don't know*, hilo si jambo jema, tuachie vyombo vyetu vya serikali vifanye kazi yake. Lakini Waheshimiwa Wajumbe mliomba

mpate habari kuhusu ujio wa Mhe. Rais wa China mpya ili tuweze kujua Zanzibar imejipangaje kuhusiana na masuala ya maendeleo mbali mbali kwa ushirikiano na wenzetu wa China.

Mhe. Waziri kaona kwamba basi inafaa tupeleke habari hii kwenye Baraza ili Waheshimiwa Wajumbe wajue. Hatua kwa hatua tena huko kama kutakuja jambo la mjadala hiyo itakuja baadae, lakini kwa kweli hivi sasa atoe kauli ya serikali juu ya ujio wa Mhe. Rais wa China na mambo ambayo labda wamekubaliana.

Kwa hivyo, mimi nakubaliana na hivyo, ije namna hiyo, tusichukue hatua ya kujadili tukaja tukafanya **pre-emption** ikaharibu mahusiano na mipango ambayo serikali imepanga na wenzetu hawa wa China. Naomba Waheshimiwa Wajumbe mkubali itolewe kauli hapa na kwa sababu hiyo basi naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kabla hujamruhusu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutoa Taarifa ya Serikali mimi kidogo nilikuwa nataka muongozo wako Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika hii *order paper* imeeleza utaratibu mzima wa shughuli za leo, lakini nikija katika kifungu cha nne Taarifa za Serikali kuna Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kuna Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi halafu kuna Waziri wa Nchi, Ofisis ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Halafu inafuata (b) hatua ya pili atakuja Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, atakuja Waziri wa Katiba na Sheria. halafu inayofuata Taarifa za Kamati hatua ya kwanza Mwenyekiti wa Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Sasa Mhe. Spika, nahisi kama hii mijadala tutakuja kuichanganya na tutajichanganya, kwa sababu kwa kuwa hizi taarifa zilikuwa zinaowana mimi nadhani tungekwenda kama mtiririko wa jana ulivyokuwa, kwamba waanze mawaziri kama walivyoelezewa halafu baadae imalizie Ripoti ya Mwenyekiti kutoa majumuisho ili kwa upande wa wizara hizi tuwe tumeshamaliza kazi, halafu baadae tena tuendelee na hizi wizara nyengine. Lakini vyenginevyo tukisema kwamba Waheshimiwa watoe maelezo yao halafu waje mawaziri wa wizara nyengine, halafu turudi tena tuje tuzungumze mambo ya wizara zile zile mimi nafikiri Mhe. Spika, nilikuwa naomba tufanye marekebisho, ili wakishamaliza mawaziri watatu ambao kamati yangu inasimamia baadae

nimalize mimi mwenyewe halafu tuendelee na wizara nyengine. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nataka nikiri anachokisema Mhe. Mwenyekiti wa Kamati inayoongoza Ofisi za Viongozi Wakuu, lakini kumekuwa na dharura inayomhusu Mhe. Waziri na ameniomba basi tumpatie nafasi hiyo kwa sababu kuna dharura muhimu ya safari ya kikazi kwa ajili ya masuala yetu ya maendeleo. Nilimwambia kwamba basi tukuweke mwisho itapokuja Wizara ya Fedha ili tufanye hivyo, lakini ikawa hiyo inatuletea tatizo kidogo kwa sababu Kamati ya Mwisho ni Kamati ya *PAC* na Kamati ya *PAC* ina wizara karibu zote, ina mambo mengi. Sasa ili tusije tukachanganya mambo mengi na kwa sababu Mhe. Waziri anataka aondoke aende safari ya kikazi kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar, nataka nirudie kwa ajili ya maendeleo ya Zanzibar, tukaona basi jambo hili ambalo halichukui muda mrefu tulipatie nafasi amalize tuendelee na shughuli nyengine na kipindi hicho aje aendelee na shughuli hiyo inayohusu masuala ya *PAC* ambayo itachanganya pamoja na wizara nyengine zote ambazo atakuwa na mambo ya kuzungumza.

Sasa hii imekuja kwa sababu ya dharura, lakini vyenginevyo unavyosema ilikuwa tumalize shughuli hii halafu tena tuendelee na nyengine. Lakini dharura iliyotufika inabidi tupangue kidogo shughuli zetu ili tumpatie nafasi hiyo. Naomba mpokee utaratibu huu kwa sababu ndio hali halisi tuliyonayo na muda wetu kimsingi ni finyu sana. Nyote mnaelewa hilo kama vile ambavyo tulikuwa tumekubaliana huko nyuma.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa Kauli ya Serikali juuya ziara ya Rais wa China Mhe. Xi Jinping iliyofanika nchini Tanzania tarehe 24 na 25.

Mhe. Spika, mnamo tarehe 24/3/2013 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka historia baada ya kumpokea Rais mpya wa Jamhuri ya Watu wa China Mhe. Xi Jinping ambaye alifanya ziara ya siku mbili hapa nchini. Mhe. Spika, nimesema Tanzania imeweka historia mpya kutokana na kwamba Mhe. Xi Jinping baada ya kuapishwa mnamo tarehe 14/3/2013 ziara yake ya kwanza ilikuwa nchini Urusi na ya pili ni Tanzania. Hii ni kusema kwamba Tanzania ni nchi ya kwanza katika Bara la Afrika kuitembelea mara tu baada ya kuapishwa kuwa Rais wa China.

Mhe. Spika, nchi ya China na ya pili yenye uchumi mkubwa duniani baada ya Marekani. Ujio wa Rais wa China hapa Tanzania tumeupokea kwa furaha kubwa sio tu kwa kuwa China ni nchi ya pili kuwa na uchumi mkubwa

duniani, bali ni kutokana na udugu wetu wa miaka mingi. Wakati China bado haijaendelea kiuchumi kwenye miaka ya 60 na 70 Zanzibar na Tanzania kwa ujumla tayari zimeshaanza kufaidika na misaada mbali mbali kutoka China. Mfano, ujenzi wa Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba, Kiwanda cha Sukari Mahonda, Uwanja wa Amani, Kiwanda cha Viatu Mtoni na kwa upande wa Tanzania Bara Njia ya Reli ya Tazara, Kiwanda cha Urafiki na kadhalika.

Mhe. Spika, ziara ya Rais wa China nchini Tanzania ilikuwa na malengo makuu yafutayo:

1. Kujitambulisha kwa Watanzania akiwa Rais mpya wa China
2. Kuangalia jinsi ya kukuza mashirikiano baina ya Tanzania na China
3. Kusaini mikataba mbali mbali ya kimaendeleo.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine ziara ya Rais wa China imechukuliwa kuwa ni njia moja ya kuimarisha mahusiano ya kiuchumi baina ya Tanzania na China. Kwa maana hiyo, ujio wa Rais wa China pia umeimarisha mahusiano hasa katika masuala ya uwekezaji na biashara.

Mhe. Spika, wakati wa ziara ya Rais wa China nchini Tanzania tumeshuhudia pia kusainiwa mikataba 17. Kati ya hiyo, mikataba mitatu ni kwa ajili ya kuisaidia Zanzibar na 14 ni kwa ajili ya Tanzania Bara. Mikataba iliyosainiwa kwa ajili ya kuisaidia Zanzibar ambayo Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alisaini kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kama hii ifuatayo:-

Kwanza mkataba wa kuisaidia Zanzibar Yuan milioni sitini sawa na US$ milioni kumi, fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu pamoja na huduma za jamii kutegemeana na makubaliano na Serikali ya China.

Pili, msaada wa ujenzi wa Hospitali mpya ya Abdalla Mzee iliyoko Mkoani Pemba. Hospitali hii ilijengwa kwa msaada wa China mnamo mwaka 1969/70. Ujenzi mpya utatoa nafasi ya kuongeza kwa vitanda kutoka 80 vya sasa hadi kufikia 160 pamoja na kuipatia vifaa mbali mbali vya kisasa vya uchunguzi kama vile *Scanner, Ultra-sound* na kuwa na vifaa vya *ICU*. Hatua hii ya ujenzi mpya itaifanya hospitali ya Mkoani kuwa ni Hospitali ya Rufaa kwa upande wa Pemba na ya Mkoa kwa Mkoa wa Kusini Pemba. Aidha, hatua hii itasaidia sana kuongeza idadi ya madaktari watakaokuja kutoka China.

Tatu, mktaba wa tatu uliotiwa saini ni msaada wa *scanner* mbili kwa ajili ya kutuwezesha kutambua bidhaa mbali mbali zitakazokuwemo ndani ya

kontena, *scanner* hizi zitawekwa bandarini na taalamu kutoka China watakuja Zanzibar kuwafunza vijana wetu jinsi ya kuzitumia. Hatua ya kuwepo kwa *scanner* bandarini itasaidia kutambua vitu hatarishi vinavyoingizwa nchini.

Mhe. Spika, wakati wa ziara hiyo ya Rais wa China Mhe. Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alifanya mazungumzo na Rais wa China pamoja na ujumbe wake, katiak mazungumzo hayo Zanzibar iliwakilishwa na mawaziri watatu, ambao ni Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Aidha, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein akiongoza ujumbe wa baadhi ya mawaziri na makatibu wakuu kutoka katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pia alifanya mazungumzo na Rais wa China.

Mhe. Spika, mazungumzo ya Rais Kikwete na yale ya Dkt Shein suala kubwa lililozungumziwa ni mashirikiano ya kiuchumi hasa katika sekta ya ujenzi wa miundombinu, uimarishaji wa biashara, uendelezaji wa sekta ya elimu na afya pamoja na suala zima la uwekezaji na uwezeshwaji wa wananchi kiuchumi kwa lengo la kuongeza ajira kwa vijana.

Mhe. Spika, kwa upande wa mashirikiano ya kiuchumi Zanzibar imewasilisha miradi saba ambayo imegawika kwa mpango ufuatao:

Kwanza miradi iliyoombewa mkopo nafuu, mradi wa kwanza ni ujenzi wa bandari mpya ya Maruhubi au banda ya Mpigaduri. Mradi wa pili upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba na mradi wa tatu uimarishaji na upatikanaji wa maji safi na salama kwa Zanzibar pamoja na uimarishaji wa *ZAWA*.

Pili, miradi iliyoombewa misaada, wa kwanza ni uimarishaji wa Tume ya Mipango na ya pili *program* za kukuza ajira kwa upande wa Zanzibar.

Tatu miradi ya uwekezaji kupitia uwekezaji wa pamoja (*Public Private Partnership*). Kwanza uanzishwaji wa kituo cha kufundishia uvuvi, ya pili uwekezaji katika uvuvi wa bahari kuu viwanda vidogo vidogo kama vile *Agro Processing Industries, Assembling Industries* na kadhalika.

Mhe. Spika, ujenzi wa bandari mpya Maruhubi utakapokamilika utakuza sana biashara hasa kwa kutilia maanani kuwa Bandari ya Zanzibar inaweza kutumika kwa ajili ya bidhaa za mpito na hivyo kupelekea kukua kwa uchumi wa Zanzibar. Aidha, upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba utatoa nafasi ya ndege kubwa kuweza kutua Pemba na hivyo kuongeza idadi ya abiria na watalii watakaoitembelea Pemba. Pemba iko karibu sana na Mombasa Kenya,

kuwepo kwa uwanja wa ndege mkubwa kutatoa fursa kwa watalii kutoka Mombasa kuitembelea Pemba na kuangalia maeneo mbali mbali ya kitalii. Kukua kwa shughuli za utalii Pemba pia kutakuza ajira kwa vijana wa Pemba na hatimaye kupunguza makali ya umasikini.

Mhe. Spika, kama tunavyoelewa mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato letu la Taifa ni mdogo, hali hii imetokana na kwamba bado hatujawekeza zaidi katika sekta hii. Kutokana na kwamba Sekta ya Uvuvi ina nafasi kubwa ya kuchangia katika pato la taifa na kwa kuwa China ina utaalamu mkubwa wa uvuvi wa bahari kuu pamoja na ufugaji wa samaki, serikali imeona ni vyema kuanzisha mashirikiano ya kibiashara na China katika Sekta hii ya Uvuvi na ujenzi wa viwanda vya kusindika samaki pamoja na viwanda vidogo vidogo. Wafanyabiashara wa China wana uwezo mzuri wa kuanzisha viwanda vidogo vidogo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, miradi hii na mingineyo inayoangaliwa kwa mashirikiano na taasisi mbali mbali za kimataifa inalenga tu sio kukuza uchumi, bali pia kuongeza ajira kwa vijana wa Kizanzibari.

Mhe. Spika, majadiliano juu ya miradi hiyo niliyoitaja baina ya wataalamu weu na wale wa China yanaendelea na kwa kiwango kikubwa tulitarajia utiwaji wa saini juu ya makubaliano kutofautia mara tu baada ya kukamilika majadiliano baina ya serikali yet na Serikali ya China.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa sasa naomba kwa ruhusa yako kuwasilisha taarifa hii mbele ya Baraza lako tukufu ahsante sana naomba kuwasilisha.

Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekit wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii kama ulivyo utaratibu niweze kutoa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kifupi tu kuhusu ziara hii ya Mhe. Rais wa China, Mhe. Xi Jinping aliyoifanya nchini kwetu Tanzania tarehe 24 na 25 mwaka huu wa 2013.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii ya Fedha Mhe. Omar Yussuf kwa kutupa taarifa juu ya ziara hii muhimu ya Rais wa China kuitembelea Tanzania, taarifa ambayo sisi tukiwa Wawakilishi wa wananchi tunapaswa kuifahamu.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mhe. Waziri kwamba, ziara hii imejenga historia mpya Tanzania. Kweli sote ni mashuhuda kwamba tumejenga historian a kwa sababu Mhe Rais wa China baada ya kuapishwa

basi ziara yake ya kwanza katika Bara la Afrika ameifanya hapa Tanzania. Kwa hivyo, hii ni historian a kwa sababu China ni marafiki sana wa Zanzibar na tunakumbuka kwamba miongoni mwa nchi ambazo zimeyatambua Mapinduzi ya Zanzibar mwanzoni ni ndugu zetu wa Serikali ya China. Ambapo baada ya Mapinduzi ya tarehe 12 January, mwaka 1964 basi China haikusita kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, hawa ni rafiki zetu, ni wenzetu, ni ndugu zetu wa damu, hivyo tunapaswa kujivunia urafiki wetu huu kati yetu Tanzani hususan Zanzibar.

Mhe. Spika, ziara hii ya Mhe. Rais wa China imeelezwa na taarifa kwamba iligusa zaidi maeneo matatu, au ilikuwa na malengo matatu ambayo Mhe. Waziri ameeleza kuwa kujitambulisha kwa Watanzania kwamba yeye ni Rais mpya wa China, lakini kuangalia jinsi ya kukuza mashirikiano baina ya Tanzania na China. Pia kusaini mikataba mbali mbali kama ilivyosema taarifa mikataba ya maendeleo.

Lakini kwa upande mwengine imechukuliwa kuwa ni njia pekee ya kuimarisha mahusiano ya kiuchumi baina yetu Tanzania na China, hasa katika maeneo ya uwekezaji.

Mhe. Spika, maeneo yote yaliyozungumzwa ya mashirikiano ni muhimu lakini katika eneo zaidi hili la uhusiano katika masuala ya uwekezaji na biashara ni muhimu zaidi katika kukuza uchumi wetu. Na hapa kwetu katika maeneo haya ndipo penye matatizo. Mhe. Spika, tumeshuhudia wawekezaji wengi wanafika kwetu Zanzibar kwa ajili ya kuwekeza lakini matatizo tuliyonayo ni suala zima la urasimu katika maeneo ya uwekezaji. Urasimu ambao unasababisha wawekezaji wengi washindwe kuwekeza.

Sasa maoni ya Kamati kwamba, juu ya maeneo haya tuondoshe urasimu katika suala zima la uwekezaji. Wenzetu wa China wanataka kuwekeza lakini tukiendelea kuwa na urasimu katika maeneo ya uwekezaji huku tukitaka kwamba kabla ya kuidhinisha mradi huo tupate chochote kitu, basi miradi hii haitoweza kufanikiwa. Kwa hivyo suala la kwamba mimi nitapata nini katika mradi huu hilo tuachane nalo kabisa, lazima tuone kwamba miradi hii kama itakuwa imekamilisha taratibu zake inapitishwa kwa manufaa ya wananchi. Kwa hivyo tuangalie zaidi kwamba Tanzania au Zanzibar itapata nini kuliko kuangalia kwamba mimi nitapata nini. Hilo haliwezi likatusaidia.

Mhe.Spika, taarifa ya Mhe. Waziri imetueleza kwamba kuna mikataba 17 ambayo Mhe. Rais wa China ambayo amesaini kwa niaba yetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mikataba mitatu inahusu Zanzibar. Kuna mkataba wa karibu *Yuan* milioni sitini ambapo fedha hizo ni kwa ajili ya

kuimarisha miundombinu pamoja na huduma za kijamii kutegemea na makubaliano.

Na mradi mwengine au mkataba mwengine ni msaada wa hospitali hii mpya ya Abdalla Mzee ambapo kuna mambo mengi yatafanyika katika hospitali hiyo. Na mkataba mwengine ni kwa ajili ya vyombo hivi vya kisasa ambapo Mhe. Waziri ameeleza vya kuangalia makontena kwamba kuna kitu gani ndani yake.

Makubaliano hayo Mhe. Spika, au mikataba hii ni muhimu kwa sababu itaiwezesha nchi yetu kuweza kutatua mambo mbali mbali. Hospitali ya Abdalla Mzee Pemba inahitaji kuwa ni hospitali ya rufaa kama Mhe. Rais alivyosema Rais wetu wa Zanzibar alivyosema kwa ajili ya wananchi wa kule na kuweza kupata huduma mbali mbali lakini hili suala la kuangalia vifaa viliomo ndani ya makontena litasaidia sana kwa wale wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi, na kwa sababu tunajua kwamba maeneo yale ya bandarini wafanyabiashara huwa wanayatumia zaidi katika suala zima la ukwepaji wa kodi. Kwa hivyo kama kwenye *container* kutajulikana kuna nini basi inakuwa ni rahisi kwa watu wetu watoza ushuru kujua ni namna gani ya bidhaa zilizomo na kiasi gani cha kodi kinahitajika kulipa katika bidhaa hizo

Lakini jengine Mhe. Spika, Mhe. Rais wa China amefanya mazungumzo na Rais wa Zanzibar na baadhi ya Mawaziri na Makatibu Wakuu na katika mazungumzo hayo yalihusu zaidi masuala ya uchumi na kwa bahati Mhe. Spika, serikali imewasilisha miradi saba na kama alivyo Mhe. Waziri imegawika kwa mpangilio kama alioueleza. Kuna miradi iliyoombewa mkopo nafuu ambapo imezungumziwa kwamba kuna mradi wa ujenzi wa bandari mpya ya Maruhubi na Mpiga Duri lakini upanuzi wa uwanja wa ndege wa Karume. Lakini na tatu uimarishaji wa upatikanaji wa maji safi na salama kwa Zanzibar pamoja na uimarishaji wa ZAWA.

Mhe. Spika, maeneo haya ni maeneo muhimu sana kwa ajili ya uchumi wetu wa Zanzibar. Lakini kwa kweli yametutonesha vidonda kwa hivyo tuitake serikali kuwa makini katika maeneo haya. Suala la upanuzi wa uwanja wa ndege wa Karume na suala la upanuzi wa uwanja wa ndege wa Zanzibar na kujenga *terminal* 2 pale ambao umekwama na ilhali ndugu zetu hawa hawa Jamhuri ya China wametupatia zaidi ya dola milioni sabiini kwa ajili ya kupanua uwanja wa ndege na hadi leo hii umekwama. Na sasa serikali inawasiliana na wenzetu wa China katika miradi kama hii ya upanuzi wa uwanja wa ndege wa Karume Pemba. Lakini ikiwemo pamoja na ujenzi wa bandari mpya ya Mpiga Duri kwa kweli mambo haya serikali inahitaji kuwa makini yasije yakatokea kama yaliyotokea uwanja wa ndege. Kwa kweli Mheshimiwa suala la ujenzi wa *terminal* 2 katika uwanja wa taifa wa Abeid

Aman Karume linatutia unyonge. Na linatutia unyonge kwa sababu fedha kwa ajili ya utanuzi ule zipo na hakuna linaloendelea.

Kwa hivyo tumefanya mashauriano na Rais juu ya miradi 7 na miradi muhimu tunaiomba sana serikali isimamie vyema miradi hii itakayoanzishwa ili tuone kwamba inakamilika. Lakini donda jengine kubwa zaidi ni juu ya suala la uimarishaji wa upatikanaji maji safi na salama Zanzibar ambapo mradi mkubwa wa Mkoa wa Mjini Magharibi ambao uligharimu zaidi ya bilioni 30 ambapo wenzetu walituahidi kwamba mradi huu utakapokamilika kutokana na msaada wa wenzetu wa Jamhuri ya Japan, basi Mkoa wa Mjini Magharibi utakuwa hauna tatizo tena la maji. Lakini tunalolishuhudia kwamba bado Mkoa wa Mjini Magharibi una matatizo makubwa ya maji mbali ya fedha nyingi za walipa kodi kwa wananchi wa Japan zilizotumika katika kutatua matatizo ya maji.

Mhe. Spika, ni lazima tuwe *serious* katika mambo kama haya wenzetu wapo tayari kutusaidia na wanatuangalia na wanaona tunafanya nini. Kwa hivyo tujitahidi kuona kwamba mambo haya mazuri ambayo wenzetu wanatuletea tunayasimamia na kuona kwamba yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara tunaunga mkono taarifa hii ya Mhe. Waziri na tuwatakie kila la kheri katika maazimio haya ambayo yamepangwa na Mwenyezi Mungu atatusaidia. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, asubuhi hii ya leo kunipa nafasi kuchangia ripoti ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa, naomba nimuulize swali Mheshimiwa wangu Waziri katika ripoti yake ambayo nzuri sana na hasa leo Ijumaa na alivyotia kanzu kubwa amesema kuwa kuna miradi 17, lakini miradi 3 ndio ya Zanzibar je, Mhe. Waziri huoni kuwa kupewa miradi 3 Zanzibar tumepunjwa haki yetu kwa kuwa hawa ni wapenzi wetu?

Lakini pili Mhe. Waziri huoni kama iko haja sasa hivi na sisi Mhe. Rais kama alivyosema hapa Mnadhim wangu Mwenyekiti wa Kamati hiyo ni wapenzi wetu tangu asili na jadi tangu wakati wa Mapinduzi ya Zanzibar ni watu wa mwanzo waliotuunga mkono huoni kama iko haja sasa hivi kuwaita wakaja tena *special for* Zanzibar huoni ipo haja hiyo?

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba nimuulize maswali manne mafupi sana Mhe. Waziri ili anielimishe.

Mhe. Spika, kwenye taarifa hii kama alivyosema mwenzangu miradi ambayo iliwasilishwa na kutiwa saini ni 17 na 3 ndio ambayo ilikubaliwa kwa Zanzibar. Naomba kujua miradi yote 17 ilikuwa na thamani ya kiasi gani cha fedha na asilimia ngapi Zanzibar walipata kwenye thamani hiyo.

Mara nyingi wenzetu SMZ na wafadhili wanapotiliana mikataba kampuni za ndani ya nchi zao huchukua nafasi ya kukusanya miradi hii. Kwa mfano hapa Zanzibar mara nyingi Kampuni ya CRJE ya Kichina ndio inayofanya kazi. Je, mradi huo wa ujenzi wa miundo mbinu nao pia atapewa huyo CRJE.

La tatu, Mhe. Spika, wakati SMZ inapeleka mradi wa upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Karume Pemba hivyo SMZ waliwahi kumwambia huyo Rais kwamba Uwanja wa Ndege wa Unguja umefeli au wamenyamaza kimya.

Mwisho ni nani aliyewaalika Rais na Mawaziri waliopo Zanzibar ni Rais Kikwete au Rais wa China ndio aliyewaalika kwenda kule Dar es Salaam.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali nadhani na mimi kama manne kwa Mhe. Waziri.

Kabla ya kuuliza swali kwa nusu dakika tu nimwambie Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kwamba taarifa yake ingependeza zaidi kama ingelikuwa kama ina maelezo ya utangulizi yaliyokuwa yakielezea msingi wa mahusiano kati ya Zanzibar na China. Nadhani ni muhimu sana kuwepo katika *records* za Baraza. Baada ya tanbihi hiyo Mhe. Spika, na mimi naomba niulize maswali yafuatayo:

Kwanza, katika taarifa yake Mhe. Waziri katwambia kwamba kulikuwa na miradi au mikataba iliyotiwa saini ya miradi 17 ambapo Zanzibar ilipata 3. Mbali ya swali ambalo ameliuliza mwenzangu Mhe. Hija mimi nilikuwa namuomba kama anaweza kutusaidia mbali ya hii 3 aliyotutajia ya Zanzibar je anaweza kututajia na ile miradi mengine 14 ambayo ilikuwa inahusu upande wa Tanganyika katika miradi hiyo?

Lakini la Pili Mhe. Spika, naomba nimuulize katika hii miradi 3 ambayo ameiorodhesha ya Zanzibar kuna mradi wa kwanza umetajwa huku kwamba mkataba wa kuisaidia Zanzibar Yuan 60 milioni sawa na dola za kimarekani milioni10 fedha hizi zinatumika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu pamoja na huduma za jamii kutegemeana na Serikali ya China. Nakumbuka kwa kipindi cha takriban mwaka tu lakini ni miezi kadhaa nyuma tuliwahi kumsikia Mhe. Waziri wa Fedha akitangaza msaada wa kima kama hiki cha fedha, sasa nataka kujua je ule msaada alioutangaza wakati ule ndio huu huu ambao tumeambiwa sasa umetiwa saini ama hii ni nyongeza nyengine zaidi

ya zilizokuwa zimetajwa wakati ule milioni kumi. Na kama ni hivyo kwangu mimi naona kumbe hatukupata kitu kipya.

Lakini la tatu, Mhe. Spika, naomba na mimi niulize hili thamani ya miradi *interest* kulijua lakini la tatu nataka kuuliza katika taarifa yake Mhe. Waziri ametaja mazungumzo haya ambayo yalifanyika na miradi hii ambayo Zanzibar imewasilisha. Mhe. Spika, katika miradi ambayo imetajwa kwamba imeombewa mkopo nafuu; *concessional loan* kwa kuanza ujenzi wa Bandari mpya ya Maruhubi au Mpigaduri.

Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba katika Baraza hili hili niliwahi kuleta swali la msingi ambalo lilijibiwa na Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu, lilionesha kwamba mradi kama huu ulipopelekwa kupitia benki ambayo serikali ya Jamhuri ya Watu wa China inayotumia kutoa mikopo kama hii yaani Exim Bank of China iliongeza mno thamani ya mradi kufikia dola milioni 800 wakati baada ya kufanya uchunguzi Wizara ilijiridhisha kwamba thamani halisi ilikuwa ni dola milioni 400 tu kwa kiwango kama kile cha Bandari kutoka katika nchi nyengine kama Uholanzi.

Sasa je, swali langu ni kwamba kwa kukimbilia mikopo hii ambayo baadae inawagharimu sana walipa kodi kwa sababu haya ni madeni kuwa juu ya vichwa vya wananchi wa Zanzibar walipa kodi kwa miaka mingi, hatuoni kwamba tulipaswa kufikiria upya kupeleka mradi huu kwa Wachina baada ya kuonekana thamani pale mwanzo ilizidishwa mara dufu mara mbili ya thamani yake halisi?

Mhe. Spika, la mwisho kabisa katika masuala yangu nilikuwa naomba kumuuliza Mhe. Waziri kwamba katika mazungumzo yake aliyotwambia hapa katwambia kulikuwa na mazungumzo yaliyomhusisha Rais wa Jamhuri ya Muungano na mazungumzo yaliyomuhusisha Rais wa Zanzibar na timu yake. Nilikuwa naomba kujua kwamba huu utaratibu wa itifaki umetokana na msingi upi Mhe. Spika, kwamba badala ya kuwa na mgeni akatembelea Zanzibar ameondoka Rais wa Zanzibar na jopo lake zima kwenda upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano kwenda kufanya mazungumzo na Rais anayetembelea nchi hii naomba kujua msingi huo wa itifaki umeanzia lini Mhe. Spika. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi nikamuuliza maswali mawili matatu Mhe. Waziri wa Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Spika, kwanza napongeza sana ziara ya Rais wa China Tanzania na tunamuomba Mwenyezi Mungu ziara hiyo ailetee faraja kubwa na matumaini katika nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nataka nimuulize kwanza Mhe. Waziri kwamba katika ripoti yake hii ameelezea misaada ambayo tuliyoipata mwanzo hospitali ya Abdalla Mzee, Kiwanda cha Sukari Mahonda na Uwanja wa Amani na Kiwanda cha Viatu Mtoni. Lakini vile vile katika ripoti yake akaelezea vile vile na misaada ambayo tunayotegemea kuipata pamoja na mikopo sasa masuala yangu yapo hivi.

Mhe. Spika, tumeona hapa katika hii mikopo nafuu kwamba kuna mazungumzo sasa yanaendelea ili kuupeleka mradi wetu wa Bandari ya Mpigaduri. Mhe. Spika, suala la bandari ya Mpigaduri ni suala ambalo linazungumzwa zaidi ya miaka 20 hivi sasa kwa Zanzibar. Sasa leo tumepata bahati hii tayari tumeshatia saini mikataba mbali mbali lakini sasa hivi ndio kwanza tunaanza kufanya tathmini na mazungumzo kuhusu mradi huu wa bandari ya Zanzibar.

Sasa swali langu lipo hapa je, Mhe. Spika, ugeni mkubwa kama huu katika matayarisho ya kuja kwake mawaziri wetu kwa upande wa Zanzibar au watendaji wetu ndani ya serikali yetu ya Mapinduzi Zanzibar walishirikishwa katika maandalizi wa ziara hii, na kama walishirikishwa katika ziara hii, suala la bandari la Mpigaduri ambalo limekuwa mdomoni zaidi ya miaka 20 kwa nini leo ndio ukaja ukawekwa ndio mradi wa mwisho ambao sasa ndio mazungumzo yanaanza. Wakati kuna bandari ambayo tayari Rais wa China alipokuja alipotia saini ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, bandari ile …..

Mhe. Spika: Tunaomba maswali Mheshimiwa, sasa toa swali usilete maelezo mengi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ndio swali langu nakuja hapo kwa nini bandari ambayo ilikuwa haikuzungumzwa miaka 20 iliyopita ndio ikaja ikatiwa saini na hii bandari ambayo ilitiwa saini miaka 20 iliyopita ndio kwanza ikawekwa katika hatua ya mazungumzo.

Lakini la pili Mhe. Spika, nilikuwa nataka niulize Mhe. Waziri atusaidie ufafanuzi hii aliyosema miradi inaombewa mikopo nafuu nini maana hasa ya mkopo nafuu ili tuweze kupata ufafanuzi wake.

Jengine Mhe. Spika, je, katika miradi hii ambayo tutakayopata mikopo ya China kuna masharti gani ambayo Wazanzibari watatakiwa wayafuate katika mikopo hii.

Mhe. Spika, katika fedha ambazo tulizozipata tumeambiwa hapa kwa ajili ya kusaidiwa, sasa katika miradi hii ambayo tutakayoitia saini kwa ajili ya kusaidiwa, je, hakuna mradi ule ambao tuliouzungumzia kuhusu suala la kuanzishwa benki ya wanawake pamoja na watoto wadogo.

Vile vile vipi kuhusu suala la uwanja wa Mao katika hii miradi ambayo tutakayosaidiwa hakuna sehemu yoyote ambayo uwanja wa Mao tutaweza kuufanyia ujenzi mkubwa na wao ukapunguza mzigo ambao unaobebwa sasa hivi na huu uwanja wa Amani. Ahsante sana.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kunipa fursa na mimi nimuulize Mhe. Waziri maswali.

Mhe. Spika, ninamuuliza Mhe. Waziri, Tanzania imepatikana jina Tanzania kwa muungano wa nchi mbili Zanzibar na Tanganyika. Kwa kuwa China ni marafiki wetu Zanzibar tangu zamani, na kwa kuwa Rais wa China amekuja Tanzania, kuna sababu ipi ya msingi viongozi wetu waende wakazungumze na Rais wa China Tanzania Bara asije Zanzibar na wakati Wazanzibari wanataka kumuona Rais wa China na wao wanataka kufaidika na maendeleo, kuna sababu ipi ya msingi mpaka asije Zanzibar.

La pili Mheshimiwa kwa sababu miradi ni 17 iliyotiwa saini lakini tumeona ni miradi 3 tu ya Zanzibar, hivi kulitumika vigezo gani kugawa miradi hii.

La tatu napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu tumeona katika mikataba kama kuna neno ukarabati wa hospitali ya Abdalla Mzee Pemba, je, ninamuuliza Mhe. Waziri ni ukarabati au kujenga hospitali mpya.

Swali la nne kwa kuwa Zanzibar tuna matatizo ya bandari yetu ni finyu ni ndogo na haiwezi kukidhi haja kuna haja gani ya wenzetu kukimbilia kwenda kujenga bandari ya Bagamoyo wasitujengee sisi Wazanzibari.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwanza Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri aniweke sawa kwamba Zanzibar iliomba miradi 7 kama alivyoiainisha hapa lakini miradi 7 hiyo iliyoombwa ambayo ni miradi ya kiuchumi na hapa napenda niipongeze serikali ya Mapinduzi kwa kuona kwamba tatizo letu ni uchumi lakini mikataba iliyotiwa saini ni miradi mitatu nje ya hii miradi 7.

Sasa hebu Mhe. Waziri tuwekee wazi hapa hii mitatu iliombewa lini na hii ikoje? Maana yake iliyoombewa ni 7 lakini mikataba iliyotiwa saini ni 3 ambayo ni nje ya hii 7 Mhe. Waziri tuweke sawa hapa. Na miradi hii mitatu iliyombewa nadhani haizidi zaidi ya dola 60 milioni. Wakati Bandari ya

Bagamoyo leo asubuhi nilikuwa nikifuatilia ni zaidi ya bilioni kumi ambayo mradi mmoja tutaona ni kiasi gani Zanzibar ilivyokuwa ni mnyonge katika muungano wetu.

Swali la pili, Mheshimiwa katika mahusiano ya kidiplomasia kando ya China ambapo Tanzania ina Balozi na ambaye Balozi wake sasa yupo, kuna balozi 8 za Tanzania sasa hivi hazina balozi na baadhi ya maafisa wa kibalozi. Kwa sababu Zanzibar ni mshiriki wa muungano je, Zanzibar inalijua hilo na kama inalijua ni kwa kiasi gani mshiriki huyo wa Muungano anakaa pamoja na walio na mamlaka ya kuteua katika kuhakikisha kwamba na Zanzibar inapata nafasi katika nafasi 8 pamoja na maofisa wa ubalozi.

Suala la mwisho Mhe. Spika, nafikiri serikali ya China ilitoa mualiko kwa maafisa wote waandamizi serikalini ikiwa ni pamoja na Mawaziri na Makatibu Wakuu na wengine. Na kule kwa kweli tulikwenda tukafundishwa mambo mbali mbali ya maendeleo ya maeneo huru. Naomba nimuulize Mhe. Waziri na Serikali, kati ya mambo ambayo tumejifunza ni yepi sasa hivi yamefanyiwa kazi na yepi ambayo hayajafanyiwa kazi.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka nikushukuru sana kwa muda huu kusaidiana na Wajumbe wenzangu katika kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya maswali ili sote kwa pamoja tuweze kufahamu ujio wa Rais wa China hapa Tanzania pamoja na muelekeo wetu wa baadae kama nchi au kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Nikianza basi Mhe. Dr. Salmin Awadh Mwenyekiti wa Kamati, yeye ameanza na kupongeza ujio wa Rais wa China lakini vile vile amesisitiza uwekezaji na suala la kibiashara, mahusiano yetu yapewe umuhimu mkubwa sana baina ya Zanzibar na China. Na kasisitiza hasa tatizo liliopo katika urasimu katika suala la utekelezaji. Nakubaliana Mhe. Mwenyekiti na mimi pamoja na mwenzangu tuliopewa dhamana nadhani hili tukiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais tutalisimamia kwa dhati ili tupunguze urasimu basi na ikiwezekana tuondoshe kabisa urasimu ili hawa wewekezaji waweze kuwekeza kwa faida yetu na kwa faida ya wananchi wetu.

Lakini la pili alisema suala zima la kuangalia zaidi mikataba, mikataba hii tunayotia saini ili baadae isije ikatuletea matatizo au kero kama ilivyotuletea *terminal* ya hapa katika uwanja wa ndege wa Zanzibar. Nataka nimuhakikishie kwamba serikali ya awamu ya saba, kwa ule uangalifu wake ndio imeliona kwamba *terminal* ina matatizo. Na katika haya ambayo

yanayokuja, tutahakikisha kwamba kuanzia siku ya kwanza tunaangalia mkataba pamoja na uwiano wa ujenzi ili tusije tukapata matatizo. Na nataka nikwambieni tu kwamba katika misaada ya China ambayo imeshaingia hapa Zanzibar katika awamu hii na utekelezaji wake ambao tunauona na tumeanza kuusimamia vizuri zaidi tunaanzia na taa za njiani na tumesimamia vizuri zaidi na tumeona baadhi ya *shortfalls* ambazo zilizomo katika taa hizi na tumeshaanza kulifanyia kazi. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba na mikataba mengine, hospitali ya Mkoani itakapoanza kujengwa tutaiangalia kwa dhati ili yale ambayo tuliyokubaliana ndio ambayo yanayokwenda *on the ground.*

Vile vile Mhe. Dr. Salmin ametutaka tuwe makini zaidi katika usimamizi. Hili nataka niwaambie mawaziri wenzangu kwamba tuwe karibu sana katika miradi yote sio ile inayosaidiwa na China tu, hata ile inayosaidiwa na taasisi nyengine au nchi nyengine. Kwa hivyo, kwa upande wa Dr. Salmin mimi namshukuru sana kwa maoni yake na kwa muangalizo wake, tutayasimamia na kwa bahati nzuri Makamu wa Pili wa Rais tunae ndani leo kwa hivyo na yeye atakamata usukani ili mawaziri twende pamoja naye.

Mhe. Makame Mshimba mbarouk shemegi yangu naye ametaka ufafanuzi katika maeneo mawili, amesema kupewa miradi mitatu katika 17 hatujavunjiwa hadhi? Nasema kwa udogo wetu na idadi yetu ya wananchi tulionao hii mikataba imekamilika ndio imetiwa saini, sisi tuna mikataba kama mitatu mine hivi iliyokuwa haijakamilika. Baada ya wenzangu kunijia nikawaambia hii haijakamilika isije ikatuletea matatizo ya kikatiba, tuiache tusaini hiyo iliyokamilika hii mingine tutasaini baadae.

Lakini nataka niwakumbushe tu ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi, Mhe. Ismail Jussa uliliona miezi sita iliyopita alikuja Naibu Waziri Mkuu wa China tulisaini vile vile mikataba mingine wakati wenzetu hawakusaini. Kwa hivyo sisi ki-*ratio* ukichukua idadi ya watu na mikataba tunayosaini *against* China sisi tunasaini mingi na katika kipindi kifupi. Na mimi ninakuhakikishieni katika mwaka huu huu tutasaini mwengine tu na China. Kwa hiyo hili lisitupe wasi wasi hata kama kuna 20 kule mitatu huku *speed* ya kusaini kwetu sisi ni nzuri zaidi.

Vile vile alitaka kuelewa kwamba kuna sababu zipi za msingi hata Rais wa China asije hapa badala yake Rais wetu akenda Dar es Salaam kuonana naye. Sababu ya msingi ilikuwa ni muda tu, kama mtakumbuka Rais wa China amewasili Tanzania ndege yake imetua katika Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam saa kumi kasoro za jiopni na ameondoka katika ardhi ya Tanzania tarehe 25 saa kumi za jioni *hardly* alikuwepo kwa muda wa masaa 24 na *program* aliyoandaliwa ilikuwa ni kubwa na sisi tulihisi ni vyema tukenda tukaonana naye tuka-*present* kesi zetu wenyewe badala ya kwamba

tuwakilishwe na wenzetu. Sisi wenyewe madhali tupo tukaona twende tukaseme kesi zetu tuonane naye na tuzungumze naye na kwa kweli alitupokea vizuri sana.

Na nataka niunganishe hapa hapa, wakati wa mazungumzo Rais wa China na Rais wa Zanzibar mawaziri karibu saba humu ndani tulikuwemo. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko alikuwemo, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mimi mwenyewe nilikuwemo, Mhe. Waziri wa Afya, Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika alikuwemo, Rais wa China alitamka mwenyewe akasema kwamba urafiki wetu na Zanzibar sisi ndio tulioitambua Mapinduzi ya Zanzibar wa kwanza duniani, na yeye mwenyewe akasikitika akamwambia Mhe. Rais wa Zanzibar nadhani wenzangu mawaziri tulikuwemo na Makatibu Wakuu walikuwemo, akasema kwamba kwa sababu nakwenda *South Africa* kesho kuhudhuria Mkutano wa BRICs, kwenda *South Africa* sio kwamba anaitembelea nchi kama alivyotutembelea sisi, alikwenda kule kwa ajili ya kuhudhuria mkutano wa BRICs**,** mkutano ambao unajumuisha nchi tano zinazokua kiuchumi, Brazil, Rusia, India, China and South Africa.

Akamwambia Rais kwamba, *next time* nikija *I will make sure I will visit Zanzibar*. Kauli yake mwenyewe Rais wa China na mimi naamini kwa sifa anazopelekewa uzuri wetu wa Zanzibar atakuja tena na atatutembelea.

Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua miradi yote ina thamani kiasi gani na Zanzibar imepata kiasi gani. Hili sitaweza kulitoa kwa sababu hata katika ripoti haikuwemo thamani ya mradi. Kwa sababu miradi ambayo tumetia saini 17 myengine iko katika *system* ya mkopo nafuu. Mingine iko katika msaada wa moja kwa moja na mingine ipo katika PPP *(Public Private Partnership*). Sasa kwa sababu haikutiwa *cost* na mimi sitaweza kumpa thamani ya ile miradi, labda baadae hatua kwa hatua tukipata kama hivi ilivyojitokeza ule mradi wa Bandari tukipata tutakuwa tunaarifiana. Namuomba hilo Mhe. Hija Hassan anistahamilie.

Aliyetaka kujua zile *ten million dollars* yeye uzoefu wake serikali miradi mingi hapa mnampa China Railway na hii ya ujenzi wa miundombinu mtampa China *Railway*? Zile *ten million dollars* ni pesa kidogo sana kimaendeleo lakini kwetu sisi Zanzibar ni pesa nyingi. Tutaweza kuzitumia kwa miundombinu Sekta ya Afya, Sekta ya Maji, Sekta yoyote tutakayokubaliana sisi kwamba hizi tuzitumie kidogo hapa, kidogo hapa zitakwenda huko na kikawaida kwa sababu ya *gratis aid* wao wanakuwa wana-*propose* makampuni kutoka China ambayo sisi tunaona kwamba yanaweza kutufanyia kazi kwa ufanisi zaidi, tukiona China *Railway* haku-*qualify* basi tutasema hii tutampa kampuni nyengine.

Zipo kampuni ambazo zimefanya vizuri sana hapa kwa mfano, Kampuni ya *ZTE* iliyojenga *E-Government* ndio hiyo hiyo inayojenga *street light*. Kwa hivyo, ziko kampuni nyingi za Kichina nzuri sana *Shanghai* Construction, ziko nyingi sana sisi wenyewe tutachagua ni kampuni gani. Kwa hivyo, hilo nataka nimhakikishie Mhe. Hija kwamba tutakuwa waangalifu.

Amesema kwamba Uwanja wa Ndege wa Unguja umefeli na kwa nini tunakwenda, *terminal* ya Unguja ina matatizo, sitaki nitumie moja kwa moja kwamba imefeli. Serikali imesema kwamba sasa hivi kutokana na ile michoto ambayo wenzetu wamechora, serikali imesema kwamba tunahitajia *an independent consultant* kuisoma ile michoro na kutoa ushauri kwa serikali. Ma-*Consultant* kutoka Ufaransa wanawasili siku ya Jumatano watakaa, wataitazama ile *terminal* halafu watatushauri serikali. Kwa hivyo, mimi naliomba sana Baraza lako tukufu Mhe. Spika, wawe wastahamilivu kidogo, lakini lengo letu sasa hivi tuko waangalifu sana kuliko hata hivyo mnavyofikiria.

Nani aliyemualika ujio wa Rais wa China, Rais wa China kajialika au kaalikwa na Dr. Jakaya Mrisho Kikwete. Mhe. Spika, nataka niseme sisi utamaduni kama Watanzania unaweza ukamwambia Mhe. Mohammed Aboud kesho nitakuja kula *lunch* kwako, na Mhe. Mohammed Aboud kwa sababu ya uswahiba wangu na yeye asinikatalie akasema sawa njoo tu na yeye akatayarisha *lunch* tukala. Na tuna utamaduni mwengine vile vile, Sheikh Jussa anaweza akanambia Sheikh Omar nakualika kesho baada ya swala ya Ijumaa *lunch* nyumbani, kanialika yeye sasa. Sasa sisi tamaduni hizi tunazo kwa Watanzania. Lakini kwa ujio wa Rais wa China ni ujio ambao Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiye aliyetamani kwamba Rais huyu aitembelee Tanzania.

Lakini Rais huyu alipopata urais alikuwa na maamuzi yake angesema kwamba mimi nitaitembelea Tanzania iwe nchi ya kumi kwa Afrika, lakini akasema aa kutokana na ukaribu wangu na Tanzania nitaifanya iwe ya kwanza katika Kontinenti la Afrika. Kwa hivyo, hapa kuna keki ame-*share* Dr. Jakaya Mrisho Kikwete na kuna keki ame-*share* Rais wa China. Hivyo sote sisi hizo kwa kwetu tunazifurahia na ni matunda kwa Tanzania.

Mhe. Ismail Jussa ameeleza kwamba katika taarifa yangu ingekuwa uzuri hasa ningeweka msingi wa mahuriano baina ya Zanzibar na China. Ni kweli nakubaliana na yeye lakini kutokana na muda nilidhani kwamba niifanye iwe fupi sana,*I could even write hundred or two hundred pages* kwa ajili ya taarifa tu na ujio wa Rais wa China, mambo mengi yapo baina yetu na China.

Miradi mingine 14 kwa Tanzania Bara tuwatajie, ili kunusuru wakati miradi yote ninayo hapa iliyotiwa saini nadhani baadae tunaweza tukarudufua ili kila mmoja akaweza kupata nisipoteze wakati. Lakini yote ipo iliyotiwa saini.

Mhe. Jussa vile vile alitaka kujua ile saini niliyosaini wakati anakuja Naibu Waziri Mkuu nilisaini Ikulu pale kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio hii niliyosaini juzi au nyengine? Siwezi nikasaini mara mbili kitu hicho hicho, ile nilisaini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais atakumbuka ilikuwa ni *Fifty Million Yuan*, hii niliyosaini juzi ilikuwa ni *Sixty Million Yuan*. Kila mwaka Wachina wanaisaidia Zanzibar *gratis aids* kwa kiwango ambacho wanaona wao kila mwaka ambapo hizo tunaangalia ni maeneo gani ya kimaendeleo tuweze kuzipeleka na zinasaidia. Sehemu ya ile *Gratis Aid* tuliyosaini mwaka jana ndio hii ambayo tumeitumia kwa ajili ya taa za njiani.

Mhe. Jussa alitaka kujua nimeshajibu Rais wa Zanzibar kwenda Bara na sisi ni rafiki yetu sana Rais wa China ni muda tu, kwa sababu mimi naamini wangepata zaidi ya masaa 24 Rais angekuja kwa sababu usafiri tunao wa kumleta hapa anakuja anazungumza na ndugu zake wa Zanzibar akaondoka.

Mhe. Hamza Hassan Juma alisemea kuhusu ushiriki wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maandalizi. Tumeshiriki katika maandalizi na tumeyaanza hapa ndani, tumeanza wenyewe ndani kabla hatujashiriki na wenzetu.

UTARATIBU

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Naomba tu mkumbushe swali langu moja Mhe. Waziri amelisahau nadhani. Niliuliza thamani ya ule mradi wa Bandari ya Maruhubi au Mpigaduri ambao umepelekwa. Nikilinganisha na majibu ambayo niliwahi kujibiwa humu humu ndani na serikali hii hii kwamba pendekezo lililopelekwa mwanzo ilikuwa ni mara mbili ya kilichokisiwa kwamba ni thamani halisi, badala ya US$ 400 milioni zilizozaniwa Wachina wakataka kujenga kwa shilingi US$ 800 milioni. Naomba alijibu Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, namuomba radhi sana, kweli aliliuliza suala hili na nililiandika lakini katika kusoma nikaliruka tu. Ni kweli Mhe. Spika, kuna kitu ambacho sisi tumekiona, kitu kimoja ambacho tumekiona na hiki tumesema tunataka kidogo tukifanye katika njia mbili pale ofisini kwetu Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kushirikiana na Tume ya Mipango. Tumekiona kwamba huwezi ukawa na kesi ya panya unampelekea buku, utaratibu wa Wachina wanakuja wanakwambia kwamba wao watafanya *feasibility study*, wanapofanya *feasibility study* maana yake *the cost* wanaiweka wao. Sasa

wanapoweka *cost* wao wewe unakuwa kama huna macho ya kuangalia, unaipeleka kule mradi unaweza kuwa ni very *expensive*.

Sisi tumesema tutafanya mambo mawili, tumezungumza tayari pale ofisini na tayari tumeshakubaliana. Kimsingi tumesema la kwanza, aidha tutatafuta wenyewe fedha tufanye *feasibility study* wenyewe, *any independent consultant* ambaye atafanya *feasibility study* ile *feasibility study* sasa unaipeleka kwao kwa ajili ya kupatiwa fedha. Hii itarahisisha kuweza kujua kwamba hizi ndio gharama halisi za mradi hilo la kwanza.

Lakini la pili tumekubaliana ndani ya ofisi kwamba, kama hatuna fedha za kufanya *feasibility study* tutakuwa tuna *close* kifungu tutakiweka ndani ya mikataba yetu na Wachina kabla ya kufanyha *feasibility study* kwamba *feasibility study* itakapokamilika kabla hatujasaini mkataba wa mkopo *an independent consultant* atafanya *valuation* ili ku-*determine* zile gharama zilizomo mle ndani sio kubwa, kama ni kubwa wapi tuweze ku-*negotiate* ili ziweze kupunguzwa. Hayo mawili tumesema kwamba yanaweza yakatusaidia katika kufikia ile gharama ambayo Mhe. Jussa alikuwa na wais wasi nayo. Ni kweli wao walileta na ule mradi ulikuja kama na *six hundred plus milioni dollars*. Ilikuwa ni kampuni moja ya China na tukaiangalia tukaona *very expensive* kwa mradi wetu ule sasa tukasema kwamba tutafute *an independent consultant*, ndio yale niliokuwa nayasema Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kwamba *feasibility study* itakapokuwa imekamilika ndio zile hatua sasa za kutafuta pesa zinapokuwa zinaanza.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza aliuliza kwamba ushiriki wa SMZ katika maandalizi. Ni kweli tulishiriki na tulianza wenyewe ndani kabla hatujaenda kuzungumza na wenzetu wa Tanzania Bara, tukatizama sekta, tukatizama kwamba sio kuwa Rais wa China anakuja tuna matatizo mengi haiwezekani mgeni anakuja sasa tena unamwambia matatizo yako yote mimi sina kitanda, kijiko, chuma, sinia, matatizo yote unamwambia, sasa mgeni huyo utamchosha; tukaona tuchague matatizo ya msingi ndio tuyapeleke. Kwa hivyo, tulifanya wenyewe ndani baadae tukafanya mawasiliano na majadiliano na wenzetu Tanzania Bara kama ni *Tanzanian Team*.

Aliuliza swali zuri sana kwa nini mradi huu wa Bandari ya Zanzibar miaka 20 tunauzungumza tu hatujautia saini umekwenda kutiwa saini wa Bagamoyo wa juzi. Majibu yapo mengi, lakini la kwanza hata sisi tungekuwa tushautia saini huu kama tungekubali milioni mia sita na kitu ungekuwa ushatiwa saini au uongo wenzangu mawaziri, Mhe. Hamad shahidi, lakini tulipoona gharama kubwa na ile *study* iliyoletwa kwetu tukasema tukasema *this is not complete feasibility study*, na kwa nini imezaa gharama hii, tukasema *no*, lazima tutazame wenyewe ili tuweze kujua.

Lakini kwa bahati vile vile kwamba ile Kampuni tuliyoikabidhi mwanzo ilikuwa ina matatizo na tuliona mapema, lakini sisi hii bandari tulitaka tuijenge kama ni serikali, taarifa ambazo nimezipata lakini sijathibitisha. Mhe. Spika narudia, tarifa ambazo nimezipata lakini sijazithibitisha kwamba Bandari ya Bagamoyo inajengwa *under PPP, is not a Government,* ni *Public Company* ndio wanayoijenga Bandari ya Bagamoyo sijaithibitisha ndio ninaifuatilia ili tuone *model* gani. Nimeshazungumza na Balozi mdogo wa China amenambia nimualike Meneja wa ile Kampuni anayejenga Bagamoyo tufanye mazungumzo naye, na hivi sasa tuko katika kufanya utaratibu wa kumualika ili tuweze kuthibitisha zaidi kama ile iko kwenye PPP. Kwa hivyo, hiyo tu ndio sababu na ziko nyenginezo. Na hii *ten billion* sio *development* ya bandari peke yake kuna *development* ya mambo mengi katika eneo la bandari hii *ten billion dollars*.

Alitaka kujua pia Mhe. Hamza maana ya mkomo nafuu ni nini. Mkopo nafuu kwa kifupi una maana mbili tu, riba ndogo chini ya asilimia mbili, halafu muda wa kulipa zaidi ya miaka 20 halafu wanakupeni *gross period* miaka mitano kabla hata hamjaanza kulipa, ndio maana ya mkopo nafuu sio ule nakupa unilipe papo kwa papo ule ni mkopo au ule wa riba kubwa kama kibiashara unaweza ukaanzia riba asilimia kumi ule si mkopo nafuu. Kwa hivyo Wachina riba yao inakuwa chini ya asilimia mbili na kipindi cha kulipa kinakuwa zaidi ya miaka 20 wanakupeni na *gross period* miaka mitano kabla hamajaaza kulipa kwa hivyo mnajiandaa katika malipo na hiyo ndio maana yake. Masharti, hakuna masharti. Sisi wenyewe tuangalie mradi ambao iko *economical viable* kiuchumi una thamani ule tupeleke ili waweze kutusaidia. Labda kuna zile taratibu zetu za ndani tu kwamba tusifikie zaidi ya asilimia fulani tukawa tunakopa tu.

Kuanzishwa Benki ya Wanawake, Benki ya Vijana kwa nini hatujazungumza. Hata tungelilizungumza wasingetusaidia katika eneo hili, hili tunalizungumza wenyewe sasa hivi ndani. Kuna kamati ya mawaziri bahati nzuri wenzangu wote hawapo leo Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika yumo kwenye kamati ambaye yeye ana vyama vya ushirika, Mhe. Waziri a wa Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto yuko kwenye kamati na mwenyekiti wao ni mimi tunataka kuanzisha hiyo benki itaweza ika-*cover* sekta zote hizi, tutakuja baadae kuitolea taarifa.

Uwanja wa *Mao-Tse-Tung* kwa nini hatukuuzungumza. Huu uwanja hatujauzungumza katika *level* hii ya Rais, lakini tunaendelea na mazungumzo baina ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Balozi Mdogo wa China.

Mhe. Subeit Khamis Faki ametaka kujua sababu za msingi Rais wa China kwa nini asije Zanzibar. Nafikiri hili nimeshalijibu katika moja ya maswali. Vigezo vilivyotumika kwa miradi hii. Sasa akisema miradi hii hapa pana makundi mawili, kuna miradi tuliyoitia saini kigezo kikubwa tumeangalia matatizo yetu, Hospitali ya Pemba Mkoani imejengwa na Wachina 1969 kwa hivyo ile hospitali sasa hivi ime-*deteriorate* tukaona tuwaambie wenyewe Wachina waisaidie kuiboresha zaidi. Kigezo cha pili kwenye ile miradi saba tuliyoiomba ni kwa sababu tunataka ku-*improve* uchumi wetu.

Ukarabati au ujenzi wa hospitali mpya ya Mkoani isipokuwa lile jingo la mbele majengo mengine yote yatavunjwa yanajengwa mengine na inaongezwa. Kama nilivyosema katika ripoti yangu sasa hivi ina vitanda 80 itakuwa ina vitanda 160, itakuwa ni hospitali ya rufaa ya Pemba, itakuwa ina vifaa vyote vya ukaguzi, itakuwa ina ICU, itakuwa ina sehemu ya kuchomea taka taka, itakuwa inaongezwa madaktari na eneo la pale lote nyumba za pake zote tumeshaandaa sasa hivi tathmini tumeshaifanya kwa wale ambao tutawaondoa tutawalipa fedha zao ili tuweze kuipanua hospitali hiyo kwa faida yetu wenyewe.

Upanuzi wa Hospitali ya Mkoani ni kwa faida yetu wenyewe, badala ya kuwa tunapata hasara ya kumleta mgonjwa Unguja na nini tuweze kufanya shughuli zetu pale pale, kwa yale makubwa ndio tutapelekana nje na tutaomba Mwenyezi Mungu asituoneshe makubwa.

Mhe. Omar Ali shehe alitaka kufafanuliwa juu ya miradi tuliotia saini. Tuliotia saini ni miradi mitatu tofauti na miradi saba, ile miradi saba ndio sasa hivi tuko kwenye *negotiation* tunafanya mazungumzo nao baadae tutakuja kuitia saini na hiyo saba, ile mitatu imeshakamilika ndio imetiwa saini na *implementation* zake sasa hivi zimeanza kwa sababu *scanner* zitawasili mwezi wa Mei.

Kwa bahati nzuri Mhe. Spika, nina mawaziri humu ndani wamekwenda kuziona *scanner* zile. Mhe. Haji Omar Kheir, Mhe. Mohammed Aboud na wakati huo Mhe. Hamad Masoud alipokuwa waziri, hawa wameziona zile *scanner* zinavyofanya kazi kontena linapita dakika tatu tu imeshasoma kila kilichomo ndani, nimewapeleka China wakenda kuziona wakafurahi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, alitaka kujua suala la kuteuliwa kwa mabalozi je, kuna mashirikiano yoyote? Mimi nataka niridhike kwamba mashirikiano yapo na ndio kwa maana *from no where* unamsikia mtu kateuliwa anakwenda ubalozini unajiuliza Jakaya Mrisho Kikwete anamjua huyu? Hamjui. Kampataje, kampata kupitia kwa Dr. Ali Mohammed Shein. Kwa hivyo, mashirikiano yapo tuombe yaimarike zaidi, tuliojifunza katika ziara za China

na utekelezaji wake Mhe. Spika, mimi naomba tu kwamba tuliyojifunza ni mengi na mengi yameanza kutekelezwa, nikianza kuyachambua sasa hivi nitapoteza muda wako hivyo namuomba somu yangu Mhe. Omar Ali Shehe basi tupate muda halafu nimpatie.

Kuna ripoti ambayo niliitoa kwenye semina ya Mawaziri na Makatibu Wakuu juuya China, naweza nikamtafutia ile karatasi nikampa akaiona jinsi tulivyokuwa tumetekeleza na hapa tulipofikia.

Mhe. Spika, baada ya kueleza hayo nataka nimalizie kwa kuwashukuru sana Wajumbe *(Makofi).*

UTARATIBU

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, Mhe. Waziri swali langu moja naona kalisahau sijui kama kwa bahati mbaya au sijui kwa nini naona kaliacha. Nilimuuliza Zanzibar tuna matatizo ya bandari hasa kuwa ni finyu na sote tunajua, lakini kuna sababu ipi ya msingi ya kuachwa kutiwa saini ujenzi wa bandari yetu ya Zanzibar kwanza na ikenda kutiwa saini kujengwa Bandari ya Bagamoyo ni sababu zipi za msingi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo: mhe. Spika, nimelieleza wala sikuliwacha, nimesema kama tungekuwa tumeyakubali yale masharti ambayo Mhe. Jussa ameliona tungekuwa sisi Bandari ya Zanzibar tushatia saini tangu mwaka jana wakati Mhe. Hamad Masoud alipokuwa waziri. Lakini tumeona ile *cost* waliyotuletea wenzetu ilikuwa ina gharama kubwa na ile kampuni tuliigundua kwamba ina matatizo ndio tukasema hapana. Nataka kukuhakikishieni tu kwamba, mkopo kwa ajili ya *development* ya Bandari ya Zanzibar hivi sasa iko kwenye *Exim Bank* tayari. Pale China *Exim Bank* Beijing iko maombi ya mikopo hii, tusubiri tumalize, tukimaliza na sisi tutatia saini wala usifanye haraka, unaweza firimbi ikapigwa ukaanza kukimbia wewe *round* ya mwisho ukawa umechoka mwenzako aliyekuweko nyuma akaanza kupita akachukua *gold medal***.** (*Makofi)*

Kwa hivyo, wanaweza wakaanza sisi tunatroti tukawapita njiani tukamaliza sisi. Sasa nawaomba Waheshimiwa wastahamili na wala hatujayakalia haya mambo wala hatuko mbioni tunayafanyia kazi. Ahsante sana Mhe. Spika.*(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kauli ya waziri imewasilishwa nione kama tumeipokea kauli hiyo. Wanaoipokea kauli wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Kauli ilitolewa iamuliwe)

(Kauli iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Waziri nawashukuru na Waheshimiwa Wajumbe kwa kupokea Kauli hiyo ya Serikali. Waheshimiwa Wajumbe kuna dakika chache ambazo ilikuwa tuzifanyie kazi kwa sababu muda wenyewe nao unatukimbia.

Waheshimiwa Wajumbe nataka mnisaidie kuhusu namna ya kufanya shughuli zetu kwa ufanisi tukizingatia na muda tulionao, lakini si tu muda tulionao lakini pia na hali ya bajeti tuliyonayo vile vile. Masuala yote hayo matatu Waheshimiwa Wajumbe ni wajibu wetu kuyazingatia ili hatimaye tuweze kufanya shughuli zetu vizuri kwa ufanisi kwa muda mfupi tulionao lakini pia kwa bajeti finyu tuliyonayo. Na hili la bajeti finyu nataka nilisisitize kwamba kimsingi bajeti yetu ni finyu mno haiwezi kumudu kufanya shughuli nyingi kwa kipindi hiki, tukizidisha muda kwa kweli tutakuwa tumekwenda nje ya matumizi ambayo tumeyaweka katika bajeti zetu. Sasa hili ni tatizo kubwa na kama ni tatizo sisi ndio viongozi ambao tuone matatizo haya tunayafanya vipi.

Waheshimiwa Wajumbe naomba niwapeni taarifa kwamba kwa mujibu wa shughuli zetu za mwaka huu tumeshakwenda *deficity* kwa kiasi cha shilingi milioni mia mbili na arobaini, nje ya matumizi kabla hatujafikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2012/2013. Na kwa mkutano huu nao fedha inaelekea kumalizika lakini bado shughuli zetu hizi hazijaisha, sasa moja kati ya mambo hayo inabidi tukubali ama tufanye shughuli zetu kwa mujibu wa fedha tuliyonayo nyengine tuziache si sahihi wala si vizuri. Au tutumie muda mfupi tulio nao fedha kidogo tulizonazo tumalize kazi hizi kwa kujitahidi kufanya shughuli zetu kwa kutumia muda mfupi tulionao na fedha ndogo tuliyonayo lakini kazi tuzifanye. Sasa haya ni maamuzi yetu sisi waheshimiwa wajumbe sisi ndio viongozi wa Baraza la Wawakilishi ndio tunaongoza serikali na kuisimamia serikali. Ni vyema basi tuzingatie kwa makini sana juu ya jambo hili.

Tulikaa katika vikao vyetu mbali mbali tukaona tutatekelezaje kanuni yetu ambayo tuliipitisha juu ya masuala ya maelekezo ya mambo mbali mbali ambayo serikali kupitia usimamizi wa kamati zetu za kudumu katika maeneo mbali mbali imetekeleza vipi. Kanuni imetaka kwamba mawaziri basi waoneshe namna gani tumetekeleza shughuli hizo kabla ya hapo huko nyuma hatukuwa na kitu cha aina hiyo. Lakini kwa kuongeza ufanisi juu ya usimamizi wa Baraza juu ya serikali basi tukaona tuweke kifungu hicho ili

mawaziri sasa watupe taarifa juu ya utekelezaji wa mambo mbali mbali ili kuongeza ufanisi na hiyo ndio hasa ile *function* ya Baraza.

Sasa hali hiyo baada ya vikao vyetu vya nyuma kwenye Kamati ya Uongozi na vikao vyengine na *briefing* tukaona njia gani bora sasa tuitumie zimekuja njia nyingi lakini njia ya mwisho ambayo tumekubaliana ambayo na mimi hata hiyo niliipendekeza ni kwamba mawaziri watoe taarifa ya utekelezaji lakini hatimae wenyeviti wa kamati ambao wizara zile zinaangukia chini ya kamati hiyo nao pia wawasilishe ripoti mpya ya kamati. Mchango wende kwa ujumla na tukakubaliana kwamba tuitumie siku hii moja ili kamati zote hizo tuweze kuzifanyia kazi vizuri na kwa ufanisi.

Kabla ya hapo wakati huo hatujajitanua, hatujatanua shughuli zetu ili kuleta ufanisi ulio mzuri zaidi tulikuwa tunafanya kazi ya kusikiliza ripoti mbili za kamati kwa siku hii moja lakini tukaona hapana haileti yale majibu ambayo kamati wameona na wananchi wanataka kujua yametekelezwa vipi, tukabadilisha kanuni na tukasema kwamba hapana, serikali ijibu basi. Sasa tukakubaliana kwamba tutumie siku moja kwa ripoti ya kamati moja. Lakini kuna kamati nyengine Wizara inazoshughulikia ni nyingi na zina mambo mengi lakini bado tulizingatia siku hiyo moja.

Sasa kazi iliyofanyika jana ilikuwa imalizike hiyo jana haikumalizika wachangiaji ni wengi, pengine ni nusu tu waliopatikana na bado kuna nusu wengine hawajapatikana. Kazi ambayo hata tukisema tuipanue kwa kiasi hicho kwa michango basi ripoti moja itatuchukua siku mbili. Maana yake shughuli zetu hizi zinaweza hata kukaribia mwisho wa mwezi huu ambayo hiyo tutakuwa tumetumia fedha nyingi sana nje kabisa ya bajeti ya mkutano huu. Sasa sisi ndio viongozi tusaidiane hichi kiti niko huku mmeniambia tusaidiane tutafute rai ili tufike pahala shughuli zifanyike kwa fedha ambayo tuliipitisha sisi ndani ya Baraza. Kama vile tunavyowauliza wizara nyengine namna walivyotumia fedha na ufanisi upi umepatikana ndio sisi ni kazi yetu kwa hivyo na sisi tuangalie suala hilo.

Sasa kutokana na hali hiyo na ili kuweza kulinda utaratibu wa matumizi lakini pia kuweza kuona kwamba kanuni yetu tuliyopitisha kutaka serikali itoe majibu juu ya utekelezaji wa mambo mbali mbali yaliyoonekana na kamati basi tumefanya hivyo kutekeleza kanuni hiyo lakini muda unatukwaza; tuna matatizo ya muda, tuna matatizo ya fedha.

Kwa hivyo njia ni mbili tufanye sehemu ya kazi nyengine tuiache, mimi ninavyoona si sahihi, si vizuri na hatutendea haki kamati nyengine ambayo imefanya kazi lakini ikawa hakuna majibu wala hazikuweza kuwasilishwa ndani ya Baraza letu, si vizuri haielekei. Na kwa yale mambo yanayowagusa

wananchi watakuwa wanadai kupata majibu kutoka serikalini juu ya mambo ambayo kamati zinazosimamia wizara mbali mbali zimeleta maelekezo kwamba jambo hili litekelezwe lakini halijatekelezwa na wananchi hawajui nini kilichofanyika.

Kwa hivyo tupo kwenye *cross road*, tunafanya nini. Rai ambayo niliyokuwa nafikiria ili tuweze kwenda vizuri ni kutumia muda mfupi na fedha ndogo tuliyonayo lakini mawaziri wajibu, wajumbe wamepata kuchangia na ku-*highlight* hasa yale mambo muhimu, kuacha marejeorejeo kama kanuni inavyokataza, lakini hatimaye tuone kama fedha ndogo tuliyonayo tunafanya kazi iliyopangwa kwa mkutano huu.

Waheshimiwa Wajumbe mimi nilikuwa na rai hiyo, kama kuna rai nyengine basi tupeana lakini mimi rai yangu ilikuwa kwamba muda mfupi tulionao, fedha ndogo tuliyonayo tuifanyie kazi hiyohiyo lakini tufikie pahala shughuli zote zilizopangwa katika mkutano huu tuzimalize.
Ratiba inaonesha shughuli zetu zimalizike tarehe 19, nimemuuliza Katibu kama ana uwezo wa kulipa zaidi ya hizi, akaniambia tukifanya hivi, hata kama Mhe. Waziri wa Fedha ataelekeza watie fedha nyengine, maana yake tunakula mfuko mapema wa mkutano mwengine ambao utakuwa ni mkutano wa bajeti ambao kuna mwezi wa Juni nzima tutakuwa kwenye bajeti lakini fedha hatuna.

Matatizo tuliyopata miaka mitatu iliyopita ni kwamba hata mishahara tulishindwa kulipa. Ikabidi tutumie vifungu vyengine vyote na kukopa nyengine lakini mishahara ilipike, hatuwezi tukawaacha wananchi wetu na sisi wenyewe humu ikawa tumefanya kazi lakini tusilipane mshahara, hiyo kiutaratibu haikubaliki.

Kwa hivyo Waheshimiwa Wajumbe naomba mukubaliane na mimi kwamba tutumie muda mfupi tulio nao na fedha ndogo tuliyo nayo lakini shughuli zetu tuzimalize. Kama hivyo ndivyo nategemea mutanikubalia rai yangu hiyo basi wachangiaji waliochangia tuseme *alhamdullah* wamepata nafasi hiyo, wengine mumewawakilisha wengine na muda mfupi tuliobaki nao tuanze kuita baadhi ya mawaziri mpaka saa sita watakaoweza kutoa majibu kwa yale mambo ambayo yameshachangiwa tayari na mengine tuje tumalizie jioni, na baada ya hapo tuite mawaziri wengine ambao ni Waziri wa Utumishi wa Umma pamoja na Waziri wa Katiba na Sheria na mwenyekiti kama nafasi itakakuwepo awasilishe, tuje tupate tuchangie labda siku ya Jumatatu.
Sasa hiyo ndio hali halisi tuliyo Waheshimiwa Wajumbe naomba sana tuzingatie hiyo sisi kama viongozi ambao tuna wajibu wa kuona shughuli zinakwenda vizuri, fedha tunatumia vyema lakini muda mfupi tuutumie.

Waheshimiwa Wajumbe basi nilikuwa na rai hiyo, nataka nione kama kuna rai nyengine basi munambie.

(Hapa Wajumbe walipiga makofi tu kwa muda)

Mhe. Spika: Makofi hayo yananiambia kwamba tumekubaliana.
Waheshimiwa Wajumbe ninachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa kukubaliana na rai hiyo. Kwa maana hiyo basi niombe twende kwenye *item number* 4 ya kirumi pale hatua ya kwanza ambayo ni kumuomba Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais ili kutoa majibu kwa yale michango aliyopata na pia kwa ripoti ile mpya ambayo amepata ili hatimaye twende kwa utaratibu huo na mwisho tumalizie kwa mwenyekiti wa kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa busara zako pia nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kueleza machache kutokana na taarifa iliyowasilishwa na mwenyekiti wa Kamati ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Spika, nianze kwa kuwashukuru wale wote waliochangia katika ripoti na kwa kuwa Mhe. Mwenyekiti atakuja kuwatambua kwa kuwataja majina, mimi kwa sababu hiyo ya kukimbizana na muda nisirudie.
Aidha niwashukuru wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa namna ambavyo tunashirikiana kuendeleza shughuli zetu za Baraza za kila siku.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kuanzia suala la utekelezaji wa shughuli za serikali. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumba sisi sote tuliomo humu ndani; wajumbe kutoka serikalini na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, sote kwa pamoja tunajenga nyumba moja, nia na madhumuni ni kuwatumikia wananchi ili kuwajengea mazingira yaliyo mazuri zaidi katika shughuli zao za kila siku za kuendeleza maisha pamoja na kuhakikisha kwamba tunapambana na umaskini na kuimarisha uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Spika, taarifa yetu ilitutaka serikali kuhakikisha kwamba tunapambana na maovu na kuhakikisha kwamba hatua zinachukuliwa. Kazi hiyo Mhe. Spika, ndio uamuzi wa serikali pale popote panapokwenda kinyume na taratibu na sheria za utendaji hatua huchukuliwa na mabadiliko wakati mwengine hufanywa na kwamba kuna hatua nyengine zozote za kupelekana katika vyombo vya sheria basi jukumu hilo hufanyiwa kazi. Ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba utaratibu huo upo na unaendelea na kadri tutakavyogundua makosa mbali mbali basi hatua zitachukuliwa.

Mhe. Spika, serikalini tunafanya kazi kwa pamoja ili kuhakikisha kwamba mambo yetu yanakwenda kama wananchi wanavyotaka na kwa sababu wao ndio waliotuajiri sote tuliomo humu ndani, kwa hivyo lengo kubwa ni kuhakikisha tunatekeleza matakwa yao.

Katika suala la utekelezaji Mhe. Spika, mjumbe mmoja hapa alizungumzia kwamba serikali hii ya awamu ya saba haina jambo lake la msingi ililolifanya bali yote ni yale ambayo yaliyoanzishwa na awamu ya sita, ndio sasa kwa kiasi kikubwa yanatekelezwa.

Mhe. Spika, niseme katika utaratibu wetu serikali ni suala endelevu na yapo mambo mengi ambayo serikali hii ya awamu ya saba imeyafanya na katika hotuba ya Mhe. Rais ya tarehe 12 Januari, 2013 aliyaeleza mengi ambayo yamefanywa na serikali hii ya awamu ya saba. Yapo mengi sana katika sekta mbali mbali sina haja ya kuyarudia.

Lakini utaratibu wetu katika serikali yale pia yanayoanzishwa na awamu inayomalizika basi yanaendelezwa kwa msingi wa kuhakikisha serikali ni endelevu na yote yale mazuri yanatekelezwa ipasavyo. Ndio maana miradi ile inayoanzishwa na awamu ya sita inaendelezwa pia katika serikali ya awamu ya saba. Na hivyo hivyo serikali ya awamu ya sita kwa mambo waliyorithi katika awamu ya tano nao wakaendeleza katika awamu ya sita, na hasa hasa ukitazama msingi wa utekelezaji wetu unatokana na ilani ya uchaguzi ina mipango ya muda mfupi na muda mrefu na huenda kwa kadri ya vipindi vilivyoekwa. Mara nyingi katika ilani yetu hueka vipindi vya miaka mitano mitano na baadae tukaendeleza katika vipindi vya miaka mitano na kuendelea. Kwa hivyo utaratibu huo ndio tunaoutumia Mhe. Spika.

Alipoondoka Dr. Salmin Amour alikuja Dr. Karume akaendeleza yale ya Dr. Salmin na yale ambayo aliyoanzisha kutokana na utaratibu wa ilani anavyofanya. Halikadhalika Dr. Karume alimkabidhi ilani ya uchaguzi Dr. Shein nao ni utaratibu ndio huo huo. Kwa hivyo hili si jambo geni Mhe. Spika, kutekeleza yale ambayo yaliyoanzishwa na vile vile kutekelezwa mapya yaliyofanyika na mengi yapo katika ilani ya uchaguzi mutayaona na vile vile katika hotuba mbali mbali za Rais na mawizara husika wanakuwa wanatoa taarifa za utekelezaji huo.

Kwa hivyo kazi nzuri inafanywa na inafanywa kwa pamoja. Napenda nichukue fursa hii kuwashukuru mawaziri wote wa serikali na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza hayo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Jeshi la Polisi. Waheshimiwa Wawakilishi hapa wamezungumza sana suala zima la kuimarisha Jeshi la Polisi, hasa hasa

wakazungumzia uchakavu wa majengo, matatizo ya magari na mafuta, uduni wa vitendea kazi, kujenga vituo vya Polisi na vile vile kuangalia maslahi ya askari wetu pamoja na kuweka utaratibu wa kukutana kati ya viongozi wa pande mbili kwa nia ya kulisaidia Jeshi la Polisi pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kulisaidia jeshi hili ili kufanya wajibu wake vizuri zaidi.

Mhe. Spika, huu ndio utaratibu ambao tupo nao serikalini. Tunafanya kazi kwa karibu kwenye masuala haya. Ni hivi karibuni tu ujumbe wa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na mawaziri, akiwemo Waziri wa Nchi (OR) Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Katibu, Katibu fedha na watendaji wengine tulikutana na ujumbe wa Waziri Mkuu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mkuu wa Jeshi la Polisi na watendaji kuzungumzia kwa kina matatizo ya Jeshi la Polisi.

Haya yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe wameyasema hapa ndio ambayo tuliyazungumza. Kukutana kwetu kulitokana na maagizo ya Baraza la Mapinduzi tukutane tuzungumzie kwa kina hali ya Jeshi la Polisi, matatizo ya uhalifu nchini na kuweka hali ambayo itakuwa inaridhisha wananchi wetu ili hali ya amani na utulivu iendelee kuwepo katika nchi yetu.

Kwa hivyo yale yote ambayo Waheshimiwa Wajumbe mumelalamikia ni mambo ambayo tumeyazungumza kwa kina, na tukakubaliana kwamba yatekelezwe kwa utaratibu mzuri. Jeshi la Polisi nao waliweka tayari mpango wao wa kutekeleza mambo mengi kati tuliyoyazungumza. Lakini mpango mkubwa kati yao ni mpango wa maboresho katika Jeshi la Polisi na ambao ndio wanaotekeleza.

Na walituelezea mipango yao. Tatizo kubwa Mhe. Spika, ni upungufu wa bajeti ya utekelezaji kwa sababu mpango wa maboresho ya Jeshi la Polisi unahitaji shilingi bilioni mia mbili tisini na nne, na wanahitaji kila mwaka wapate bilioni hamsini na nane katika kutekeleza mambo mbali mbali katika kuliimarisha Jeshi la Polisi, ikiwemo makaazi ya askari, vifaa, utaalamu kwa kujenga vizuri jeshi letu na kadhalika pamoja na mafuta ya kufanyia patro ya kila siku.

Kwa hivyo suala la msingi hapa ni ufinyu wa bajeti. Hata hivyo katika bajeti ya mwaka huu wamesema mengi ambayo tumeyazungumza watajitahidi wayawekee katika bajeti hiyo ili mambo mbali mbali ambayo leo yanaonekana ni kikwazo basi waanze kuyatekeleza. Naomba tuvute subra tutizame hatua zitakazochukuliwa kwa upande wa wenzetu wa Mambo ya Ndani pamoja na Jeshi la Polisi ili haya yote ambayo yamekuwa malalamiko katika Baraza hili yaweze kutekelezwa vizuri na utendaji wa Jeshi la Polisi

liweze kufanya wajibu wake kwa mujibu wa sheria na kuweza kuhakikisha hali ya amani na utulivu katika nchi yetu unakuwepo.

Kwa upande wa Idara ya Uchapaji, mengi yalisemwa. Kwanza walisema jengo ambalo sasa hivi wanatumia mitambo haifai, mitambo michakavu, hakuna wataalamu, malimbikizo ya posho, idara kuwa kampuni na kadhalika.

Mhe.Spika, Waheshimiwa Wajumbe serikali tayari imeshafanya uamuzi wa jambo hili. Haya yote ambayo Waheshimiwa wameyaona ni kweli yapo lakini serikali imeyaona na imeyaamulia kuyafanyia kazi. Ndio maana serikali ikayaamulia moja kwa moja kwamba tatizo la kwanza kuhusu jengo, kiwanda hiki kihamie Maruhubi.

Na sasa na sisi tumeshampata mkandarasi anafanya ukarabati wa jengo na karibuni jengo lile litakuwa lipo tayari. Kwa upande wa mitambo tayari tumeshampata mtu kampuni ambayo italeta vifaa hivi, pesa za mwanzo wameshalipwa, *bill of landing* tumeshapokea, karibuni hivi tutapokea mitambo na muda sio mrefu mitambo itafungwa tukiamini katika mwezi wa Juni tutaanza kuifanyia majaribio mitambo yetu kama hali itakwenda kama ilivyopangwa.

Kwa hivyo kwa upande wa kiwanda hayo ndio malengo yetu katika mwaka huu katika kuhakikisha kwamba kiwanda kinafanya kazi kabla ya kumalizika mwezi wa Juni. Lakini kwa upande wa kufanya idara kuwa kampuni, jambo hili serikali imeshaliona na tayari imeshatukabidhi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kulifanyia kazi, kwanza tulitaka kufanya *business plan* na kutengeneza waraka utakaonesha kwamba kiwanda kile kitajiendesha kibiashara.

Kwa hivyo mategemeo yetu kwa kuwa tayari tumemaliza kazi ya business plan, karibuni hivi tutapeleka waraka serikalini ili tukapate muongozo, nia ni kufanya badala ya idara kuwa mamlaka ya uchapishaji ili iweze kujiendesha kibiashara iweze kufanya kazi kama ilivyotakiwa na baadhi ya vijana wamepelekwa kusoma ili kujifunza zaidi na pia tunaangalia uwezekano wa kupata mtaalamu atakayeweza kukiendesha kiwanda kibiashara kisasa ili tuweze kuwa na kiwanda cha kisasa kuweza kukidhi haja na kifanyike uzuri kutoa huduma mbali mbali. Kwa hivyo kwa upande wa kiwanda tunaamini mambo yatakuwa mazuri.

Kuhusu maslahi na posho ya malimbikizo ya muda mrefu ambayo malimbikizo haya Mhe. Spika, yameanza kuwepo tokea mwaka 2004. Sasa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inachukua hatua kuhakikisha kuwa hatua kwa hatua wale wenye malimbikizo basi malimbikizo yao madeni yao

yanalipwa na ni utaratibu wa kawaida uliopo serikalini kwamba katika kila mgao, basi mkuu wa idara husika anatakiwa atenge fedha kwa ajili ya kumaliza matatizo ya huko nyuma.

Kwa hivyo msingi ni kuwa sisi tayari tumeelewesha Idara ya Uchapishaji ichukue hatua kuhakikisha kwamba kila mgao wanaopata basi wanatenga fedha kupunguza malimbikizo ya maposho. Tutahakikisha tunasimamia zaidi ili kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondoka.

Mhe. Spika, kuhusu sherehe za miaka 50. Waheshimiwa Wajumbe walizungumzia sana suala la kujitayarisha mapema ili sherehe zetu za miaka 50 ziwe ni sherehe ambazo zinafana ziende kwa mujibu wa hadhi inayotakiwa kuwepo na kielelezo cha kutimiza miaka 50, kuhakikisha kuwa nyumba ya Marehemu Karume inakuwepo.

Mhe. Spika, tayari serikali imeshatoa muongozo wa jambo hili na maagizo 38 yametolewa kwa ajili ya matayarisho ya sherehe za miaka 50 ya mapinduzi. Maagizo yaliyotolewa mengi yanalingana na michango mbali mbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hapa. Kwa hivyo kazi iliyo mbele yetu ni utekelezaji. Kubwa zaidi tunazidi kumtizama Waziri wa Nchi Fedha kwa sababu jambo la msingi ni fedha katika utekelezaji wa mambo haya. Ni mambo mengi makubwa, matayarisho yameanza na shughuli mbali mbali zinaendelea.

Tulivyotaka hasa kuanzia mwezi wa Juni mwaka huu mambo ya awali yawe yameanza. Kwa hivyo kama ulivyosema kuwa shughuli ni kubwa maelekezo muliyotupa Waheshimiwa Wajumbe tumeyapokea lakini tayari yameanza kufanyiwa kazi, kwa hili ninataka niwahakikishie kwamba yale muliyoyasema tayari serikali imeshayafanyia kazi na kutoa maelekezo hivyo kazi iliyobaki hivi sasa ni utekelezaji na kubwa litategemea sana uwezo wetu wa kifedha. Lakini tayari muongozo upo na maagizo ndio yatakuwa dira ya sherehe zenyewe. Kwa ufupi na ushauri wenu tunaupokea itakuwa ni sehemu ya kusaidia utekelezaji huo.

Kuhusu Tume ya Uchaguzi. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe wengi wamezungumzia kuhusu suala la uraia, hasa kufundisha masuala ya Katiba mpya, kuimarisha daftari la kudumu la wapiga kura, kujenga ofisi za Tume na kadhalika.

Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe ni ukweli umuhimu wa elimu ya uraia kwa wananchi ni jambo la msingi sana na ni jambo muhimu. Tume wajibu wake mkubwa hasa ni kutoa elimu kwa wapiga kura, lakini suala zima la elimu ya uraia, tume itashirikiana na Wizara inayosimamia mambo ya

utawala bora ambayo ndio wenye dhamana kubwa suala zima hili la elimu ya uraia kwa wananchi na wao wanashirikiana na sekta mbali mbali zikiwemo taasisi za kibinafsi katika kuhakikisha kwamba elimu ya uraia inatolewa.

Kwa upande wetu tutashirikiana na Wizara husika na Utawala Bora kuhakikisha kwamba elimu ya uraia kwa wananchi wetu inatolewa lakini elimu ya wapiga kura tutahakikisha kuwa wanapatiwa wananchi na hasa hasa katika utaratibu wa matayarisho yatakayotokea kuhusu kura ya maoni badala ya mchakato ule wa Katiba kufikia hatua hiyo, ili wananchi wetu waweze kuelewa.

Kuhusu daftari la kudumu la wapiga kura, leo asubuhi Mhe. Spika, wakati nilipokuwa ninajibu swali hapa, nilielezea kwa matayarisho ya kuendeleza daftari la kudumu la wapiga kura. Kama nilivyosema kwamba kwa kushirikiana na wenzetu wa UNDP wametenga milioni mia saba hamsini na sita kwa ajili ya matayarisho hayo na tayari wameshatoa milioni mia nne thamanini na vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetenga milioni mia tatu na hamsini na tayari wameshatoa milioni mia tatu hamsini na tisa katika suala la suala zima la kuimarisha daftari la wapiga kura.

Vilevile tumo katika kufanya mchakato wa kurekebisha sheria ya uchaguzi ili ziendane na mahitaji na maoni ya Waheshimiwa Wajumbe. Kwa hivyo Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe kwenye eneo hili tunaendelea vizuri na ninaamini wananchi wataridhika na hatua ambayo inaendelea kufanywa na Tume yetu ya Uchaguzi.

Kuhusu mamboya muungano Mhe. Spika, hapa kuna watu wamediriki kusema kwamba kero za muungano zimetushinda na tukaoneshewa vidole watu maalum kwamba Mohamed Aboud kero za muungano zimekushinda. Kero za Mhe. Spika, si za Mohamed Aboud wala Balozi Seif Iddi bali ni zetu sote kwa pamoja. Masuala haya yote yanashughulikiwa kwa pamoja kwa pamoja serikali ina collective responsibity. Kwa utaratibu huo basi mambo haya tunayafanya kwa pamoja.

Mhe. Spika, kama nilivyosema hivi karibuni na katika masuala mbali mbali kwamba hoja hasa za kero za muungano zilikuwa ni 13 na kati ya hizo 6 zimepata ufumbuzi, 2 zipo katika hatua za mwisho na 5 zinaendelea kujadiliwa kupatiwa ufumbuzi.

Ukitizama Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe ukweli sasa hivi kuna mwamko mpya tunapozungumza suala la muungano. Matokeo yameanza kuonekana na tunapata moyo kwamba utatuzi wa kero za muungano unapata majibu. Lakini mambo haya ni makubwa, magumu, mengine yana utaratibu

wa kisheria, yana utaalamu. Kwa hivyo si rahisi kwamba yatakwisha kwa ghafla. Lakinio madhali nia ipo na dhamira njema ipo ninaamini kabisa tutayapatia ufumbuzi.

Lakini kubwa hapa nilililozungumzwa sana ni suala la mafuta, wamesema kwa nini haliishi suala la mafuta. Mhe. Spika, katika mazungumzo hayo ya kuyatafuta usuluhisho wa suala la mafuta ndio tumefikia hatua ya mwisho mwisho katika kulitoa jambo la mafuta katika mambo ya muungano.

Katika kufikia hatua hiyo tumefikia hatua kwamba Wanasheria wetu wakuu wakae walitazame jambo hili kisheria, kitaalamu ili watuongoze tufikie muafaka mzuri ili jambo hili litakapofikia utekelezaji lisitokee kukwamisha, liweze kutekelezwa vizuri na lisitupe matatizo. Kwa hivyo Wanasheria wetu wakuu wameunda tume zao wanalifanyia kazi na ninaamini tuna Mwanasheria Mkuu mahiri ambaye nina hakika atasimamia vizuri haki za Zanzibar na tutafikia muafaka mwema sana kwenye jambo hili. Kwa hivyo mimi sina shaka yoyote hatua inakwenda vizuri, vikao vimeanza na mambo yatafikia uamuzi wenye maslahi kwa Zanzibar na kwa Tanzania kwa jumla.

Kuhusu viongozi wakuu kwa nini hawafiki Zanzibar, Mhe. Omar Yussuf Mzee ninamshukuru sana hivi asubuhi alilieleza hili jambo hili kwa kina sana, sina haja ya kulirejea kwa nini Rais wa China hakuja hapa Zanzibar.

Kuhusu mtazamo wa SMZ kuhusu Katiba mpya. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe serikali tokea awali ilisema kwamba mtazamo wake ni uamuzi wa wananchi. Maoni ya wananchi ndio yataheshimiwa na serikali. Kwa hivyo hii kauli imeshatolewa na mtazamo unabaki hapo hapo. Maoni ya wananchi wengi ndio yataleta sura ya mabadiliko ya Katiba. Ni wananchi wenyewe maoni yao ndio yataleta mabadiliko ya Katiba wanayoyataka wao na maoni hayo yataheshimiwa.

Na naamini Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ni sehemu moja muhimu sana katika maamuzi hayo, kwa sababu katika mchakato mzima utafikia wakati wa Bunge la Katiba na kwa kiasi kikubwa wajumbe wa Baraza hili watakuwa ni wajumbe. Kwa hivyo yale yote ambayo Tume imeyakusanya, imeyaona itayaleta mbele yetu tutayazungumza vile tutakavyoona inafaa na uamuzi tutautoa kwa pamoja.

Na baada ya hapo basi katika uamuzi huo tutakaoutoa ndio tutayapeleka sasa document ile kwa wananchi kwa kufanyiwa kura ya maoni ambayo ndio watakuwa na uamuzi wa mwisho. Kwa hivyo ni jambo la wao, hakuna yeyote wa kuweza kulipinga maamuzi ya wananchi ndio maamuzi ya mwisho na mtazamo wa serikali yetu.

Pia lilizuka jambo hapa Mhe. Spika, wakasema watu wasiokuwa Wazanzibari ndio watatuamulia hatma ya nchi yetu. Hilo halitokei kabisa katika nchi yetu. Ni Wazanzibari wenyewe ndio wataamua hatma ya Zanzibar yao na mimi ninapenda niwatoe shaka wananchi.

Kuhusu migogoro ya ardhi. Mhe. Spika, na Waheshimiwa Wajumbe ni kuwa Wajumbe wengi walitaka Mhe. Makamu wa Pili kuifuatilia karibu migogoro hii ya ardhi kutokana na hali halisi inavyojitokeza.
Mhe. Spika, kwa ufupi niseme kwamba ushauri unapokelewa na uamuzi wa serikali kwamba kila muhusika kwenye masuala ya ardhi anatakiwa awajibike kwa kufanya kazi kwa kufuata utaratibu na sheria kuhusu mambo ya ardhi. Mhe. Rais ametoa muongozo kwa Wakuu wa Mikoa, Wilaya na wizara husika kulisimamia jambo hili ipasavyo. Na akasema wale ambao linawashinda basi wamjuulishe Mhe. Rais.

Mhe. Spika: Naomba uishie hapo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais: Kwa sababu ya muda Mhe. Spika, naomba niishie hapo. Naomba tuwasilishe na mengine basi tutayaandika kwa maandishi kutokana na hali halisi ya muda.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

(Saa 6.00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

TAARIFA ZA SERIKALI

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kupata wasaa huu kwa mara nyengine tena, kufanya majumuisho kwa upande wangu wa maagizo yale yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi, inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu, pamoja na maagizo mengine ya Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati yetu Mhe. Hamza Hassan Juma wa Jimbo la Kwamtipura, kwa jinsi alivyotuongoza kwa kipindi takriban miaka mitatu katika Kamati yetu hii, yeye pamoja na Kamati yake. Kwa kweli lazima niseme tumefanya kazi nzuri sana. Mengi waliokuwa wakitushauri na wakituelekeza tumeyapokea. Ishara moja wapo ni hii orodha kubwa sana ya maagizo 41 ambayo walitupa kuyatekeleza. Mhe. Spika, kwa kweli tunawashukuru sana.

Mhe. Spika, Mhe. Mwenyekiti, mengi aliyatoa katika muhtasari wa ripoti yake. Niseme tumeyapokea na yale ambayo hatujayatimiza, tutajitahidi Mhe. Spika tuyatimize ili kipindi kilichobaki mpaka bajeti, basi tuje tuoneshe ripoti nzuri sana ya utekelezaji katika bajeti ya serikali.

Mhe. Spika, naomba nirudie tena kutoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, kwa michango yao mizuri sana ambayo wamekuwa wakitusaidia na wakituelekeza katika wizara yetu. Hata juzi baada ya kutoa hotuba yangu, basi nilipata michango takriban kama 10 ambayo walitugusa moja kwa moja wizara yetu. Kama ulivyosema Mhe. Spika, ungekuwa na muda wengi wangetupa michango mingi na mizuri sana.

Mhe. Spika, lakini kwa jumla niseme yote yaliyozungumzwa kama ushauri na maelekezo tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Sio rahisi kwa kweli kuyajumuisha kwa muda mdogo huu, lakini yote tumeyaandika mimi pamoja na wenzangu walioko juu kule. Nasema kwamba yote hayo ni muongozo kwetu. Siku zote nasema nakubali kwamba pale ambapo tumekosea basi mtukosoe na mtuelekeze ili tufanye vizuri zaidi. Lakini pale ambapo tumefanya vizuri basi naomba pia mtusifu. Nawashukuru sana baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wametusifu pale ambapo tumefanya vizuri. Namuomba rafiki yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu na yeye asione tabu pale ambapo tumefanya vizuri basi atusifu, pale ambapo tumekosea. Kama kawaida mimi humwambia sisi tuko tayari kupokea *constructive criticism* ili tujirekebishe na tufanye kazi vizuri zaidi.

Mhe. Spika, kwa ujumla niseme kulikuwa na mengi yamezungumzwa, lakini yako yale ambayo takriban Waheshimiwa Wajumbe wengi wameyataja. Naomba kwa ufupi tu niyaguse haraka sana ili nisichukue muda wako mwingi.

Kwanza kulikuwa kuna suala zima la *salary slips* kwa Waheshimiwa na hasa wapiganaji wetu. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Ismail Jussa Ladhu na Waheshimiwa wengine wengi walizungumzia suala hili. Walitaka kusema tu kwamba hili suala halina tatizo na kila anayehitajia kwa kweli tutampa, ila tatizo ni kwamba kwa sasa serikali haijajiwekea utaratibu wa lazima wa kutoa zile *salary slip*, hasa kutokana na ile kazi yenyewe ni kubwa. Kwa sababu nilizungumza na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwamba nahitaji *ream* 20, hizo ni kwa uchache tu, kutayarisha zile, kwa kweli ni kazi kubwa sana. Lakini ni haki yake mtu kudai *salary slip* apewe. Kwa hivyo, pale zinapofanywa zile *voucher* aende Kalamazoo pale au kwa karani yule anayeshughulikia kutayarisha mishahara, anaomba yeye na ataoneshwa, sio siri. Ni siri kwa mtu mwengine, lakini kwa yeye ni haki yake. Kwa hivyo,

Mhe. Spika, tutawaambia maaskari wetu wasione kuwa labda hawatendewi haki, hapana, ni tatizo tu. Lakini hilo tumelizingatia siku za usoni tutaona vipi tunaweza tukalirekebisha.

Suala jengine ni lile la yule mwekezaji wa Paje, Crystal Hotel. Lile suala nalo limejitokeza na Waheshimiwa wengi sana wamelizungumza, Mhe. Hamza Hassan, Mhe. Ali Salum Haji, Mhe. Ussi Jesha Simai, Mhe. Mgeni na Waheshimiwa wengine. Ni kweli hata sisi tumekereka, tumeona kwa kweli alivyofanya sio vizuri na bahati nzuri Halmashauri ya Wilaya ya Kusini iliwahi kumuandikia barua na akadharau yule bwana, kisha akafunga *beach* ile. Kweli wananchi wanapata tabu kwenda katika harakati zao za kila siku. Sasa ilipotokezea mara ya mwisho, niliingilia kati na mwenyewe tukampa siku saba avunje mwenyewe ama sivyo sisi tutakwenda kumvunjia. Kwa bahati akaona sasa ni kweli akakimbilia mahakamani akaweka *court injection.* Kwa hivyo, hili suala sasa liko mahakamani, lakini na sisi wanasheria wetu wa wizara, wanalifuatilia, kwa sababu sheria iko wazi kabisa. Kwa hivyo, hilo Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe watufahamu kuwa tunalifuatilia na hilo hatutosinzia kuona wananchi wetu wananyanyaswa ndani ya nchi yao.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo limejitokeza ni suala la utendaji wa Mawaziri. Hasa Mhe. Makame Mshimba na Mhe. Ismail Jussa. Mhe. Makame Mshimba kwa bahati mbaya hajaja, mpaka kazungumza kidogo Mawaziri wanakaba sana na wanapiga suti. Kwa bahati mbaya hayupo, lakini nimemtolea kidude hapa cha Washington DC.

Mhe. Spika, najua kidogo lazima tuchemshwe mpaka kivazi, hapana neno. Lakini nasema sasa ikiwa tena huku-*dress* vizuri na wewe unatuambia tu-*dress* vizuri, tuwe *smart*. Sasa Mhe. Makame Mshimba rafiki yangu anaudhika kwa nini tunakaba roho. Lakini ninacho muomba sana Mhe. Jussa, aliwahi kulizungumza hili na mimi nikamwambia aah! Mhe. Jussa, serikali au kwa ujumla unaonekana, usiwe na wasi wasi, watu wanakuona utendaji wako unavyojishughulisha, sasa wewe mwachie mwenye mamlaka yupo, mwache afanye kazi yake na yeye anatuona, anatufuatilia mwenyewe na kila kitu.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Jussa a-*appreciate* wengine hatukutoka tu vuuu mpaka uwaziri, ukiwaona mawaziri wote humu wamepanda ngazi moja, mbili, tatu wame-*struggle* mpaka walipofika. Mpaka wengine juzi kina Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji wamepewa tunzo ya ujasiri. Sasa ukamwambie Waziri kama huyo hafai, aa! *It's not fair* kwa kweli.

Sasa ningeomba jamani na sisi mtusifie, usingoje aje Mmarekani amsifie Mhe. Fatma Fereji au anisifie mimi, tuanze wenyewe. Kazi nzuri anayofanya

mtu mpe haki yake. Kuhusu utendaji wa Mawaziri naona niishie hapo tu. Lakini nataka kusema kwamba ningeomba sana kuwa tusaidiane, tuelekezane na tukosoane, sisi hatukatai halina tatizo, hiyo ni kawaida na tuko marafiki mno. Lakini sasa unajua wewe ukitoa picha hapa Waziri Mwinyihaji hufai. Jimboni kwangu nitaonekana vipi, si unanimaliza.

Sasa Mhe. Spika, hili kidogo ningesema tusaidiane, tuelekezane na tufanye kazi vizuri kwa pamoja. Kuna usemi hapa nilinukuu wa Kizungu unasema; '*making mistakes simple means you're learning faster'.* Kwa hivyo, hakuna aliyekamilika, isipokuwa mwenyewe *Subhanahu Wataallah*. Sio *serious offence,* hapana, ya kawaida hayo.

Suala jengine ambalo lilizungumzwa sana ni la madiwani, kuhusu mishahara na marupurupu yale ya mwishoni. Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Ali Salum Haji. Hili nimesema kuna Wajumbe walilizungumza mara nyingi. Kwanza kama nilivyosema, tunasubiri hasa mabadiliko haya ya sheria, sera tayari. Sasa mabadiliko haya ya serikali za mitaa tuone tutakwendaje, kwa sababu bila shaka tutakuwa na mageuzi makubwa sana, huo ndio ukweli kabisa.

Lakini pili, tungekubali tuwape madiwani chochote, lakini uwezo. Ni lazima tuwe wakweli jamani, uwezo tulionao sio mkubwa kiasi hicho wa kuweza kuwalipa madiwani wetu wote. Sina idadi kamili hapa, lakini ni wengi na kima hicho hatuna. Ninachosifia kwamba wenyewe katika Halmashauri wamefanya utaratibu, wanawapa hiyo posho kidogo na wengine wamefanya kama kila mwezi kama mshahara na haitoshi, lakini angalau inawasaidia na wanajiendesha na wanajitahidi kuchuma zaidi mapato. Bado tunahisi ipo *room* ya wao kuchuma zaidi mapato na wakaweza kujilipa wenyewe zaidi.

Sasa suala hili Mhe. Spika, niseme kuwa serikali imelisikia na japo ule usemi haupendezi lakini ndio ukweli wenyewe kwamba tunalifanyia kazi.

Halafu kuhusu Sheria ya Serikali za Mitaa imezungumzwa na wengi sana. Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Hamza Hassan Juma. Hili nalo kama nilivyosema kwamba sera ipo tayari, sasa ndio tupo katika kazi hii ya kuzitunga hizo sheria za serikali za mitaa. Hapo ndio tulipo, tumemaliza *strategical plan of action* na kazi hiyo inafanywa na sisi tunataka leo hii ikamilike hii kazi. Lakini ni lazima twende kitaratibu tuone kwamba kweli tunaweka kitu cha kudumu.

Halafu Mhe. Spika, kulikuwa na suala la ujenzi wa *shopping mall*. Waheshimiwa Wajumbe wengi wamepata habari na wamevutika na suala zima la ujenzi wa *shopping mall* pale Darajani. Kimsingi serikali imeliona hilo na tayari ki-*idea* imelipa baraka zake. Kwa sababu tumeona haipendezi

kwa wafanyabiashara wetu kuuza biashara chini, wakaziba njia za magari na inakuwa mvutano wa kila siku, sio jambo la busara. Kwa hivyo, ile *idea* ni nzuri. Zimeshajitokeza kama kampuni mbili hivi; moja kutoka Uingereza kwa kushirikiana na Kenya, Lakini na wazalendo wenyewe wa pale nao wamejitokeza wako tayari kufanya *shopping mall.*

Sasa tumeunda *candle of the inter ministerial committee* ambapo tutalizungumza suala hili kuona kwa mapana yake, kwa sababu pale mahala lazima tuone masuala ya mazingira yakoje. Kwa hivyo, Baraza la Manispaa nao kwa upande wao ukoje, Uhifadhi wa Mji Mkongwe nao wanasemaje, Idara ya Ardhi, Mipango Miji, ZIPA mkoa wa Mjini Magharibi wenyewe. Kwa hivyo, tumefanya *Interministerial committee* ndogo hivi ili kulitafakari lile suala zima pale, liende vipi kwa utaratibu gani, ili hata likiondoka tuone kwamba kweli hatutengenezi huko tukabomoa humu. Kwa hivyo, kimsingi hilo wazo lipo na sisi tumelikubali kimsingi na tunalifanyia kazi.

Suala jengine lililozungumzwa sana ni usafi wa mji kwa jumla. Nafikiri hili nimelijibu mara nyingi sana. Uwezo wetu ni mdogo, lakini tunajipanga upya kuona kwamba angalau zile taka humu mitaani zisikae. Sasa hilo tunalifanyia kazi kwa nguvu sana, tunajaribu kuona tutafanya vipi, kama walivyotoa ushauri tuombe vikosi au tuombe magari ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, hilo tunalifanya.

Mhe. Spika, nataka kusisitiza tu kwamba na watu wenyewe nao twendeni pamoja sote, tukubali kuweka mazingira yetu katika hali ya usafi. Hilo ni suala la msingi sana, lazima tubadilike na sisi tuone kwamba kweli tunakerwa na uchafu. Lakini suala la msingi sana ambalo nahisi litatusaidia, ni lile wazo la kuzigeuza taka kuleta mazao mengine au kuleta matunda mengine. Kama asubuhi pale Mhe. Spika, alipowatambulisha wale wageni wa *Syncrona West Management*, ambao wao watazalisha taka kufanya umeme, hilo ni wazo moja.

Lakini juzi tulikuwa na mgeni mwengine kutoka Bangalow MK Aromatics, wao wanataka hizo taka za *plastic* wazigeuze mafuta. Kweli tumeona mtambo mmoja mzuri sana. Tulikuwa mimi, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza. Wanasema kilo moja ya taka inazalisha lita moja ya *gruel oil*. Kwa kweli imetuvutia sana na tukaona kweli tukichacharika kwa suala hili, basi tunaweza tukafanikiwa kuona kwamba taka hizi hasa za *plastic* tunaweza kuzisanifu vipi.

Lakini pia kuna mwekezaji mwengine aliyejitokeza wa ZANREC, huyu wa Kampuni ya Sweden na yeye anataka kununua haya ma-*plastic* na yeye hivyo

hivyo kutengeneza mbolea, kuona namna gani tunaweza kuzisarifu taka kwa mpangilio huo.

Vile vile nimshukuru Mhe. Waziri, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kwa ule mswada Mhe. Spika, kama ulivyosema. Sasa madhali ZURA tumeshaipitisha, basi haya mambo mengine sasa yatakuja wenyewe kama yanavyopaswa.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala zima la ZAN ID, au kitambulisho cha Mzanzibari, nalo Wajumbe wamelizungumzia. Lakini kama nilivyosema sisi hatuna matatizo na tunahisi kila mwenye haki yake apatiwe kitambulisho cha Mzanzibari. Lakini tunachosisitiza tu kwamba tujitahidi watu wetu wafuate taratibu zilizowekwa.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la wanafunzi wa skuli. Kwa kweli haitokuwa vyema tukawafuata sisi maskulini wao itakuwa kero. Kule waache watoto wasome, lakini kama yupo ambaye keshatimiza miaka 18 na cheti anacho, basi aende kwa Sheha, aende katika ofisi ya vitambulisho atapewa. Nafikiri kama nilivyosema haki hiyo ni ya msingi, kwa sababu kitambulisho cha Mzanzibari sio tu kwa mambo kadhaa, lakini ni kwa mambo yote, kila mahala kinatakiwa kitambulisho cha Mzanzibari.

Mhe. Spika, kulikuwa na hoja nyengine ya Chuo cha mafunzo kwamba wanafunzi wanachanganywa na watoto wadogo. Kwa kweli tumelifuatilia na nimezungumza na wenzangu wa Chuo cha mafunzo Kilimani pale na wamenihakikishia kwamba kwa kweli haliko hivyo hilo suala. Wamenipa mtiririko kama ifuatavyo.

Mahabusu Mhe. Spika, wao ambao ndio wengi wao wanawekwa sehemu yao maalum. Halafu idadi ya wanafunzi hao wa kawaida ambao wameshahukumiwa. Wao wapo kiasi ya nusu ya mahabusu. Halafu wanafunzi watoto wapo sehemu ambayo walikuwa wakikaa wanawake, watoto wamepelekwa kwa wanawake kule, huo ndio utaratibu uliopo hivi sasa, kwa sababu mara nyingi wanawake sio wengi sana. Kwa hivyo, wanafunzi ambao ni watoto wadogo wamewekwa sehemu ya wanawake. Halafu wanawake sasa wanakaa katika sehemu ambayo ilikuwa inaitwa maarufu kwa Ba Mkwe, maarufu jina hilo na wengi wetu tunalifahamu Mhe. Ismail Jussa anakujua keshatembelea mara nyingi sana kule.

Mhe. Spika, halafu kuna wanafunzi ambao wameshakuwa *sentenced* kunyongwa, wao wapo sehemu yao ya asili, ile ambayo sio nzuri kutembelea, lakini ndio huko wanakowekwa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, ile dhana ambayo tulikuwanayo kuwa wanafunzi watoto wadogo wanachanganywa na wengine,

kwa kweli haipo na kama ipo tutazidi kulipiga vita hili suala lisiwepo, sio zuri na halifurahishi na tunajua madhara yake.

Vile vile Mhe. Spika, kulikuwa na suala zima ambalo Waheshimiwa Wajumbe wawili au watatu walilizungumza suala la vijana waliochukuliwa fedha zao kwa kutaka ajira. Kwa kweli naomba niseme kwa uwazi kabisa hili sio serikali wala chama tawala wala mtu yeyote aliyeliagiza. Ni utashi wa watu wenyewe tu. Mhe. Spika, serikali imetoa tamko wazi kabisa kila yule ambaye anahisi katapeliwa basi amtaje huyo aliyemtapeli, na atafikishwa mahakamani. Tayari wapo watu kadhaa ambao wamehusika na suala hili wameshafikishwa mahakamani na kesi inaendelea.

Kwa hivyo, suala hili naomba niwahakikishie Waheshimiwa kama wanao vijana kama hao basi waseme na wajitokeze wawataje hao waliotapeli. Hiyo ni mipango yao wenyewe, hawakuagizwa na mtu yeyote kabisa.

Mhe. Spika, suala la mradi wa ZUSP kwamba unachelewa. Naona kama tumetia chumvi tu, mradi wee, mradi wee. Jamani mradi wa ZUSP upo na utekelezaji kwa kiasi kikubwa au niseme kwa kiasi fulani umeshaanza na baadhi ya mambo yako wazi kabisa. Ukipita Baraza la Mji la Chake Chake utaona magari yameshafika pale ya kuzolea taka, mpaka na vikapu vimeshafika pale na tunatarajia na Unguja nao. Unajua hawa waliopewa walikuwa tofauti, walikuwa sio kampuni moja tu waliopewa kuagiza haya mambo.

Lakini Mhe. Spika, tatizo kubwa lililojitokeza ni suala la washauri. Unajua mradi wowote ni lazima washauri wapatikane. Sasa yule meneja wa World Bank aliyeondoka ndiye aliyetukwamisha, tulikuwa na matatizo naye na kwa bahati nzuri wenyewe World Bank wameliona hilo na akaondoka yule, sasa wamemleta meneja mwengine na tunafanya kazi vizuri sana. Kwa kweli tulivyojulishwa na kitengo cha *management* ya mradi huu ambao uko Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, sisi ni watekelezaji, wizara ya fedha ndio wanaotekeleza mradi huu, wametuhakikishia kwamba kipindi hiki cha Mei/ Juni mambo mengi sana yatakwamuka na *Inshaallah* mambo tunategemea yata-*take off* haraka sana.

Kwa hivyo, nawaombeni sana tusubiri na sisi tuna hamu nao kweli kweli. Najua Mhe. Jussa kwa Mji Mkongwe na Waheshimiwa wengine wana hamu na wao kuona kwamba kweli. Mhe. Hamza Hassan Juma, mitaro yake kule na yeye anasubiri. Usiwe na wasi wasi. Mhe. Fatma Mbarouk wote wa mjini, wa Mji Mkongwe na wa mjini. Rahaleo yale mambo yaliyosemwa yote yapo, hayajafutwa. Kikwajuni yote yapo hayo. Kwa hivyo, tusiwe na wasi wasi jamani yapo na yatakuja.

Mhe. Spika, tatizo unajua unapopanga, kuna tofauti kidogo, unapopanga na utekelezaji. Unapopanga unapanga vizuri, lakini kupanga nako kuna matatizo yake ni lazima tukubali. Hatuwezi kuja kwenye Baraza hili tukaliongopea kwamba tutafanya hivi na hivi hapana. Kwa hivyo, nawaombeni, tuwe pamoja tushirikiane na tuzidi kubadilishana mawazo. Mtuambie, nyinyi kila mkituambia mkitupigia kelele na sisi ndio tunazidi kuchacharika tuone kuwa mambo yanakwenda.

Mhe. Spika,

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tujitahidi na muda.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ahsante Mhe. Spika, namalizia. Kwa kweli

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri atusaidie kidogo kwa faida ya wananchi kwa sababu huu mradi wa ZUSP uko tokea mwaka 2010/2011 na tayari kuna fedha zilikwishatengwa. Je, mpaka sasa hivi bado zile fedha zitaweza kutosha, na kama hazikutosha kuna maeneo gani ambayo yataathirika. Zaidi nilikuwa nataka na wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, kuhusu mtaro wa Darajabovu mpaka Saateni wapate kusikia. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, naomba nimtoe wasi wasi Mhe. Hamza, asiwe na wasi wasi wowote, mipango kama tulivyopanga iko pale pale. Hayo mapungufu ya fedha atuachie sisi na Benki ya Dunia, tumeshawaambia ni kosa lenu, kwa hivyo mutusaidie sisi tuko tayari kukopa zaidi, lakini ni kosa lenu mlirekebishe. Kwa hivyo, turekebishe kwa hali ilivyotokezea, na wao wamesema hapana tatizo na wao tutakwenda nao sambamba.

Mhe. Spika, naomba nisisitize tu kwamba, matokeo ya mradi ule ni kufanya vizuri kwa mradi wetu wa mwanzo wa michirizi, ambao uliopita pale Darajani. Mwanzo kulikuwa na kisingi kidogo tu, taka zinakwama na maji yanatuama. Ulikuja mradi ule wa Ujerumani, ukapitishwa msingi ambao Mhe. Hamza unaweza kupita mzima mzima na ukatokea Bwawani kule. Sasa ule mafanikio yake ndio umezaa mradi huu. Kwa hivyo, naomba Mhe. Spika, suala hili tusiwe na wasi wasi tutajitahidi, tunataka sisi tuone mambo yote yanakwenda vizuri.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema neno moja tu. Mimi nafurahi sana kwa kauli nzuri zetu ambazo tunazitoa hapa Barazani, za ukereketwa wetu tukaushadidia Muungano wetu mpaka tukaonesha picha za waasisi wa Muungano. Lakini nataka kusema Mhe. Spika, haya tunayosema humu ndani ya Baraza basi tuyaseme na nje kweli kweli kwa wananchi, tusiyaseme hapa halafu tukitoka hapa tunakwenda kupanda viriri huko tunazungumza tofauti na tunayozungumza hapa. *(Makofi).*

Mhe. Spika, ukisikiliza baadhi ya hotuba zinazotolewa huko na Waheshimiwa wetu humu wengine, utasema huyu ndiye anayehubiri humu ndani umoja wa kitaifa, Muungano tuudumishe, ndio huyu kweli. Sasa hilo mimi ningeomba sana Mhe. Spika, tukihubiri humu umoja na tupendane na tukienda nje basi tuyaendeleze hayo hayo na tuzungumze hivyo hivyo.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumnukuu kidogo *author* mmoja wa kitabu maarufu hiki. *The rules of management*, ziko 100 hizi, sasa mimi nachukua moja tu. Naomba nisome kwa Kizungu tu anasema;

"Watch your thought they become words, watch your words they become actions, watch your actions they become habits, watch your habits they become character, and watch your character they become your destiny".

Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsate sana Waheshimiwa Wajumbe, mimi nasawazisha moja dogo tu kwenye mtaro ule ambao Mhe. Hamza anaweza akaingia mzima mzima. Mwenyezi Mungu apishie mbali. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kusema machache kuhusiana na mambo mawili. Kwanza kuhusiana na ripoti ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Kamati yetu hii tukufu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Lakini vile vile kutokana na ripoti mpya ambayo imewasilishwa ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kumshukuru sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati hii, pamoja na Wajumbe wake wote kwa mashirikiano makubwa ambayo wametupa. Pia niwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Baraza lako tukufu hili, nao kwa mashirikiano makubwa wanayotuonesha katika utekelezaji wa shughuli zetu na kutusimamia ipasavyo kuona kwamba tunapata utekelezaji ulio wa ufanisi katika shughuli zetu.

Mhe. Spika, karibu Wajumbe wanane walipata fursa ya kuzungumzia juu ya ripoti ya utekelezaji ambayo niliiwasilisha, pamoja na ripoti mpya ambayo imewasilishwa na Mhe. Mwenyekiti wa Kamati.

Mhe. Spika, kwanza naomba nianze kwa kumtanguliza Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati), ambaye aliyapokea yale ambayo tulijibu kutokana na maagizo tuliyopewa na maelekezo waliyoyatoa, ushauri pamoja na maelekezo tunaendelea kuyafuatilia na kuyatekeleza.

Lakini nianze kuwataja wale ambao waliochangia. Tukianza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye alizungumzia suala zima la wawekezaji kuweza kufunga njia na kuleta usumbufu kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, naomba hili nisilizungumze tena kwa sababu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tayari ameshalizungumzia hili.

Mhe. Spika, naomba niendelee kwa kuzungumzia masuala ambayo Mhe. Ismail Jussa Ladhu yalikuwa yamemkwaza na alizungumza sana kwa uchungu juu ya kuchelewa kufika kwa Sheria ya Mazingira ambayo itakuwa imerekebishwa, ili kuweza kusimamia vyema uharibifu wa mazingira ndani ya visiwa vyetu.

Ni kweli *process* hii imechukua muda mrefu, lakini kwa sababu suala zima lililokuja katika ulimwengu hivi sasa ni suala la mabadiliko ya tabia nchi, ambalo katika Sera yetu iliyopita ya mwaka 1992 suala hili lilikuwa halikuzingatiwa ipasavyo. Kwa hiyo, kabla ya kurekebisha sheria tuliona ni afadhali tufanye mabadiliko katika sera ile, ili sheria nayo iweze kusimama katika misingi vyema.

Mhe. Spika, napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wajumbe, kwamba mara baada ya kumaliza Kikao cha Bajeti kitakachofuata, na ni kwa sababu wakati huo hatuwezi kuwasilisha waraka kwa ajili ya kupitisha sheria, basi kikao kinachofuata chengine sheria hii naahidi kwamba italetwa hapa Barazani kwa ajili ya kupitishwa. *(Makofi)*

Vile vile Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitaka kujua kama kuna dawa ambazo zimekamatwa hivi karibuni. Kwa kweli na kwa taarifa ya Waheshimiwa Wajumbe tu, kwamba katika vyombo vyetu vya habari hasa katika mitandao na vyombo vya habari kulitangazwa kwamba mnamo tarehe 29 mwezi wa Machi, kulikamatwa meli nje ya mwambao wa Zanzibar ambayo ilikuwa na shehena ya nusu tani ya dawa za kulevya aina ya *heroin.*

Dawa hizi zilikamatwa katika *operation* maalum iliyokuwa inafanywa na Jeshi la Majini la Wananchi wa Canada na Australia. Lakini kwa

mashirikiano makubwa ya mataifa mengine 27, kwa hivyo hii ni *operation* ya kimataifa.

Mhe. Spika, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, warudie maneno yangu ambayo ninakuwa nayazungumza sana hapa kuhusu suala zima la kupambana na usafirishwaji na uingizwaji wa dawa haramu ni zito na linahitaji nguvu za pamoja za taifa kwa taifa, kanda kwa kanda, lakini pia za kimataifa.

Kwa kweli hii moja wapo ilikuwa ni juhudi ya kimataifa na kwa maelezo yaliyotolewa kwamba mara ya kwanza ni katika historia kiwango kikubwa cha dawa kimekamatwa katika mapambano ambayo ni ya ukamataji wa dawa ndani ya bahari.

Sasa naomba kujibu swali kwamba kwa taarifa tulizozipata dawa hizi zilikamatwa nje ya mwambao wa Zanzibar, kwa hiyo hazikukamatwa ndani ya Zanzibar na kwa kuthibitisha hilo hata katika Jeshi letu la Polisi Zanzibar taarifa hii hawakupokea ripoti yoyote.

Taarifa nyengine katika mitandao hiyo zinaeleza kwamba ni eneo ambalo labda linatizamana na Zanzibar au linaweza kuiona Zanzibar kwa mbali, lakini si katika eneo la Zanzibar. Vile vile taarifa nyengine zinasema karibu na Tanzania, lakini katika eneo ambalo halijatajwa hasa labda meli ngapi kutoka mwambao wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakubaliana sana na Mhe. Mwakilishi kwamba tunahitaji kuviboresha vikosi vyetu hasa hivi vya Wanamaji na kuvipatia vifaa bora, ili kuweza kushiriki katika mapambano hayo. *(Makofi)*

Lakini kwa sababu tu meli hizi au vikosi hivi vya kigeni vilikamata dawa hizi haimaanishi kwamba vikosi vyetu havina uwezo, isipokuwa tatizo tulilonalo ni kwamba uwezo upo, lakini jitihada za pamoja zinahitajika za kiintelejensia.

Mhe. Spika, ukiifuata zaidi hadithi hii utaona kwamba meli hii ilikuwa za kiintelejensia karibu miezi miwili nyuma ilionekana ikitokea Pakistani. Kwa hiyo, ikawa *trusted* na hata ndege ya Canada ilitumika katika ku-*locate* wapi ilipo kwa kuweza ku-*intercept* kukamata dawa hizo. Kwa hivyo, juhudi za pamoja zinahitajika katika shughuli hii. *(Makofi)*

Pia Mhe. Mjumbe alitaka kujua nini hatima ya shimo kubwa la Bumbwini ambapo kumekuwa na kutupiana mpira kati ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Mhandisi wa *MECCO*, ambaye alijenga barabara ile ya Mfenesini na Bumbwini.

Suala hili ofisi yangu imelifuatilia na tumeahidiwa kwamba litafuatiliwa kwa kina kuona kwamba eneo lile linaendelezwa na *MECCO*, kwa sababu *MECCO* kidogo ametingwa na masuala ya fedha, yaani anao mtihani mkubwa katika kumalizia barabara ya Wete na Gando kutokana na ukosefu wa fedha.

Lakini Wizara imeahidi kwamba itafanya kila jitihada kwa kushirikiana na *MECCO* kuikabili hii hali, ili hili eneo liweze kutumika na ikiwezekana basi hata kuacha kumlipa mkandarasi huyu fedha zake zote mpaka hapo eneo hili litakapoweza kushughulikiwa. (*Makofi*)

Nikiendelea na ufafanuzi Mhe. Spika, kuna Mhe. Mjumbe mwengine ambaye alichangia ni Mhe. Ali Salum Haji, kwa kweli tunapokea pongezi na tunachukua mawazo yake katika kuhakikisha kwamba Kampeni dhidi ya Marufuku ya Mifuko ya *plastic* inakuwa endelevu, ili kunusuru maisha yetu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, natoa wito kwa yale ambayo aliyaona yeye kutokana na vyombo vya *Azam Marine*, napenda niwapongeze sana kwa jitihada wanazochukua kuhakikisha kwamba sheria yetu hii inatekelezeka kwa kuweza kutoa mifuko mbadala kwa wasafiri wanapokuja ndani ya visiwa vyetu. Kwa hivyo, natoa wito kwa vyombo vyengine vyote kuweza kufuata mfano huo, ili tusaidiane.

Mhe. Mgeni Hassan Juma naye alichangia na alitaka kujua zaidi vipi serikali inazisaidia *Sober House*. Mhe. Spika, napenda nimueleze kwamba sisi tunathamini sana kama serikali juhudi nzima za uanzishwaji wa *Sober House* na Taasisi Binafsi, nisingependa kurudia asubuhi hii ya leo na Mhe. Mjumbe alikuwemo humu ndani nilieleza jinsi gani serikali inazisaidia. *(Makofi)*

Nadhani ni vyema nimueleze tu kwamba serikali haijakataa jukumu lake wala haijaondosha nia yake ya kuwa *rehabilitation* yake yenyewe kwa ajili ya kuwashughulikia vijana hawa. Mhe. Spika, tunafanyia kazi kiwanja tunacho tayari, isipokuwa tulichokwama kidogo ni kwamba serikali ina mambo mengi sana, kwa hiyo tunafanya kwa awamu, ili kuhakikisha kwamba na serikali tunachukua jukumu letu la kuwashughulikia vijana wetu hawa ambao ni watoto wetu wanaoathirika na dawa hizi za kulevya.

Mhe. Mjumbe pia alitaka kujua vipi udhibiti wa ndege wetu tuliozoea wa asili, ndege kama vile mnana na wengine. Mhe. Spika, napenda kumkumbusha Mhe. Mwakilishi kwamba kampeni ambayo inaendeshwa katika mradi uliopo katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa kuwaua kunguru ni njia moja wapo ya kuwadhibiti ndege hawa, ambayo tuliona kwamba kunguru wanawala kwa wingi na kuwaondosha katika maeneo yao.

Vile vile ofisi yangu imeandaa andiko la mradi na tayari imeshaliwasilishwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa ajili ya kupelekwa *costec* kwa lengo la kupata ufadhili wa kufanya utafiti sasa jinsi gani tunaweza kuwahifadhi ndege wetu hawa wa asili katika maeneo yetu.

Mhe. Farida Amour Mohammed naye alikuwa na *concern* kubwa juu ya bidhaa chakavu. Mhe. Spika, ni kweli nikubaliane naye kwamba hii ni changamoto kubwa inayotukabili katika suala la mazingira Kwa hivi sasa na athari za bidhaa hizi chakavu zinaeleweka kwamba ndani yake zina sumu na tusipodhibiti sawa sawa zinaweza kutuchafulia vyanzo vyetu vya maji na kusababisha uharibifu wa mazingira katika hali ya juu.

Mhe. Spika, nipende kumuarifu Mhe. Mjumbe, kwamba tatizo kidogo hili suala limekuwa gumu, lakini halishindikani kwamba vijana wetu wengi ambao hawana kazi au ajira wanajishughulisha katika bidhaa hii ya kuuza bidhaa hizi chakavu. Hata hivyo, wananchi wetu wa Zanzibar nao kiwango chao cha hali ya uchumi, yaani soko hili la bidhaa chakavu linawasaidia kupata baadhi ya vifaa ambavyo wanavitumia katika maisha yao.

Sasa ofisi yetu ikishirikiana na wadau wengine inapima jinsi gani tutaweza kwa wakati mmoja kutowaondolea ajira vijana wetu, kutowakatisha kupata mahitaji wananchi wetu ambao hali yao ya uchumi ni ndogo pamoja na kudhibiti hali ya uchafuzi wa mazingira.

Mhe. Spika, tunakusudia katika hili kuweza kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko katika kutayarisha viwango vya ubora vya vifaa hivi vya *second hand*, ambavyo vitaweza kuingizwa badala ya kupiga marufuku kabisa suala hili.Kwa kweli hivi karibuni Mhe. Spika Baraza lako litaarifiwa juu ya hatua zinazoendelea katika hili.

Mhe. Mjumbe alielezea zaidi juu ya suala zima la dawa za kulevya na nisingependa nirudie tena, kwani tayari nimeshalitolea maelezo juu ya ugumu wake.
Mhe. Fatma Mbarouk Said, kwanza napenda nipokee pongezi alizonipa pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wengine kutokana na kukabidhiwa Tunzo ya Mwanamke Jasiri katika mwaka huu wa 2013 na Balozi wa Marekani. *(Makofi)*

Mhe. Mwakilishi naye alizungumzia suala zima la uchafuzi wa mazingira. Mhe. Spika, nilizungumza kwamba ofisi imetayarisha Kanuni za Kusimamia Maliasili zisizorejesheka, kanuni hii itatusaidia kwa hivi sasa kuongeza ufanisi juu ya kusimamia uharibifu wa mazingira ndani ya visiwa vyetu,

sambamba na hilo Sheria mpya ya Mazingira nayo itatusaidia katika kukabiliana na hali hii.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla naye alizungumzia kuhusu suala zima la uharibifu wa mazingira na mmong'onyoko wa fukwe. Mhe. Spika, niseme kwamba awali kulikuwa na tatizo kwamba kufanya *Environmental Impact Assessment* kwa wawekezaji ilihitajika tu kwa wale wawekezaji ambao walikuwa wanajenga hoteli yenye vitanda kuanzia mia moja.

Sasa suala hilo sisi tunaliona kwamba ni mapungufu na tunalifanyia kazi na kwa tunavyojipanga sasa, basi hakuna mwekezaji ambaye ataanzisha mradi wake kabla haujafanyiwa tathmini za athari za kimazingira, kwa hiyo tunahisi tutaweza kwa pamoja kulizuia.

Mhe. Mjumbe, pia alizungumzie suala zima la mtu ambaye anasema anamuelewa na yuko kwenye Jimbo lake sehemu ya Pujini mwenye kukata kwa wingi mno miti ya mikoko katika hali hii inayotisha hivi sasa ya nchi yetu kuweza kuingiliwa na maji ya bahari kwa wingi.

Mhe. Spika, namuahidi Mhe. Mjumbe kwamba nitakaa naye, ili anipe taarifa kikamilifu kwa sababu kwa kadri inavyoelewa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar hakuna mtu yeyote aliye juu ya sheria na sheria za kumbana zipo, kwa hiyo tunalishughulikia suala hili na nitaonana naye Mhe. Mwakilishi kwa ajili ya kunipa taarifa zaidi. *(Makofi)*

Naomba nimalizie Mhe. Spika, kwa mchango wa Mhe. Saleh Nassor Juma, ambaye alielezea suala zima la athari za kimazingira kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na je vipi serikali inapanga bajeti ya kiasi gani.

Mhe. Spika, kwa mara ya kwanza Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira itakuwa na bajeti ya kupambana na athari za kimazingira japo kuwa haitakuwa kubwa, kwa sababu tatizo hili ni kubwa, Mhe. Spika watakumbuka Waheshimiwa Wajumbe nikieleza kwamba karibu maeneo 125 ya Unguja na Pemba yanakabiliwa na athari hii ya kuingiwa na maji ya chumvi kutoka baharini.

Kwa hivyo, tumepata fedha kidogo za wafadhili na tunafanya tathmini na mpango Mkakati wa jinsi ya kushughulikia na kuandaa vipaumbele wapi tuanze na nini tufanye katika masuala haya. Mhe. Spika, hatuja-*relax* na tunalifanyia kazi kwa kuona kwamba nchi yetu inapata athari kubwa na inaathiri hali ya uchumi ya wananchi wetu, kwa sababu athari za mabadiliko ya tabia nchi Mhe. Spika tayari zinaonekana kupiga katika eneo la utalii,

kilimo na maeneno mengine kama vile ya uvuvi katika suala zima la kazi ambazo zinafanywa na wananchi wa visiwa vyetu.

Mhe. Mwakilishi naye alielezea kuhusu suala zima la jinsi ya mapambano ya dawa za kulevya. Mhe. Spika, kama nilivyoeleza kwamba ofisi yetu imeandaa *road map* kwa ajili ya kuonesha jinsi gani kila mdau ataweza kushirikiana kwa pamoja katika vita hivi vya mapambano dhidi ya dawa za kulevya ingawaje ugumu wake sote tunaweza kuuona.

Vile vile Mhe. Mjumbe alizungumzia suala la *Sober House* ambalo tayari nimeshalitolea maelezo na nafikiri amepata.

Mhe. Spika, jengine ambalo alilizungumzia la mwisho sana kwa masikitiko ni suala zima la kuwashughulikia ndugu pamoja na watoto wetu ambao wanaishi katika hali ya ulemavu kuhakikisha kwamba miundombinu inakuwepo ya kuwawezesha kufika, basi na wao katika sehemu ambazo wanazozihitaji kufika kwa kupata huduma kusiwe na vizingiti vyovyote.

Mhe. Spika, niseme suala hili tunalizingatia na kwa sasa majengo yote ambayo yatajengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi basi yanalazimika kabisa kuweka miundombinu inayowawezesha ndugu zetu wenye ulemavu kuweza kufikia maeneo hayo na kwa kweli tunapata mashirikiano makubwa. Kwa mfano, hivi karibuni jengo letu la *ZRB* mukilichunguza mtaliona limejengwa katika utaratibu huo na sisi tutasimamia zaidi tukishirikiana na Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati kuhakikisha kwamba hilo linafanyika.

Mhe. Spika, niwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na waendelee kutupa mashirikiano yao nathamini sana maneno ya Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ambaye alikuwa mkali najua kwa nini alikuwa mkali, tena najua nia yake ni kutufanya tufanye kazi kwa ufanisi zaidi, ili nchi yetu ipige hatua za maendeleo kwa haraka zaidi na sio vyengine vyovyote.

Nawashukuru sana, Mhe. Spika naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Waziri ambaye ni Mwanamke Jasiri kwa uwasilishaji ya Taarifa hii ya Utekelezaji. Kwa hivyo, tumalizie hatua hii ya kwanza kwa kumkaribisha Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. (*Makofi*)

Imani yangu Mheshimiwa atachukua muda mfupi, ili tuweze kumaliza shughuli hii mapema iwezekanavyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Spika, kwanza na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kutoa ufafanuzi kuhusu michango kwanza ya Waheshimiwa Mawaziri pamoja na Waheshimiwa Wajumbe Wawakilishi.

Lakini kabla sijaanza Mhe. Spika, kama unavyojua Kamati yangu ni nzito, yaani ni Kamati inayosimamia viongozi Wakubwa sana katika nchi hii ingawa viongozi wote wanavyo vimurimuri, isipokuwa yeye Mwenyekiti hana. *(Vicheko/Makofi)*

Kwa hivyo, nitaomba kidogo unipe nafasi, ili niweze kutoa ufafanuzi wa kutosha kabisa, kwa sababu nikiweza kutoa ufafanuzi wa kutosha napunguza maswali hata huko mbele tunakokwenda pia. Mhe. Spika, nitajitahidi nitumie muda wako vizuri na pia kwa faida ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kimsingi sina mambo mengi sana au makubwa, isipokuwa nitahitaji nitoa ufafanuzi wa kutosha, ili yale maeneno ambayo tumeyazungumza pamoja na kwenye zile ziara ambazo tulizoitwa na wananchi mbali mbali, wahisi kwamba Waheshimiwa Wajumbe wao wanapokwenda kuwaeleza matatizo yao, basi kweli matatizo yao yanafika serikalini.

Kwanza nataka niwataje Waheshimiwa Wajumbe waliochangia hoja zangu ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
2. Mhe. Ussi Jecha Simai
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu
4. Mhe. Ali Salum Haji
5. Mhe. Mgeni Hassan Juma
6. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
7. Mhe. Farida Amour Mohammed
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Saleh Nassor Juma
10. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
11. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na
12. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Mhe. Spika, baada ya kuwatambua na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote waliochangia hotuba yangu, sasa nitaomba moja kwa moja niende kwenye ufafanuzi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alisema kwamba gari za *escort* za viongozi ni mbovu. Vile vile Mhe. Mjumbe alisema kwamba jitihada hazionekani labda wenzetu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hatuelezei hasa matatizo na alitoa mfano mzuri kabisa.

Wakati walipokwenda kwenye Kamati Mhe. Ali Mzee Ali yeye moja kwa moja alitamka tu kwamba kuna gari zina matatizo basi wiki ile ile gari zilifanyiwa utaratibu zikaja. Pamoja na hayo, Mhe. Mwakilishi alizungumzia masuala ya Muungano.

Mhe. Spika, sasa naomba kutoa ufafanuzi sio kama, kwa sababu haya majibu yameelekezwa zaidi kwa serikali. Lakini alieleza kwamba labda Kamati haifuatilii vizuri masuala haya.

Mhe. Spika, nataka nikuthibitishie kuhusu suala la *escort* gari za viongozi maarufu hapa Zanzibar tunaviita visakina, ni kweli gari zile zimechoka tena sana na ni hatari kwa kuwa-*escort* Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa. Kwa mfano, sisi wenyewe tunashuhudia misafara ya viongozi hao inavyokuwa na *speed* kubwa. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, tuliishauri serikali katika Baraza lililopita, kwamba Viongozi wetu hawa Wakuu gari zao zisizidi zaidi ya miaka mitano, yaani kila baada ya muda watafutiwe gari mpya. Kwa kweli tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Sita, iliweza kusikia kilio chetu na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikanunua gari mpya kabisa kwa Viongozi wetu Wakuu wa Kitaifa.

Sasa nadhani Mhe. Spika, si busara gari ambazo mpya zina nguvu zikawa-*escort* na gari ambazo tayari zimechoka. Jambo hili tulilizungumza wakati tulipokwenda Dar-es-Salaam na Kamati yangu na tulikutana na Uongozi wa Jeshi la Polisi Tanzania chini ya Uongozi wa mwenyewe *IGP*.

Kwanza Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati yangu tunamshukuru sana *IGP* na tunamshukuru kwanza kwa kukubali kutupokea, lakini Mhe. Spika alitupa mashirikiano makubwa sana. Vile vile alitupa uwanja na kutuambia Waheshimiwa Wajumbe mumekuja na sisi hatujui hasa mlichokijia, isipokuwa mlitaka kujua masuala ya ajira, nyumba na mambo mengine, lakini alitupa uwanja na kutuambia hebu zungumzeni nini ambacho mnachohisi tuna mapungufu kwa upande wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Kamati yangu na nataka nimshukuru zaidi Mhe. Mgeni Hassan Juma ingawa yeye bado hajapata nafasi ya kupewa kile cheo cha Mwanamke Jasiri, lakini kwa kweli Mhe. Mgeni Hassan Juma ni Mwanamke Jasiri kweli.

Kwa kweli maneno aliyoyasema kule mimi mwenyewe sikuamini kwamba yule ndiye Mhe. Mgeni ninayemjua mimi, yaani alitoa macho na povu la mdomo linamtoka, lakini kwa nia ya kuisaidia Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na mvuto na hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yako nzito ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Mhe. Spika *IGP* alituahidi na alitujibu pamoja na kututolea ufafanuzi wa mambo yote haya. Lakini alituahidi kwamba Waheshimiwa Wajumbe ninakuombeni haya niliyokuelezeni mimi basi naomba nije nilieleza Baraza zima.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, nategemea *IGP* pamoja na Uongozi wake wa Jeshi la Polisi Tanzania watakuja ndani ya kipindi hichi yaani tuko ndani ya Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kutupatia semina vile vile na sisi tutapata kuwaeleza yetu ambayo tuliyonayo. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, hii ndio ninamfahamisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba Kamati yako imefanya kazi ya ziada ya ile aliyoifanya Mhe. Ali Mzee Ali. Kwa hiyo, Mhe. Spika tutegemee semina hiyo na tujiandae Waheshimiwa Wajumbe na ninaomba sana tusijekuwa na jazba, isipokuwa tuzungumzie namna ya kuliboresha Jeshi letu la Polisi lakini kwa kuweza kuisaidia Zanzibar pamoja na usalama wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Miongoni mwa mambo ambayo aliyotuahidi ni kwamba wataangalia bajeti ya mwaka huu kuangalia uwezekano wa kuweza kubadilisha hizi gari za *escort* za viongozi. Lakini pia alituahidi kwamba tuliwahi kujenga mabanda ya farasi hapa Zanzibar hayakuwahi kumaliza, basi aliahidi kwamba atayamaliza na tayari wapo farasi wetu watatu wawili majike na moja dume wataletwa Zanzibar kwa ajili ya kusaidia ulinzi katika Jeshi la Polisi pamoja na wananchi wetu wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Ussi Jecha Simai, naye alielezea kuhusu suala la bango tulilolikuta pale tulipotembelea Paje Bango la *Crystal*. Mhe. Spika, ni kweli na hili namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba kuna ndugu zetu wa *Crystal Hotel*, ambao wao wamejenga Nyumba za Makaazi ya Polisi pale, baada ya kujenga zile nyumba wakaweka lile bango lao pale kuwa huu ni ufadhili wa *Crystal Hotel*.

Lakini kutokana na matendo ya uongozi wa *Crystal Hotel* kuwanyanyasa, kuwafanyia vituko na maudhi wananchi wa Paje, basi Mhe. Spika wananchi wa Paje wameanza kukosa imani na mwekezaji yule na kimsingi wanafanyiwa vituko vingi. Kwa mfano, wanafukuzishwa mbwa wanapopita kule ufukweni baharini. Mhe. Spika, suala hili naomba sana Ofisi ya Makamu

wa Pili wa Rais kupitia Jeshi la Polisi waweze kulichukulia hatua za haraka. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wakati mwengine wananchi hasa wanapofanyiwa vitengo vya aina kama hiyo wanaogopa hata kwenye kituo cha polisi, kwa sababu anayekwenda kumshtaki tayari kuna bango yeye ni mfadhili aliyejenga zile nyumba. *(Makofi)*

Sasa tunaiomba sana serikali kwamba ili kurejesha hadhi ya Jeshi la Polisi na katika eneo la Paje, basi tunaomba bango lile liondolewe na kwa sababu tayari tumejaribu kufuatilia kwamba kile kituo cha polisi kuna mfadhili mzalendo wa kizanzibari ambaye amekijenga na wala hakuandika jina lake. Kwa hivyo, ili Jeshi la Polisi lisidhalilike, basi tunaomba bango lile liondolewe kwa ajili ya kurejEsha imani ya wananchi hasa katika eneo la Paje. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu alinilaumu kidogo na kusema Kamati haikupata majawabu ya kutosha. Mhe. Spika, nataka nikuthibitishie maagizo mengi ambayo tuliyatoa katika kipindi kilichopita, kwa kweli tunamshukuru sana Mhe. Waziri amekuwa akiyatekeleza kwa vitendo na kuna mengi anaendelea na hapa nakusudia Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ripoti ya Kamati yangu iliyopita iko tofauti sana na ripoti ya mwaka huu, kwa sababu ripoti ya mwaka jana nilikuwa mkali sana, kwa sababu tulikuwa tunaona kuna mambo mengi hayafanyiki vile wananchi wanavyotarajia. Lakini tunashukuru mambo mengi yameanza kurekebishwa na ndio maana safari hii ukakuta ripoti yangu iko laini kwa kiasi fulani. Kwa hiyo, pamoja na ulaini wake bado Kamati yangu itaendelea kufuatilia haya ambayo tuliyoyaahidi au Waheshimiwa mawaziri wetu waliyoyaahidi. Kwa hivyo hili Mhe. Jussa asiwe na wasiwasi wala Mhe. Dr. Mwinyi mimi na yeye hatujawahi kukaa pembeni tunafanya kazi tu kwa pamoja tunashirikiana vizuri katika kazi zetu.

Mhe. Spika, Mhe. Jussa vile vile alielezea ripoti iliyopita kuna mambo mengi ya muungano ambayo waliyahoji kama Kamati na mpaka leo bado hayajapatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, mimi nataka niwaambie wenzangu, mimi nishashiriki vikao vingi vya kero za muungano. Mheshimiwa mambo haya tumepata nafasi Wazanzibari tumetoa maoni yetu mimi nadhani kwa sababu kuna mambo mengi tatizo lake utekelezaji wake una utata kisheria na kikatiba. Lakini vile vile kuna mengine yamo ndani ya katiba lakini hayana muongozo ni namna gani yatatekelezwa katika utaratibu gani. Sasa mimi nadhani kama tulimfuatilia sana Mhe. Mwanasheria Mkuu alipokuwa akituaidhi katika maoni mbali mbali mimi naomba sana tuangalie ile *paper*

yake, kuna mambo yamo kikatiba, lakini katika utekelezaji yanashindwa kutekelezeka kikatiba kwa sababu hakuna muongozo mwengine ambao unaofuata.

Sasa mimi nadhani fursa tumeipata wananchi wetu wamesema mpaka wamemaliza maneno, keshokutwa madiwani wetu watashiriki katika mabaraza ya katiba na wengine wajumbe watakaoingia kule wajaribu kuangalia ni matatizo gani ambayo yanayokwaza utendaji wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili tuweze kuyarekebisha. Lakini sio hivyo tu Baraza la Katiba Mhe. Spika, linamalizia kwetu sisi kama Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, tukija tukiyabakisha mambo ambayo yataendelea kuwa na utata Mhe. Spika, hapa hatutokuwa na nafasi tena ya kumlaumu Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar.

Kwa hivyo tuwe makini Waheshimiwa kuna mambo mengi ambayo yanahitaji mabadiliko makubwa ya kisheria, mengine mabadiliko makubwa ya kikatiba kwa hivyo ndio maana sikuwa na haja ya kuyarejea, kwa sababu kama kuyasema tumeshayasema sana, jitihada tumeziona mimi mwenyewe nishashiriki, kuna mambo mengine yanaamuliwa unaambiwa yatatekelezwa tukirudi tena hayakutekelezwa, kwa sababu tunaambiwa kuna sheria gani, kwa hivyo ndio maana Mhe. Spika, ninajua unajaribu kuangalia muda lakini ninahisi hili nilikuwa nilitolee ufafanuzi ili tusije tukaonekana kwamba yale ndio yameisha.

Mhe. Spika, nikiendelea Mhe. Ali Salum Haji alieleza suala mgongano wa sheria za Mji Mkongwe na hili Mhe. Spika, tuliwashauri Waheshimiwa Mawaziri wawili. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi lakini vile vile na Mhe.Waziri wa Ardhi Makaazi Maji na Nishati ili kukaa kuwaita taasisi hizi mbili, Mhe. Rashid Seif naomba nipe raha kidogo wakae na hizi taasisi mbili vyenginevyo Mhe. Spika, itakuja kuwa ni aibu kubwa bustani ile iliyojengwa kwa ufadhili wa wenzetu *Agakhan foundation* baada ya muda mchache bustani ile ikaja ikapoteza haiba yake. Mhe. Salmin alizungumza hapa alipokuwa akichangia ile taarifa ya serikali. Tunasaidiwa mambo mengi lakini je tunayaendeleza haya mambo tunayosaidiwa isiwe kila siku kazi yetu kusaidiwa halafu baadae jambo lile likaharibika. Sasa hili nawaomba Waheshimiwa mawaziri wakae na mamlaka ya Mji Mkongwe pamoja na Baraza la Manispaa ili ajulikane hasa nani mwenye *mandate* ya kuweza kuishughulikia bustani ile. Mhe. Spika, bustani ile imebadilisha hata sura ya mji wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, Mhe. Ali Salum alidokeza neno hapa na neno alilodokeza kwa kweli ni suala zito ni lazima serikali yetu suala hili isilifanyie mas-hara, amezungumza mambo mawili ya ubadhirifu wa fedha za serikali. Mhe. Spika,

mimi nataka kusema hata jana nilipokuwa nikichangia hii hotuba yangu nilimuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais awe mkali. Sasa hivi watendaji wa serikali hawaogopi, hawamuogopi Makamu wa Pili wa Rais, wala hawaiogopi serikali. Mhe. Spika, kelele tunazozipiga hapa kuhusu suala la ubadhirifu wa mali ya umma leo mwaka mmoja tu tumerudi tena hapa kuna watu washachota wengine milioni 60, wengine zaidi ya bilioni moja na nusu.

Mhe. Spika, narudia msemo wa rafiki yangu sahibu yangu Mhe. Rashid Seif alipokuwa mwenzetu *are we serious!* Sasa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hasa haya mambo mawili aliyoyazungumza Mhe. Ali Salum Haji ayasimamie kidete na ahakikishe kwamba hao waliotufanyia uovu huu basi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa. Mhe. Spika, Balozi kweli mpole lakini katika kazi suala la upole halitakiwi, tunataka asimamie mali za serikali ili fedha zisiendelee kuvuja. Na vile vile Mhe. Spika, kama halijatekelezwa hili basi sisi maana ya kuja hapa Barazani bado itakuwa haisaidii. Kwa sababu ina maana chombo hiki kazi yake kusema, tunatafuna hapa pesa za umma lakini hakuna hatua zozote ambazo zinazochukuliwa. Kwa hivyo naomba hili Mhe. Spika, lichukuliwe hatua za dharura au hatua maalum.

Mhe. Spika, alizungumzia tena suala la unyanyasaji wa Hoteli ya *Crystal*, hili vile vile nataka niseme kwamba kamati yangu katika hii ripoti mwisho huku nilikuomba Mhe. Spika, kwamba kutokana na ile kadhia iliyopo pale kwa sababu sisi tuliendea jambo moja suala la wananchi kuzuiliwa njia kwenda baharini na suala la kuzuiwa wasitumie fukwe. Lakini tuliyoyakuta pale Mhe. Spika, ile hoteli inahitaji ukaguzi wa dharura, na naomba Mhe. Spika, katika ripoti yangu nimeeleza naomba sana uiagize Kamati yetu ya Uchumi na Fedha kwanza kama wamefuata yale masharti ya ZIPA kwa sababu ZIPA iko chini ya Kamati ya Uchumi na Fedha. Lakini vile vile wafuatilie uhalali wa ulipaji kodi wa yule muwekezaji.

Mhe. Spika, tumevikuta vibanda ambavyo hatuwezi kuamini kwamba yule ni muwekezaji wageni kawalaza kwenye vibanda vya *full suit*, mbao kuanzia chini kuti mpaka juu. Tunauliza je wale wageni wanaolala katika nyumba zile wanakuwa *registered?* Sasa tunaomba Mhe. Spika, tukimaliza Baraza lako hili naamini utafanya maarifa yoyote ili kuwawezesha Wajumbe waende, naamini ndani ya wiki moja kazi ile wataweza kutuletea ripoti ambayo itakayoweza kuturidhisha kabisa. Kwa sababu tuna wasiwasi ukiacha ule unyanyasaji na maneno ambayo aliambiwa Mhe. Mgeni na mlinzi wa hoteli ile akasema aa nyingi kazi yenu bure tu sisi serikali tumeiweka hapa mkononi. Sasa kwa kweli ile ni kauli ya dharau kabisa.

Sasa kama serikali ameiweka mkononi tena amesema Ofisi ya Mkoa, ZIPA tumewaweka mkononi sijui Ardhi tumewaweka Mkononi, sijui nani Mkuu wa Mkoa, lakini sasa Mhe. Spika, ili kuthibitisha kwamba Baraza la Wawakilishi halitiwi mkononi kwa mtu basi uitume Kamati yako iende ikachunguze haya ambayo tuliyoyashauri.

Mhe. Spika, kwa hivyo hoja ya Mhe. Ali Salum kuhusu unyanyasaji wananchi wa Paje kwa muwekezaji wa Hoteli ya Crystal tunaomba na ingawa Mhe. Waziri alizungumza kwamba amepeleka kesi mahkamani. Mhe. Spika, tulielezea maeneo karibu sita aliyepeleka mahkamani ni maeneo mawili tu, eneo la kuzuia lile geti alilojenga kwenye ile njia waliyokuwa wanapita wananchi na kesi nyengine amemzuia muwekezaji mzalendo, amemfungia njia asiingie katika eneo lake ambao amelivamia analitumia.Sasa hayo mawili tutaiachia mahkama ifanye maamuzi yake. Lakini mengine kuhusu kufuatilia ulipaji wa kodi za serikali na uhalali wa uwekezaji wake kama umefuata masharti ya ZIPA hilo haliko mahkamani kwa hivyo naomba Mhe. Spika, Kamati yako ya Uchumi na Fedha uiruhusu iende ikafanye kazi hiyo.

Mhe. Spika, alizungumzia suala la mifuko ya *plastic* amemshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na mimi pia namshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Mwanamke jasiri ameweza ku-*fight* akapambana na mifuko ya *plastic*. Lakini wananchi unajua siku hizi Mheshimiwa tunapozungumza hapa wananchi wanatutumia ma-*message* wanatupa changamoto mbali mbali. Wananchi wametueleza vipi wamenieleza mimi Mheshimiwa mwanamke jasiri ameweza kupambana na mifuko ya *plastic*, tunamuomba sasa apambane na ma-*pampers* yaliyojaa kila uchochoro. Mhe. Spika, sasa hivi ma-*pampers* ni hatari. Leo watoto wetu wadogo wengine wanatembea katika majaa wanatembea maeneo mbali mbali zikija mvua kama hizi Mhe. Spika, ukiona maji yanatiririka usiyakanyage hatari ma-*pampers* kwa hivyo naomba Mhe. Waziri hili naomba uweze kulishughulikia.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni alieleza malalamiko ya *government press* nadhani Mhe. Waziri, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anatusikia na tunashukuru tumeweza kutatua tulikaa na uongozi wa Idara ya Uchapaji pale lakini bado kuna malalamiko ya wale wafanyakazi tunamuomba sana Mhe. Waziri kama alivyotueleza katika ripoti yake kwamba ahakikishe kwamba yanakamilika na ni vizuri wafanyakazi wale Mhe. Spika, kabla ya kuhamia katika jengo jipya la *government press* Maruhubi na Mitambo mipya basi si vizuri kuondoka na madeni wakahamia kwenye jengo jipya. Na madeni yenyewe Mhe. Spika, Mhe. Mwalim Haroun naomba unipe raha Mhe. Spika, hayo madeni yenyewe wala si makubwa sana. Kwa hivyo nadhani wale wafanyakazi ili wakalifungue lile jengo la Maruhubi kwa furaha basi ni vizuri hiki kidogo

ambacho kilichokuwa kimebakia waweze kulipwa ili wafanyakazi wetu wakaanze kazi kwa raha kabisa.

Mhe. Spika, sherehe za miaka 50 ninafikiri Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameyazungumzia vizuri, lakini Mhe. Spika, kulikuwa na ombi maalum la Kamati yetu Mhe. Waziri hakutupatia ufafanuzi lakini najua hili atakwenda kulifanyia kazi kwa utekelazaji. Tulimuomba kwamba kwa kuwa Mapinduzi ya Zanzibar nchi ya mwanzo kuyatambua Mapinduzi ya Zanzibar ilikuwa ni nchi ya China basi tunamuomba sasa wamuandikie barua rasmi mapema ili aweze kutafuta nafasi Rais wa China aje ashiriki katika sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na pengine Mhe. Spika, inawezekana na ule mchakato alozungumza Waziri wa Fedha na Mawaziri wengine na ile *package* ya ile miradi yetu mengine pengine inawezekana katika sherehe za Mapinduzi akaja akatwambia basi ile bandari ya Mpigaduri haya endeleeni. Kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Spika, tunamuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais aweze kufanya *lobbing* hizo ili tuweze kumpata Rais wa China, kwa sababu hii tunampa heshima na tumwambie hasa nyie ndio mlotutambua mwanzo kwa hivyo tunataka mje mthibitishe kwamba yale Mapinduzi bado tunayaenzi tumeshafika miaka 50. Lakini bado uchumi mdogo tunataka Bandari. Kwa hivyo mimi nadhani Mhe. Spika, hili nafikiri litaweza kutekelezeka.

Mhe. Spika, alielezea Mhe. Mgeni kuhusu kazi za Afisa wa Habari. Kamati yangu ilipotembelea Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais tukapigwa chai pale tunashukuru viburudisho kidogo havikupambana na mkumbo wa meli, kwa hivyo tunamshukuru Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, lakini tatizo tulililoligundua pale, mimi niliuliza mbona hiki kikao kizito sioni Afisa wa Habari, kwa hivyo kikao chetu kilifanyika hatukuwa na Afisa wa Habari.

Sasa nimeelezea hapa na katika suala la Maafisa wa habari sio Wizara hii tu ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Spika, bado Maafisa wa Habari hatujaweza kuwatumia vizuri. Mhe. Spika, masuala mengi wanayotuuliza wananchi kama Maafisa wa Habari wa Wizara zote wangekuwa wanafanya kazi yao vizuri Mheshimiwa hata maswali Barazani yangepungua.

Mhe. Spika, Mhe. Rais tulimsikia alipokuwa akifanya ziara ile ya mwanzo kabisa anawaambia Wakuu wa Mikoa na Watendaji wengine na Mawaziri aliofuatana nao waelezeeni wananchi mambo mnayoyafanya. Sasa Waziri haiwezekani kila siku akenda katika vyombo vya habari. Lakini kwa kuwa Maofisa wa Habari watakuwa wanashirikishwa katika shughuli zote za mipango ya Wizara ninaamini Mhe. Spika, taarifa kila siku zitakuwa zinatoka na kama hii tulishauri katika Kamati, Mhe. Spika, tunayo *website* yetu ya

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Na kama Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye ndiye Kiongozi wa shughuli za serikali basi matukio yote ambayo hata sio ya Wizara yake yawe yanaingizwa katika *website* ya serikali ili hata wale wenzetu walioko nje wazanzibari na waliokuwa si wazanzibari waweze kuyaona yale matukio. Kwa hivyo naomba sana Mhe. Spika, hili tulilizungumzia kwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais lakini kimsingi katika maeneo yote kabisa.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni alilisisitiza hili na katika ripoti yetu vile vile liliweza kujitokeza. Lakini aliipongeza vile vile akaitolea mfano nchi ya Rwanda. Mhe. Spika, kwanza tunamshukuru ndugu yetu Salim Said Bakhressa kwa utaratibu aliouanzisha, kwamba kwa kuwa hapa tumetunga sheria za nchi tunazuia mifuko ya *plastic* lakini wenye vyombo wao wanaleta abiria akimuona mtu amepakia mzigo kupitia mifuko ya *plastic* anaweza kumbadilishia na kumpa mfuko ambao unaofuata mazingira. Mimi Kamati yangu tutawaandikia maalum ile Kampuni ya Azam Marine kwa kuwapa shukrani ili na wengine wapate kuwa na moyo na waweze kutufanyia kama vile.

Mhe. Mgeni alieleza nchi ya Rwanda, Rwanda ukifika *airport* kama umebeba begi ya *plastic* Mhe. Spika, unaambiwa begi lako weka hapa nunua mfuko ule pale, kama huna unaambiwa vitu vyako acha hapa hapa. Rwanda iko salama ni *plastic free* wenyewe wanaita kule. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaipongeza sana Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais lakini vile vile suala hili pia linahusu na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Baraza la Manispaa waweze kutusaidia katika mapambano haya dhidi ya mifuko ya *plastic*.

Mhe. Spika, Mhe. Mgeni alielezea tena kuhusu suala la bango la ufadhili wa Crystal katika kituo cha Paje lakini vile vile jeuri na kashfa na kibri alichofanyiwa na mlinzi wa Crystal Hotel. Mhe. Spika, kwa hili sina haja ya kulirejea tena kwa sababu nimeshalitolea maelezo.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Juma alitoa angalizo tuangalie zile sababu tulizoziandika kwa baadhi ya wananchi tuliandika katika maeneo mawili; wananchi wa Chwaka na wananchi wa Mtambwe ambao walisusia zoezi la sensa. Tulielezea mambo mengi wengine waliambiwa Shekhe kasema kwamba waislamu wameambiwa kidogo kwa hivyo wasikubali wasiende kwenye sensa.

Sasa Mhe. Spika, kama Shekhe kawambia waislamu kidogo kama hukwenda kujiandikisha sasa ndio tutazidi kuambiwa tuko kidogo. Sasa hapa ndio maana Mhe. tukasema kwamba elimu ya uraia ni kitu muhimu sana. Kwa sababu

ukiangalia Mhe. Spika, wananchi wa Chwaka walikuwa wakilalamika sana kuhusu suala la maji, lakini leo kama wameshindwa kujiandikisha katika sensa, wengi wamejiandikisha lakini hao baadhi yao kwa hivyo ina maana katika mipango ya serikali ina maana watashindwa kuingizwa katika ile idadi halisi katika eneo lao.

Lakini vile vile lilielezewa suala la vitambulisho vya Wazanzibari, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amelieleza vizuri kabisa vya kutosha. Lakini kitu kikubwa tulichokigundua Kamati yetu Mhe. Spika, bado elimu ya uraia wananchi wetu ni ndogo sana. Mtu jambo la haki yake mwenyewe atatoka mtu mjini anakwenda kumfahamisha yeye kijijini na anamfuata vile vile. Matokeo yake Mhe. Spika, kuna baadhi ya wananchi hawakupata hiyo nafasi lakini tunaishukuru Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais walifanya jitihada za ziada wakawafuata tena wale wakajaribu kuwashawishi wale wananchi katika zoezi lililorejewa wananchi wale wengi walikwenda kujiandikisha katika sensa.

Kwa hivyo naomba Mhe. Spika, Waheshimiwa Mawaziri katika lile eneo la sababu zilizowafanya wananchi wasiende kujiandikisha ziko nyingi pale tumezitaja kuhusu masuala wanasema wanatengwa katika masuala ya ajira tumeeleza mambo mengi kule kwa hivyo ninafikiri Waheshimiwa Mawaziri wakiangalia katika hii ripoti yetu ninafikiri inajielezea vizuri sana.

Lakini vile vile wengine wakasema mikopo ya JK na AK kwa hivyo mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, basi safari hii itakapotoka ile mifuko ya AK na JK atoe *priority* kwa haya maeneo mawili. Eneo la Chwaka na vile vile eneo la Mtambwe. Na ukishafika Mheshimiwa kama kawaida yako kwanza tusife sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hasa hii Kamati yangu iliyokwenda kuwaona wananchi, uwambie kwamba Mhe. Mwenyekiti na Kamati yake alitwambia nyinyi mligoma kwenda kuandikisha sensa kwa sababu hamkupata mkopo wa AK na JK sasa njooni hapa mje, tena wapige picha kama walivyopiga Bwawani pale. Na wale wengine waliokuja kuchukua pesa si zao ukapata kuwakamata. Tena Mheshimiwa ninakupongeza sana kwa utaratibu wako huo pesa unamwaga kama njugu huko mitaani, lakini bado wananchi wetu wanazihitaji nafikiri hilo naomba Mhe. Waziri ukilifanya wale wananchi wetu watajua ule umuhimu wa Kamati zinapokwenda yale maombi yao au maoni yao wanayafikisha serikalini.

Mhe. Spika, Mhe. Farida alipongeza Kamati yetu, pamoja na Mhe. Fatma Mwakilishi wa Jimbo la Amani wao nitawachanganya kwa pamoja kwa sababu mawazo yao nafikiri kama walikaa pamoja wakachangia kwa pamoja.

Mhe. Fatma na Mhe. Farida waliishauri Ofisi yako Mhe. Spika, kwamba wanasema wanaona unyonge wanasema zamani Mhe. Spika, katika lile Baraza letu la zamani lile la Kikwajuni wanasema tulikuwa tunafanya vikao na Pemba, lakini sasa hivi tokea kuja katika Baraza jipya hatufanyi tena vikao Pemba. Sasa hili nadhani Mhe. Spika, najua kwenye meza yako hapo huwezi ukajibu lakini hili naomba Ofisi yako iweze kulichukua na kulifanyia kazi. Wenzetu, ndugu zetu wa kule Pemba wameleta maombi yao kupitia kwa Waheshimiwa wawili Mhe. Farida na Mhe. Fatma na ninaamini Dr. Sira hajawahi kufanya kikao Pemba wananchi wakamuona, wanamuona tu kwenye Televisheni, kwa hivyo nafikiri wakimuona kule mambo yatazidi kuwa mazuri.

Mhe. Spika: Mheshimiwa zingatia muda na hilo tunalifanyia kazi pamoja na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kuhusu kufanya vikao Pemba kumbe Mhe. Spika, huwa anajibu pale pale wakati mwengine. Mhe. Spika, Mhe. Mwanamapinduzi Mhe. Saleh Nassor Juma yupo yeye alielezea sana kukerwa kwake na jinsi wananchi wanavyokata mikoko na maji yakawa sasa hivi yanavamia maeneo ya kilimo, na vile vile yakawa yanavamia maeneno ya makaazi. Mhe. Spika, hili ni kweli Kamati yangu ilitembelea Kisiwa Panza Mheshimiwa kuna makaburi ya masharifu ambao walizikwa kwenye miaka 40 iliyopita, Mhe. Spika, makaburi yale tuliyakuta baharini. Kwa hivyo sasa hivi Sharifu yuko baharini. Sasa Mhe. Spika, unajua tamaduni zetu hizi, wakati mwengine mambo yakishakuzonga unakwenda kwenu unapelekwa kaburini kwa babu yako uko baharini. Sasa umetoka Unguja unakwenda zako Kisiwa Panza maji yamejaa. Sasa Mhe. Spika, unakwenda kuwaombea dua nakusudia wazazi. Kwa hivyo hiyo inathibitisha nini kwamba Mhe. Spika, kidogo kidogo kwa jinsi tunavyoharibu mazingira kisiwa chetu kinavamiwa na kinaliwa na bahari.

Mhe. Spika, hivi sasa kuna baadhi ya misikiti ambayo kipindi kirefu imejengwa ilikuwa karibu kilomita moja kutoka kwenye bahari kuna misikiti imo ndani ya bahari sasa hivi ya zamani kabisa. Ukienda kwa wale watu wa makumbusho na mambo ya kale watakuelezea, Kamati yangu ishawahi kutembelea tukakuta kuna msikiti upo chini ya bahari. Sasa hii inaonesha kwamba Visiwa vyetu hivi kila tukilala tukiamka basi bahari inatutafuna.

Mhe. Spika, najitahidi kumalizia sasa naingia kwa upande wa Waheshimiwa Mawaziri. Mhe. Spika, mimi kwanza nataka niwapongeze Waheshimiwa wote Mawaziri kwa sababu hakuna hata mmoja aliyepinga maoni yetu na aliyekanusha maoni yetu. Wametupongeza sana na hii Mhe. Spika, kwa sababu hii kazi tuliifanya kwa pamoja, ziara tulikuwa tunakwenda kwa

pamoja kwa mambo mengi ambayo tuliyoyaona hii ripoti imekuwa kama ni ripoti ya Kamati na serikali, kwa sababu tulifanya kazi safari hii kwa karibu sana. Kwa hivyo nawashukuru sana kwa mashirikiano ambayo walitupa ingawa kidogo nitajaribu kuna baadhi ya maeneo hasa Mheshimiwa wangu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kutokana na muda wake ulikuwa mdogo hakuweza kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya mambo, kidogo nilikuwa nataka haya mengine aje ayafanyie kazi.

Mhe. Spika, suala la migogoro ya ardhi, Mhe. Waziri wan chi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hili najua alililenga katika kuja kulitolea ufafanuzi kwa sababu linawagusa wananchi wengi. Sasa Mhe, mimi nilikuwa nashauri au Kamati yangu inashauri hii migogoro ni kweli tunakubali Mhe. Rais wetu aliwaachia masheha na wakuu wa wilaya kule wayatatue. Lakini Mhe. Spika, hii migogoro iko kisheria zaidi tukiwaachia wakuu wa wilaya na masheha. Mheshimiwa hii migogoro haifiki mwisho na sisi tunataka ifike mahala Mhe. Spika, suala la migogoro ya ardhi tusilisikie yaani lifike pahala tupige mstari. Tunashukuru sana serikali yetu hivi karibuni wamefanya zoezi la usajili wa ardhi na Mhe. Rais tayari ameshalizindua zoezi lile.

Sasa mimi naomba kwa sababu ukimwangalia sheha, sheha nguvu yake kwa Mkurugenzi ni ndogo pengine aliyekosa ni Mkurugenzi au pengine aliyekosa ni Waziri sheha hapo mlangoni atafika, akishajua Waziri kafanya kosa sheha atafika kule, lakini Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa kupitia Waziri wake yeye ndiye *coordinator* wa mawizara yote wana uwezo wa kumuita Waziri yoyote au Katibu Mkuu, yoyote au Mkurugenzi yoyote au mtendaji yoyote kutatua matatizo. Kwa sababu tukiangalia Mhe. Spika, kuna matatizo mengine kuna *forgery* za *document* wakati mwengine hao masheha *document* iliyokuwa ime-fojiwa hawezi kuijua.

Mhe. Spika, mimi Kamati yangu kuna mgogoro mmoja wa hapa Fumba tukawaita wale waliokuja kulalamika na walalamikiwa, Mhe. Spika, ametuletea hati ya urithi haina kichwa wala miguu, hamna majina ya wale wenyewe, hamna majina alopakana nao ni *document* iko kati kati kitumbo tumbo hivi tulimuonea huruma tu lakini kama tungechukua kile kifungu cha Kinga na Fursa ya Wajumbe ile sheria yetu ya kulidanganya Baraza, maana unapoidanganya Kamati ukileta *document* feki ina maana umelidanganya Baraza. Mhe. Spika, ungesikia sasa hivi kuna mtu tunamburuza mahkamani.

Sasa *document* kama ile Sheha eti ndio anatuonesha sisi anasema unaona hii, tunamwambia wewe sheha *document* gani hii *document* feki. Sasa mambo kama haya kama Ofisi yenyewe ya Makamu wa Pili wa Rais naamini *document* feki yoyote wakiiona wataweza kuitambua. Kwa hivyo hatupingi maamuzi ya juu lakini tunaomba

kuna mambo mengi ya kisheria ambao masheha na wakuu wilaya wakati mwengine yanakuwa yako juu ya uwezo wao.

Kwa hivyo Mhe. Spika, lakini vile vile tulizungumzia suala la *job description*, Mhe. Spika, hili baada ya kulizungumza hapa katika Kamati juzi kuna malalamiko mengi aa maana yake Mhe. Hamza amesema hakuna muongozo wa kazi. Mhe. Spika, hili nimelizungumza kwa makusudi na hili haliko katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais peke yake liko katika Wizara nyingi.

Mhe. Spika, kuna wizara moja dereva yeye mpaka manunuzi anahusika dereva umeona wapi. Tukitoka hapa nitamwambia huyo Waziri anayehusika. Sasa hapa inaonesha kwamba hakuna muongozo wa kazi kwa sababu kama mtu kuna muongozo wa kazi katika kweli masuala ya manunuzi atakwenda kuhusika dereva. Sasa kuna mengine tumekwenda *government press* pale, ingawa *government press* kutokana na uhaba wa wataalamu, kuna *engineer* mmoja pala yeye kasomea mambo ya *electricity* inabidi anashughulika mpaka mambo ya *merchanic* ina maana *all around* anacheza lakini mshahara ndio ule ule posho ndio hiyo hiyo.

Sasa mimi nadhani Mhe. Spika, kama kutakuwa kuna muongozo wa kazi serikali itaweza kujua kwamba hapa pana mapungufu, kwa sababu Mheshimiwa ukiwepo muongozo wa kazi ina maana kama kuna eneo halina mtendaji ina maana serikali itapata kuziba lile pengo. Kwa hivyo mimi nadhani wale watendaji labda nimekusudia na Wizara fulani, takriban maeneo mengi mambo haya yanafanyika.

Mhe. Spika, nilizungumzia suala la Tume ya Uchaguzi Mhe. Spika, nadhani Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alikusudia kuja kulimalizia mwisho vile vile. Mhe. Spika, sasa hivi tuna tatizo moja sasa hivi tupo katika nusu ya kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Saba na ninashukuru serikali hii toka ilipoingia inahubiri amani na utulivu, lakini bado tuna tatizo katika uboreshaji wa daftari. Uboreshaji wa daftari bila ya kuwa na Tume ya Uchaguzi utaliboresha vipi, nani atatoa miongozo.
Sasa Mhe. Spika, hivi sasa kuna tatizo, najua mchakato umo mbioni lakini naamini kutokana na muda uliobakia na hata hili zoezi Mhe. Spika, la hii kura ya kuwachagua Wajumbe wa Mabaraza ya Katiba. Mimi nilitembelea vituo vingi kwa sababu nilikuwa najaribu kuangalia changamoto, changamoto nilizozigundua Mhe. Spika, kuna watu ambao wanadai wao ni wakaazi wa maeneo fulani lakini katika buku la Sheha hawamo. Kuna wengine keshahama zaidi ya miaka mitano keshafutwa anarudi anataka aingizwe. Sasa leo kuchagua Mabaraza ya Wilaya tumefikia hali ile je, keshokutwa tuna kura ya maoni muhimu sana ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano na naamini madaftari haya yatakuja kutumika.

Sasa hili naomba sana Mhe. Spika, pamoja na elimu ya uraia itakayotolewa mwananchi kama haki yake ya msingi hajaipata hata hiyo elimu ya uraia sijui kama atakuja kuisikiliza. Mhe. Spika, naomba sasa hivi hili zoezi liweze kufanyika.

Mhe. Spika, naishukuru serikali kwamba fedha za kufanyia kazi hiyo tayari zipo Tume ya Uchaguzi wametuthibitishia fedha zipo kwa hivyo nadhani wakati wowote hiyo kazi wanaweza wakaanza kuifanya baada ya kupata miongozo.

Mhe. Spika, kuna eneo la Skuli ya Kisiwandui, hili naomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tunaomba sana Skuli ya Kisiwandui inasomeshwa wanafunzi wenye matatizo ya akili tena watoto wadogo, wengine akili zao ni taahira, wengine viziwi, wengine hawaoni. Mhe. Spika, skuli ile zikija mvua kubwa za masika skuli ile inakuwa iko ndani ya bahari, ninaposema iko ndani ya bahari inajaa maji. Tulioneshwa sisi watoto wadogo ambao wanakwenda pale kusomeshwa Mwenyezi Mungu apishie mbali, akija akiteleza akitumbukia katika maji yanayotuama ndani ya skuli ile Mhe. Spika, tutakuja kuzika. Sasa mimi naomba na suala lile nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri wawili wangelifanya ziara maalum katika skuli ile ya Kisiwandui wakaangalia mazingira ya wale watoto, elimu wanapata nzuri wanaletewa masomo kutoka Uingereza wanasoma pale, kuna masomo ya mtandao lakini wale wanafunzi wanasoma katika mazingira magumu.

Sasa Mhe. Spika, tunaomba skuli ikatiwe kifusi iwekwe *level* ya juu lakini vile vile pale pana mtaro wa kuweza kuondoa yale maji. Kwa hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Mawaziri suala hili Mwalimu Mkuu wa skuli ile aliwahi kulileta Ofisi ya Waziri Kiongozi kipindi kile alipokuwepo Mhe. Shamsi Vuai Nahodha lilikaa katika ofisi na sisi juzi tukalikumbusha lakini bado lile tatizo ni tete naomba sana Waheshimiwa Mawaziri wetu walisimamia hili.
Mhe. Spika: Dakika tano zimekwisha Mheshimiwa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Basi Mhe. Spika, haya maeneo mengine basi nitaomba niwapelekee kwa maandishi, isipokuwa naomba kuwashukuru sana mawaziri wangu kwa kuwa ndio tunamaliza muda wa kamati, tuombeane kila la kheri Mhe. Spika, na waniombee dua nirudishwe katika kamati hii hii ili tuweze kumaliza kiporo tulichokiacha. Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sasa tuone kama taarifa ya Ripoti ya Utekelezaji na Taarifa ya Ripoti hii ya Kamati kama vimepolekewa. Niwahoji basi wale wanaopokea Taarifa ya Utekelezaji wa Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2011/2012 na Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu ya mwaka 2012/2013 wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ripoti zote mbili zimepokelewa ya Utekelezaji na Ripoti mpya. Tunaendelea.

TAARIFA ZA SERIKALI

Ripoti ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Mwaka 2011/2012

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha taarifa kuhusu maagizo ya Baraza la Wawakilishi kupitia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, katika Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwenye ripoti hiyo ya mwaka 2011/2012 tulipewa maagizo matano. Maagizo hayo ni kama ifuatavyo:-

Agizo la kwanza lilikuwa agizo kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti; agizo lenyewe lilihusiana na kurahisishwa kwa taratibu za kuanzishwa kwa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

Utekelezaji

Katika utekelezaji wa suala hili muongozo wa utayarishwaji wa Bima ya Afya ulitayarishwa, utafiti wa utayari wa wadau juu ya uchangiaji na huduma zitakazotolewa na Mfuko ulifanywa Unguja na Pemba na matokeo ya awali inaonesha wadau wengi kukubaliana na azma hiyo.

Aidha, mwelekeo na tathmini ya awali ya uchangiaji wa gharama za Bima ya Afya ulifanywa chini ya usimamizi wa mtaalamu kutoka WHO na kikundi kazi cha wataalamu wanaosimamia uanzishwaji wa Bima ya Afya Zanzibar ambao wanatoka sekta mbali mbali, sekta zenyewe ni kama zifuatazo:-

Wizara ya Afya; Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo; Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Shirika la Bima; Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ripoti kamili ya utafiti ina kazi ya tathmini ya awali ya uchangiaji wa Bima ya Afya imekamilika na tayari imewasilishwa kwa wataalamu wa WHO na DANIDA ili kupata maoni yao. Baada ya kukamilika ripoti hii hatua inayofuata ni kufanya tathmini ya kina itakayaochambua mfumo mzima wa usimamizi na uendeshaji wa Bima ya Afya Zanzibar.

Agizo la pili Mhe. Spika, lilielekezwa kwenye Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Agizo lenyewe lilikuwa kuzidisha mawasiliano na wizara nyengine za SMZ ili kutoa taarifa za mabadiliko na mageuzi ya utumishi ili kupunguza migongano na kuleta uwiano katika utumishi wa umma.

Utekelezaji

Miongozo mbali mbali ya kuelimisha wananchi na watumishi wa umma imetolewa kupitia vipeperushi, vyombo vya habari, semina, maigizo kwa lengo la kupunguza migongano na kuleta uwiano katika utumishi wa umma.

Agizo la tatu lilipelekwa Idara ya Utawala Bora, nalo lilihusiana na suala la kupatia ufumbuzi migogoro ya ardhi baina ya wananchi, viongozi na watendaji wa serikali.

Utekelezaji:

Moja katika majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kupokea malalamiko mbali mbali kutoka kwa wananchi na watumishi wa serikali. migogoro ya ardhi ni miongoni mwa malalamiko ambayo yamewahi kupokelewa katika wizara yetu. Kwa kawaida wizara inapokea lalamiko ambalo hutaka lipatiwe ufumbuzi juu ya lalamiko husika katika taasisi yoyote ambayo inalalamikiwa. Wizara hulipitia na kulitafakari ili kujiridhisha juu ya ukweli wa lalamiko husika na baadae hutoa maelekezo au ushauri kwa taasisi na kuiomba ichukue hatua zinazofaa ili kulipatia ufumbuzi.

Pili kulifuatilia suala la rushwa Mahkamani ili kuwajibishwa watakaogundulika kuhusika na kadhia hii. Utekelezaji, wizara kupitia mamlaka ya kuzuwia rushwa na uhujumu uchumi moja kati ya jukumu lake kubwa la msingi ni kuzuwia rushwa na kupendekeza serikali uwepo wa mianya inayopelekea kuwepo kwa rushwa na pia kuona kwamba wale wote

wanaotuhumiwa na kutiwa hatiani wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. Mamlaka kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka itahakikisha kwamba masuala ya rushwa yatafuatiliwa na kuwajibishwa kwa watakaogundulika na kadhia hiyo pamoja na kujuilishwa wananchi kupitia ripoti ya kila mwaka baada ya Mamlaka ya Rushwa kuanza kazi rasmi.

Agizo la nne lilikuwa ni Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Agizo hilo lilikuwa ni kutafuta eneo la kujenga jingo jipya la Ofisi ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Utekelezaji

Serikali bado inaendelea kulifanyia kazi suala hili, kwani kiwanja cha kujenga majengo ya kuhifadhia nyaraka kinahitaji kuwa katika maeneo yenye mazingira maalum yenye upungufu wa unyevu, yasiotuama maji na hayana uwezekano wa kiupata mafuriko. Yanafikika kirahisi au yako karibu na mji ili kurahisisha utoaji wa huduma.

Baada ya kuzingatia mambo hayo, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeshaomba wizara inayosimamia masuala ya ardhi kuangalia mipaka ya awali pia kuangalia uwezekano wa kulinunua eneo la jirani ya jengo la nyaraka la sasa ili tuweze kutumia eneo hilo ambalo limeonesha kufaa sana kwa majengo ya nyaraka na hakuna matatizo ya kiufundi toka kujengwa kwake.

Katika Idara hii pia kulikuwa na agizo linalohusiana na malipo yote ya tafiti yafanywe katika Idara ya Nyaraka. Mhe. Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inapitia upya mfumo mzima wa vibali vya utafiti pamoja na malipo yake. Kama tunavyofahamu Mhe. Spika, suala la utoaji wa vibali vya tafiti uko chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na fedha hizo zikipatikana zinaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina, sasa mpaka pale serikali itakapofanya maamuzi mengine juu ya utaratibu hapo tunaweza tukazingatia. Sasa masuala ya malipo haya yanaweza yakafanywa chini ya Idara hiiya Nyaraka kwa mujibu wa serikali itakavyoamua.

Katika idara hiyo kulikuwa na agizo la tatu ambalo linahusiana na kurahisisha kwa zoezi la kuzihamisha nyaraka katika mfumo wa analogi kwenda katika mfumo wa *digital*, ili ziweze kudumu kwa muda mrefu na pia kununuliwa kwa kifaa maalum cha kudhibiti unyevu wakati kinapowashwa kipoza hewa.

Idara kwa kushirikiana na Idara ya Mipango, sera na Utafiti iliandaa mradi unaoitwa *Digitalization of Zanzibar Archive.* Lengo kuu la mradi huo ni kuzihamisha nyaraka katika mfumo wa sasa na kuzipeleka katika mfumo wa

digital. Kwa sasa mapendekezo ya mradi huo yamewasilishwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa ajili ya utafutaji wa rasilimali fedha.

Agizo la tatu (b) kifaa cha kuhifadhia unyevu ambacho hutumika katika kudhibiti unyevu kimo katika utekelezaji wa ununuzi wa vifaa na mashine katika mpango kazi wa Idara kwa mwaka 2012/2013.

Agizo la Tano ambalo ni la mwisho lilikuwa limeelekezwa kwenye Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Agizo hili lilikuwa linahusiana na suala la Kamisheni iajiri watu wenye sifa zaidi na itoe elimu ya sheria ya utumishi wa umma kwa Makamishna ili kuboresha utendaji wao.

Utekelezaji

Elimu ya sheria ya utumishi wa umma inaendelea kutolewa, kwa upande wa upatikanaji wa watumishi wenye sifa kwa kamisheni limeshawasilishwa ombi hili wizarani na shauri linafanyiwa kazi na jumla ya watumishi 15 wameshahamishwa kutoka katika taasisi mbali mbali kwenda Kamisheni ya Utumishi wa Umma wengi wao wakiwa ni wataalamu. Na taratibu za kuajiri watumishi wengine 15 zinaendelea.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kuwasilishwa ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na Baraza lako tukufu naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako taarifa hii ya utekelezaji wa maagizo yanayotokana na Ripoti ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inayo jukumu kubwa la kuratibu shughuli za sekta ya sheria na kusimamia utoaji haki, kutoa huduma za usajili wa makampuni, mali, matukio ya kijamii na hatimiliki; kusimamia mali za wakfu na mali ya amana na kuratibu masuala ya Dini ya Kiislamu. Majukumu hayo yanatekelezwa na taasisi za wizara 12 ikiwemo Mahkama, Ofrisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Tume ya Kurekebisha Sheria, Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo, Ofisi ya Mufti, Ofisi ya Msajili wa Hakimiliki, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Utumishi na Uendeshaji na Ofisi Kuu Pemba.

Mhe. Spika, taarifa hii inazungumzia utekelezaji wa maagizo mbali mbali yaliyotolewa na Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza lako tukufu kwa wizara yangu kwa kipindi cha mwaka 2011/2012. Aidha,

maelezo ya utekelezaji yanayotolewa katika taarifa hii yanahusu kipindi cha mwaka wa bajeti hadi mwezi Machi, 2013.

Mhe. Spika, Ripoti ya Kamati za Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya mwaka 2011/2012 imeonesha kuwa jumla ya maagizo 13 yanayohusu Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi na idara za wizara hiyo zilizoguswa moja kwa moja na maagizo hayo ni kama ifuatavyo:

Mahkama, Tume ya Kurekebisha Sheria, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Idara ya Utumishi na Utendaji. Utekelezaji wa maagizo hayo unaoneshwa katika Bango Kitita yaani *matrix* iliyoambatanishwa.

Mhe. Spika, maagizo haya 13 yamegawika kama inavyofuata:

Katika maagizo 13 mawili yametekelezwa kwa asilimia mia moja, saba utekelezaji wake ni baina ya asilimia 50 au 80 kwa mia na hizi shughuli bado zinaendelea, haya ni maagizo nambari 2, 6, 7, 8, 9, 11 na 12 kama inavyooneshwa; na maagizo manne utekelezaji wake ni chini ya asilimia 50. Hayo ni maagizo nambari 3, 4, 5 na 13. Maagizo haya tatizo kubwa ni uhaba wa fedha.

Mhe. Spika, ukitizama katika bango kitita kwanza kuna kuongezwa kwa idadi ya Mahakimju Pemba. Hii kama inavyoonesha tumeshatekeleza asilimia mia moja, pili ni Mahkama kuondoa kwenye vituo wale Mahakimu waliotumika kwa muda mrefu. Hili Mhe. Spika, tumeshalitekeleza kwa kiwango kikubwa nab ado tunaendelea. Tatu kwamba ni makarani wanaosaidia Mahakimu wapewe *survey*. Hii kama nilivyosema kutokana na uhaba wa fedha hatujalitekeleza kwa kiwango kikubwa, lakini tutaendelea kulitekeleza mara au kila pale ambapo tunapata fedha.

Nne ni kwamba serikali iingize fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahkama ya Wilaya ya Mkoani ili kuondosha tatizo la ufinyu wa ofisi. Kama nilivyosema hili nalo Mhe. Spika, kutokana na uhaba wa fedha bado hatujalitekeleza ipasavyo. Tano, ni serikali ijenge Tume ya Kurekebisha Sheria jengo lake. Hili Mhe. Spika, bado kwa sababu fedha hatuna na tunaendelea kutafuta kiwanja na bado tunatizama uwezekano kuweza Tume ya Kurekebisha Sheria kama tui *accommodate* katika jengo lile la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu jipya, au tuliweke katika jengo la Wizara ya Katiba na Sheria jipya litalomaliza. Kwa hivyo, haya Mhe. Spika bado tunayatafakari na pemngine baadae tunaweza tukapata uamuzi mzuri.

La sita, ni kwamba watafiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria hawana taaluma ya utafiti, tume iwapatie elimu ya utafiti. Mhe. Spika, wengi kati yao karibu asilimia 89 wameshapata elimu hiyo na tunaendelea kuwapa wengine.

Halafu kuna Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana iendelee kufuatilia mali za wakfu ili kuepusha dhima mbele ya Mwenyezi Mungu. Hili tumelifuatilia kwa kiasi kikubwa asilimia 70 nafikiri tumekamilisha, lakini bado tunaendelea.

Agizo jengine la nane ni kwamba mashamba yote ya Wakfu yajulikane mipaka yake kwa lengo la kuepusha kuvamiwa mashamba hayo. Mhe. Spika, asilimia karibu 60 tumefanya, juhudi zimechukuliwa kutambuliwa mashamba hayo, baaghi yamepimwa na mengine taratibu za kuyapima zinaendelea, ingawa zoezi hili ni gumu kutokana na ukosefu wa taarifa za mashamba hayo. Lakini bado tunaendelea na mfano kama shamba la Bagamoyo ambalo ni kubwa sana lote tayari limekamilika.

Mhe. Spika, agizo la tisa ilikuwa kwa vile kuna ugumu wa utekelezaji wa sheria ya Wakfu Nam. 2 ya mwaka 2007 na kuna migongano na sheria nyengine, basi kamati imeagiza sheria zote zinazopingana na Sheria ya Wakfu zifanyiwe marekebisho. Mhe. Spika, agizo hili tumeshalitekeleza kwa kiwango kikubwa, sheria hii tumeshaipitia, tumeshajuwa wapi mapungufu yapo, sasa tunaendelea na sheria nyengine na baadae tutaziweka pamoja na tutajua turekebishe namna gani.

Mhe. Spika, agizo la kumi ni kuzipatia fedha kwa wakati na kulingana na mahitaji ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Agizo hili Mhe. Spika, tumeshalitekeleza kwa asilimia mia moja.

Agizo la 11 uhaba wa watendaji kwa baadhi ya taasisi, serikali itoe nafasi za ajira kwa kuwa baadhi ya watendaji hutoa huduma kwa zaidi ya kituo kimoja jambo ambalo hudhorotesha utendaji. Mhe. Spika, agizo hili tumeshalitekeleza kwa asilimia 70, tumepata nafasi 35 za Mahkama hizi zote tumeshazitangaza tutazijaza. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imepewa nafasi nane na hizi ni ziada ya zile nafasi 25 ambazo tumepewa. Kwa hivyo, kwa nafasi hii ambazo kidogo tulikuwa na mapengo naamini tukishakuzijana hizi kwa kweli tutakuwa nafasi tumezijaza kikamilifu. Hatua iliyobakia hivi sasa tunawasiliana na Tume ya Utumishi ili waweze kuwa *interviewed* hawa na kuwaajiri.

Agizo la 12 ni kutokana na uhaba wa fedha zinazopatia taasisi za serikali na kwa kuwa watumisi wengi wa umma wana muamko wa kusoma, kamati

imeagizo serikali kuanzisha mfumo wa *cost sharing* ili watumishi wenye hamu ya kusoma kupatiwa nafasi hizo.

Mhe. Spika, agizo hili takriban asilimia 50 tumelitekeleza kwa sababu wizara imeweza kuandaa mahitaji ya mafunzo kwa mwaka mmoja kwa kila idara na taasisi zake, lakini ule mpango wa miaka mitano wa rasilimali watu utatekelezwa mwaka ujao baada ya kupata muongozo yaani *Human Resource Planning Guideline* kutoka Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Agizo la mwisho Mhe. Spika, la 13 ni kiwamba wizara izipatie taasisi zake vyombo vya usafiri ili viweze kutekeleza majukumu yao bila ya usumbufu wowote.

Mhe. Spika, hili kama nilivyosema kutokana na uhaba wa fedha hatujalitekeleza sana na utekelezaji wake ni kiasi asilimia 30. Mhe. Spika, tutapopata fedha katika bajeti inayokuja tukijaaliwa basi tutajitahidi kujaza haya mapengo ambayo baadhi ya idara au taasisi hazina usafiri. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa hai na wazima naomba nichukue nafasi hii kutanguliza shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika hali hii ili niwasilishe Muhtasari wa Ripoti ya Utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013 kwa Wizara mbili ambazo zinasimamiwa na kamati yetu kwa mujibuwa Kanuni ya 106 fasili ya 14 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar Toleo la 2012.

Mhe. Spika, pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii adhimu na adimu kuweza kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali kama ambavyo imeelezwa hapo kabla.

Mhe. Spika, nitakachokiwasilisha hapa kwa niaba ya kamati mi muhtasari lakini ripoti hasa kamili inapatikana katika kitabu ambacho kimetolewa na sekreterieti ya Baraza na Ripoti ya Kamati ya Katiba Sheria na Utawala inapatikana kuanzia ukurasa wa 33 hadi 61 ambapo kuanzia ukurasa wa 33 hadi 34 kuna utangulizi, ukurasa wa 34 hadi 46 kuna ripoti inayohusu Wizara ya Nchi Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na ukurasa wa 46 hadi 59 kuna ripoti inayohusu Wizara ya Katiba na Sheria. Na mwisho kabisa ukurasa wa 60 hadi 61 kuna hitimishi.

Mhe. Spika, napenda niwashukuru mawaziri wote wa Wizara mbili ambazo tunazisimamia chini ya Kamati yetu pamoja na watendaji wao wote kwa namna moja au nyengine ambao wameshirikiana na kamati hii kuiwezesha kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yake ya ufuatiliaji kama ambavyo imeelezwa katika kanuni ya 113 ya kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Spika, nitakuwa sitendi haki kama sikuwapongeza wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria na Utawala wa Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano wao mkubwa waliouonesha wakati wote ambao kamati ilifanya kazi za ufatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuihoji serikali na kutoa maoni yao kwa lengo la kuimarisha utendaji na kukuza uwajibikaji serikalini.

Mhe. Spika, naomba wajumbe hao kuwataja kama ifuatavyo:-

Mhe. Ali Abdalla Ali	Mwenyekiti
Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
Mhe. Mohammed Raza Hassanali Dharamsi	Mjumbe
Mhe. Mussa Ali Hassan	Mjumbe
Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
Ndg. Latifa Saleh Suleiman	Katibu
Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi	Katibu

Mhe. Spika, kamati ya Katiba Sheria na Utawala imepewa mamlaka ya kusimamia Wizara mbili za serikali pamoja na Idara na Taasisi zilizomo katika Wizara hizo. Wizara hizo ni Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kiujumla kamati yetu imeridhishwa na utendaji wa wizara hizi mbili, bila ya shaka zipo kasoro ndogo ndogo za kiutendaji kwa baadhi ya taasisi zilizomo katika wizara hizi ambazo juhudi zaidi zinapaswa kuchukuliwa na taasisi hizo ili kukuza ufanisi kiutendaji kwa nia ya kuziletea mafanikio taasisi hizo na pia kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Nianze basi Mhe. Spika, na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, wizara hii imefanikiwa kutekeleza majukumu yake mbali mbali kupitia Idara zake zilizomo ndani ya wizara. Miongoni mwa majukumu hayo ni kama ifuatavyo:

Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Spika, kamati yetu imeridhishwa na utekelezaji wa Idara ya Mipango Sera na Utafiti hususan uimarishaji wa matumizi ya mfumo wa taarifa za teknologia ya mawasiliano yaaani ICT. Hata hivyo kamati inaishauri Wizara kuzishauri ofisi zote za serikali zikamilishe matayarisho ya matumizi ya teklonogia ya habari na mawasiliano kupitia mkonge wa taifa ili na sisi tuweze kwenda na wakati na pia kuzidisha ufanisi katika kazi zetu.
Lakini kwa upande mwengine pamoja na ahadi za kuwepo kwa mkonga wa taifa, Mhe. Spika, hadi sasa huduma za mtandano katika Zanzibar ni za kiwango cha chini na kasi yake kwa maana ya *speed* hairidhishi. Mhe. Spika, katika hali hiyo *e-government* inaonekana itabakia katika makaratasi tu zisipochukuliwa hatua za kurekebisha haya.

Mhe. Spika, kupitia ripoti hii kamati pia inataka kujua mchanganuo wa pesa zilizotumika katika kukamilisha mradi wa e-*government* kwani zile ni fedha zinazotokana na kodi za wananchi hivyo kuna ulazima zikawekwa bayana ili kila mwananchi ajue ni kiasi gani mchango wake umehusika katika mafanikio ya serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar katika suala hili.

Mhe. Spika, kamati imekuwa ikidai mchanganuo huu kwa takriban mwaka mzima sasa na hata wajumbe ndani ya Baraza walidai mchanganua huo lakini serikali inaonekana kulipiga chenga suala hili, inafanya hivyo kwa maslahi ya nani kamati haijui Mhe. Spika. Labda kwa taarifa tu Mhe. Spika, tumekuwa tukielekezwa katika wizara tofauti kupata taarifa hizi baina ya wizara hizi mbili, Ofisi iliyokuwa imesimamia kazi hii na Wizara ya Fedha, lakini kote huko pamoja na kamati kuiandikia tumeshindwa kupewa mchanganuo wa matumizi ya mradi huu.

Idara ya Utawala Bora

Mhe. Spika, Mhe. Spika, katika ufatiliaji wa kazi zake katika Idara hii kamati ilielezwa kuwa wataalam wa kufanya kazi ya kuangalia juhudi za kuzuia rushwa wameajiriwa. Na rasimu ya awali ya kanuni imewasilishwa wizarani na imeanza kupelekwa kwa wadau kwa ajili ya kutoa maoni yao. Kamati kwa kupitia ripoti hii inaishauri serikali kuharakiza mchakato wa kuiwezesha taasisi hii kuanza kazi mapema iwezekanavyo, ikiwa ni pamoja na kuharakizwa kwa rasimu hiyo.

Kamati pia inaishauri serikali kuzidisha umakini katika jambo la rushwa na uhujumu uchumi kwani nchi yetu inakosa maendeleo na kila siku wananchi wazidi kuwa hali ngumu kutokana na adui huyu mkubwa wa rushwa.

Mhe. Spika, isiwe tunazungumzia kupitishwa kwa sheria ambayo bado haifanyi kazi na matunda yake hayaonekani kwa wananchi kama ilivyodhihirika kupitia kwenye ripoti za kamati teule mbali mbali za Baraza la Wawakishi.

Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu ya Taifa

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali na wizara husika kwa ujumla itafute eneo kwa lengo la kujenga jengo jipya la nyaraka hasa ukizingatia kwamba jengo liliopo sasa ni dogo na pia limezungumwa na majengo ya wananchi. Pia wizara ifanye juhudi ya kuitafutia Idara ya Nyaraka Pemba jengo la ofisi.

Chuo cha Utawala wa Umma

Mhe. Spika, inakipongeza Chuo cha Utawala wa Umma kwa hatua yake iliyofikia ya ujenzi, kwani hivi sasa imeweza kulikabili tatizo la kuhamahama kila siku na kupelekea wanafunzi kusoma hadi nyakati za usiku, kitendo ambacho si kizuri hasa kwa hadhi ya chuo hiki.

Mhe. Spika, kamati inaona fahari kwa kuingilia kati suala hili kumeleta tija na mafanikio na hatimaye kukwamua ujenzi wa chuo hicho ambao hapo awali ulikuwa umekwama. Hata hivyo kamati imesikitishwa kuona kwamba serikali haijajiwekea utaratibu maalum wa kuziwekea ulinzi taasisi zake. Kamati pia inaishauri serikali kupitia Ofisi ya Idara Maalum kuweka utaratibu wa ulinzi kwa ofisi zote za serikali na sio ulinzi wa kutumia vurugu bali ni ulinzi wa kutumia silaha ili wahalifu wasiweze kufanya uhalifu wao katika vyombo vya serikali.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali:

Mhe. Spika, Ofisi ya Mdhibitina Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekabiliwa na changemoto nyingi ikiwemo ni pamoja kutofuatwa kwa sheria za fedha na kanuni za ununuzi na sheria nyengine kwa vyombo vya serikali, uchelewaji wa kutochukuliwa hatua mambo ambayo yamebainika katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, uelewa mdogo wa wadau kuhusu ripoti za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na kutokuwepo mashirikiano mazuri baina ya ofisi hii na Wizara ya Nchi Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kusababisha kupungua kwa ufanisi katika ofisi mbili hizi.

Mhe. Spika, haya yote yamebainika baada ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kutembelea ofisi hizo. Hivyo kamati inaishauri serikali kuvichukulia hatua za kinidhamu wizara, mashirika pamoja na taasisi zisizowasilisha

hesabu zao za mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwani mara kwa mara ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikieleza kuwepo kwa tatizo hilo ambapo kinyume na kifungu Nam. 24 cha sheria ya fedha. Serikali inaendelea kukaa kimya bila ya kutoa maamuzi jambo ambalo halifurahishi Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kuona hilo kamati kwa kutumia uwezo uliokuwa nao, inaishauri Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kujenga mashirikiano mazuri na karibu na Ofisi ya Rais na Utawala Bora kwani kufanya hivyo kutazidisha ufanisi wa kazi na kudhihirisha ile dhana nzima ya utawala bora.

Mhe. Spika, kamati pia inasisitiza tena agizo lake la kutaka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuimarisha utendaji na kufanya ukaguzi yakinifu na wa kina. Haipendezi kuona kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali ya Baraza la Wawakilishi inagundua matumizi mabaya mengi ambayo hayaonekani katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Tunalisema hilo Mhe. Spika, kwa sababu inategemea Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndio wenye wataalamu zaidi wa kufanya kazi hii kuliko kamati ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, nije katika Ofisi Kuu Pemba. Miongoni mwa malengo yaliyotekelezwa na ofisi hii ni pamoja na kuandaa mpango kazi wa wizara (Medium Term Expenditure Framework), kuandaa ripoti ya utekelezaji ya robo mwaka, kuzipitia na kuzifanyia ukaguzi uwekaji wa kumbukumbu katika wizara na taasisi za serikali, kufanya ukaguzi wa awali katika mikoa na wilaya za Pemba, kukagua vyumba vya uhifadhi wa kumbukumbu toli na hai na kuratibu mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu kwa watumishi wa umma.

Hata hivyo Ofisi Kuu Pemba ina changamoto ya uingizwaji mdogo wa fedha za matumizi mengine (*other charges*), ukosefu wa usafiri na ufinyu wa ofisi.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaishauri serikali iwe na tabia ya kuingiza fedha kwa wakati na kwa uwiano kati ya Makao Makuu ya Wizara kwa Unguja na Ofisi Kuu ziliopo Pemba ili kuzidisha ufanisi wa kila siku kwa taasisi zake kwenye visiwa vyote viwili vinavyounda Zanzibar.

Mhe. Spika, sasa nije katika Wizara ya Katiba na Sheria. Wizara hii kupitia taasisi zake mbali mbali katika kipindi hicho imetekeleza mambo yafuatayo na yafuatavyo ndio maoni ya kamati.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
Mhe. Spika, kamati yetu imeelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti pamoja na mambo mengine idara imeratibu miradi mbali mbali ya wizara katika hatua mbalimbali ikiwemo mradi wa ujenzi wa jengo la wizara, mradi wa kuzifanyia marekebisho sheria za usajili na kadhalika.

Pia idara imeandaa ripoti ya robo mwaka na taarifa za miradi ya wizara na kuziwasilisha Ofisi ya Rais Fedhe, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar.

Mahakama:
Mhe. Spika, miongoni mwa malengo ambayo yametekelezwa na Mahakama ni vikao vya kuharakisha mwenendo wa kesi ambavyo vimefanyika Unguja na Pemba. Imekamilisha kwa kiasi kikubwa matengenezo ya jengo la Mahakama Kuu Vuga, imefanya malipo kwa assessors mbali mbali wanaohudhuria katika kesi mbali mbali kuanzia pale walipokuwa hawajalipwa mpaka mahudhurio ya mwisho na pia inaendelea na matengenezo ya jengo la Mahakama ya Kadhi Mwanakwereke ambapo imefikia katika hali nzuri ya kuongezwa kuta urefu. Hata hivyo samani za ofisi, rangi na vitendea kazi bado hazitiwa.

Mhe. Spika, kamati imeona changamoto nyingi wakati ilipokuwa ikifanya ziara zake katika Mahakam mbali mbali Unguja na Pemba. Kama vile ufinyu wa bajeti jambo ambalo linalopelekea wafanyakazi kupata nafasi ya kwenda kusoma ili kuongeza ufanisi, upungufu wa wafanyakazi hasa makarani wa Mahakama na wachapaji kwa upande wa Pemba na ukosefu wa nyumba maalum za kuishi Mahakimu na Makadhi kwa upande wa Pemba hasa ukizingatia kwamba Mahakama zipo maeneo ya mbali.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kwamba Mahakama ya Makunduchi ifanyiwe matengenezo ya haraka na pia inaishauri wizara ilihamisha suala la kesi za ubakaji katika Mahakama ya Watoto ili haki iweze kupatikana kwa urahisi zaidi na pia kwa haraka, na hali hiyo pia itazidisha uhuru wa mtoto katika kesi hasa ukizingatia kwa mazingira ya Mahakama hiyo imeangaliwa kuwaweka watoto kuwa huru na kuwatoa hofu katika kutoa ushahidi wao na maelezo yanayohusu kesi zao.

Kamati pia inaishauri serikali kupitia wizara husika kulifuatilia suala la kununuliwa kwa kifaa cha DNA ili kuweza kurahisisha mwenendo wa kesi hasa za kubaka.

Mhe. Spika, inasikitisha kwa miaka sasa tunazungumzia ununuzi wa kifaa cha DNA lakini hadi leo serikali imeshindwa kutimiza ahadi ya kununua kifaa hicho.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu:

Mhe. Spika, miongoni mwa mambo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kuyatekeleza ni pamoja kuzikusanya sheria za Zanzibar kuanzia 1959 hadi 1964 na kuziweka pamoja ili kurahisisha upatikanaji wa kumbukumbu hizo. Pia mswada wa sheria wa kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu umekamilika na kujadiliwa na kupitishwa na Baraza lako tukufu.

Kamati inaipongeza wizara kwa hatua hii ya kihistoria ya kuleta Barazani mswada wa Sheria ya Kuanzishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar. Hata hivyo changamoto inayoikabili ofisi hii ni kushindwa kufikia lengo la kuhamia katika ofisi mpya ambayo ilipangwa iwe Disemba, 2012. Lakini kutokana na ucheleweshaji wa uingizwaji wa fedha hilo limeshindikana.

Mhe. Spika, kamati inaishauri serikali kujitahidi kuingiza fedha kwa wakati ili kuweza kurahisisha utekelezaji wa miradi mbali mbali ambayo wizara imepanga kuitekeleza.

Mhe. Spika, kazi kubwa ya utendaji kazi wa Mwanasheria Mkuu inapaswa kupewa msukumo kwa kutoa fedha ili jengo lao likamilike na kuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa.

Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka:

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendelea na majukumu yake kwa kuweka mitambo ya simu kwa ofisi ya Pemba, ununuzi wa mashine ya fax, kompyuta na samani za ofisi zikiwemo na vifaa vya kuandikia vya ofisi.

Mhe. Spika, ofisi pia imefanya mikutano mbali mbali baina ya Waendesha Mashtaka na Wapelelezi ili kuleta ufanisi katika kazi. Mikutano ambayo imewezesha ofisi kubaini changamoto mbali mbali zinazoikabili ofisi kwenye utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku. Hivyo kupitia ripoti hii kamati inaishauri serikali kuharakishwa kwa upelelezi ili kuondoa tatizo la

kuchelewa kusikilizwa kwa kesi na kusababisha wananchi kukosa imani na utaratibu mzima wa Mahakama.

Mhe. Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imefanikiwa kuendesha kwa utaalamu wa hali ya juu kituo cha mafunzo ya sheria ambacho imekianzisha ambapo mafunzo mbali mbali yametolewa kwa wanasheria wa serikali na hata wa taasisi binafsi wanaopata mafunzo chuoni hapo.

Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali

Mhe. Spika, katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali kamati ilielezwa changamoto nyingi zinazoikabili ofisi hiyo ikiwemo ukosefu wa usafiri kwa ofisi ya Pemba, jambo linalokwamisha utendaji wa kazi. Mhe. Spika, kwa ofisi kuu iliopo Unguja nafasi ya jengo ni finyu ambapo taasisi tatu zipo pamoja, ikiwe ni Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo, Ofisi wa Mrajis Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Makamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, zaidi jengo lenyewe ni hatarishi kwa wafanyakazi na kwa nyaraka zilizomo kwa sababu ni bovu na livuja sana.

Ofisi inapata changamoto ya kupangiwa kiwango kikubwa cha makusanyo Mhe. Spika, kutoka Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo jambo linalopelekea Ofisi hii ya Mrajis Mkuu wa Serikali kupandisha bei za usajili ili kufikia makusanyo hayo. Hali inayopelekea kurudidisha nyuma jitihada za watu kusajili hasa ukizingatia uwezo mdogo wa vipato vya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kutokana na changamoto hizo, kamati inaishauri serikali iwapatia Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali huko Pemba usafiri ili kuzidisha utendaji kazi wa ofisi. Pia kamati inaiomba serikali kuharakisha mradi wa ujenzi wa Wizara ya Katiba na Sheria ambapo jengo lake pia litajumuisha Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali ili kutatua kero zilizokuwepo hivi sasa na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na pia kupunguza kazi zilizojitokeza hivi sasa wakati wanapokwenda kufuata huduma.

Mhe. Spika, kamati pia inaishauri serikali kupunguza kiwango cha makusanyo kwa ofisi hii kuepusha kupandishwa kiholela kwa bei za usajili katika ofisi hiyo.

Ofisi ya Vizazi na Vifo

Mhe. Spika, kamati imesikitishwa sana na taarifa iliyopewa na ofisi hii kuwa bado mwamko wa wananchi kusajili vifo ni mdogo ingawa ofisi inapanga

kutoa elimu kwa jamii. Pia suala la kupata magamba ya kundikisha vyeti kwa wakati ni tatizo linalochangia kwa kiasi kikubwa uchelewezeshaji na upatikanaji wa vyeti na kumbukumbu nyingi zikiwa zimechakaa na nyengine zikiwa zimepotea jambo linalopelekea usumbufu mkubwa kwa wananchi wanapokwenda kufuata au kutaka kumbukumbu zao.

Mhe. Spika, suala la ucheweleshaji wa kupatikana magamba kuja kuchapishia Zanzibar Idara ya Uchapishaji, kamati inaishauri ofisi ijipange ili kuhakikisha inatafuta njia mbadala ya kuchapisha magamba hayo kwa haraka zaidi. Kamati inaiomba serikali kuharakisha mradi wa ujenzi wa Wizara ya Katiba na Sheria ili kutatua tatizo la ufinyu wa nafasi za kuhifadhia na kutunza nyaraka na kumbukumbu za serikali za vizazi na vifo katika ofisi hiyo.

Ofisi ya Msajili wa Hati Miliki

Mhe. Spika, wakati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilipoitembelea ofisi hii iligundua kwamba ofisi ina changamoto mbali mbali, kama vile uhaba wa watendaji ambapo Ofisi ya Pemba imefungwa kutokana kukosa watendaji na ofisi ya Unguja ina watendaji sita ambao wawili kati yao wapo masomoni.

Kamati imeelezwa changamoto ya utoaji rushwa Mahakamani kwamba ni kubwa na inarudisha nyuma juhudi iliyochukuliwa za Ofisi ya Msajili wa Hati Miliki kusimamia haki za wasanii wa Zanzibar. Mhe. Spika, kamati inaihimiza Ofisi ya Msajili wa Hali Miliki itoe elimu ya kutosha kwa jamii kuhusiana na kazi za ofisi hii na jinsi inavyoendesha shughuli zake. Elimu hiyo pia itolewe kwa Mahakimu wa Mahakama zote ambazo zinasemekana kuna harufu ya rushwa.

Hitimisho

Mhe. Spika, naomba nimalizie muhtasari huu wa ripoti ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuwashukuru Wajumbe wote kwa kunisikiliza kwa makini na kuwaomba na wao waweze kuchangia ipasavyo ripoti hii.
Aidha ninapenda kukushukuru wewe binasi Mhe. Spika, kwa mara ya pili kuniruhusu kuwasilisha muhtasari wa taarifa ya kufuatilia utekelezaji wa shughuli za kamati.

Mhe. Spika, kamati inachukua nafasi hii kuushukuru uongozi wa Wizara ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa waziri makini wa wizara hiyo Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Katibu Mkuu na watendaji wote wa wizara hiyo kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia kamati yetu ambayo imeiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake vizuri.

Aidha kamati pia inaishauri serikali kuiwezesha ofisi hii kwa malengo ya kusimamia vyema haki za wasanii ambao wengi wao hawanufaiki na kazi zao za kisanii. Kamati vile vile inatoa shukurani kwa Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora chini ya Waziri mweledi wa wizara hii Mhe. Haji Omar Kheir, Katibu Mkuu na watendaji wote. Na shukurani za pekee ziwaendelee Makatibu wa kamati yetu kwa kuipa kamati uwezo mkubwa wa kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, kwa niaba ya mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha naomba kwa dakika kama tano nitumie Kanuni ya 84 (9) kutoa maoni yangu binafsi katika maeneo mawili tu.

Mhe. Spika, eneo la kwanza naomba nilielekeze katika Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na si suala jipya mimi kulizungumzia, niliwahi kuliulizia swali kwenye kikao hiki lakini vile vile hata punde hivi limejitokeza katika ripoti mbali mbali za utekelezaji. Hili Mhe. Spika, linahusu kwamba kumekuwa na utaratibu wa ofisi nyingi za serikali kulalamikia kwamba kuna uhaba wa watendaji na watumishi. Matokeo yake kunakuwa na maombi na madai ya kuitaka Ofisi ya Umma na Utawala Bora iidhinishe uajiri wa watu.

Mhe. Spika, hili binafsi, hili halikujadiliwa ndani ya kamati likaamuliwa kwa hivyo ni langu binafsi kama mjumbe wa Baraza hili, mimi ninapata matatizo mawili na ningeomba Waziri atakapokuja hili atusaidie ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, uwiano wa watumishi wa umma kwa Zanzibar ukilinganisha Zanzibar na watu wake ni mkubwa mno ukilinganisha na nchi nyingi sana kama si zote nchi za Kiafrika. Mhe. Spika, Zanzibar yenye watu milioni moja na laki tatu kwa mujibu wa matokeo ya sensa iliyofanyika mwisho, ina watumishi wa thalathini na nane elfu. Wakati tunaambiwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina watumishi kama laki nne wanaohudumia wananchi karibuni milioni tariban arobaini na nne. Unaweza kuona ule uwiano ulivyokuwa mkubwa kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, taarifa zinaniambia kwamba watumishi hao thalathini na nane elfu tulionao tayari wanatumia takriban nusu kwa kulipa mishahara tu nusu ya makusanyo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Spika, utafiti mdogo niliofanya nimeambiwa kama makusanyo ya serikali hivi sasa imefikia kama bilioni ishirini na mbili kwa mwezi ambapo yamepanda kutoka bilioni kumi na tatu zilivyokuwa hapo mwanzo 2010, lakini katika bilioni ishirini na mbili, bilioni kumi na moja peke yake ni bajeti ya kulipia mshahara.

Sasa Mhe. Spika, hali hii huwezi uka-*sustained*. Tatizo ninadhani mimi ni kwamba sio uhaba wa wafanyakazi lakini ni kuajiri watendaji ambao hawana sifa ambao mara nyingi tunaajiri kwa kujuana, kupenyezana na humu tumeona katika ripoti za kamati teule zilipokuwa zinawasilisha ripoti limeonekana hilo kwamba kuna watendaji na viongozi wa wizara wanatumia nafasi zao kuwaajiri watu ambao pengine jamaa zao na watoto wao, hatuzingatii sifa, matokeo yake tunasema kila siku kazi hazifanyiki, kumbe tatizo Mhe. Spika, tunaajiri watu hawana sifa.

Mhe. Spika, mfano mzuri ni chombo chako hiki cha Baraza la Wawakilishi. Hatuna watendaji wengi sisi. Mpaka leo serikali inaendelea kutuona kama vile Baraza si muhimili kama vile ni idara ya serikali lakini watendaji walioajiriwa hapa wengi kwa sababu wana uwezo mzuri, matokeo ya ufanisi wa chombo hiki yanaonekana Mhe. Spika. Kwa hivyo wingi wa watendaji si ubora wa ufanisi wa kazi, inachotegemea uwezo na sifa. Mhe. Spika, ninachoomba kwanza waziri akija anisaidie.

La pili Mhe. Spika, ninachotaka kuzungumzia ni suala la ninalielekeza katika Wizara ya Katiba na Sheria. Hili Mhe. Spika, linalielekeza katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ndio inayohusika ingawa katika hili sasa simkusudii hasa waziri, ninaiambia serikali kwa jumla.

Mhe. Spika, hili linahusu suala ambalo hata jana nilizungumza. Mhe. Spika, hivi sasa nchi inapitia mapitio ya kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Imeelezwa punde hivi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwamba tukikosea hapa ndio Zanzibar tumekwisha, kwa sababu pengine itachukua miaka 50 mengine kuweza kupata fursa kama hii kama si zaidi.

Sasa Mhe. Spika, mimi ninasema ninalielekeza katika Wizara ya Katiba na Sheria kwa sababu ndio wizara inayosimamia kwa Katiba. Lakini nilikuwa ninadhani wakati sasa umefika na ninashukuru hivi asubuhi Mhe. Mohamed Aboud Waziri wa Nchi (OR) Makamu wa Pili wa Rais katoa maelezo mazuri sana katika kujibu hoja kwamba imefika wakati sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iwe na muongozo wake juu ya nini Zanzibar inakitaka, wananchi washafanya kazi yao kwa hivyo kama hoja kwamba serikali ilikuwa inashindwa kutoa maoni pale mapema ili isishawishi maoni ya wananchi, sasa yale yamemalizika wananchi wameshatoa maoni yao.

Lakini kuna hatari Mhe. Spika, ya kwenda katika hatua zilizobakia ya Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na taasisi nyengine zitakazoamua kujiunda katika Mabaraza ya Katiba na hatimaye Bunge la Katiba tukiwa tumegawanyika kutokana na mawazo yetu mbali mbali baada ya kuwa na

msimamo mmoja kama Zanzibar. Kwa hivyo nilikuwa ninaiomba serikali, naona hili kama hayupo lakini Mhe.Spika, mimi nilikuwa ninataka kumuomba hasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa niaba serikali hebu atupe kauli katika Baraza hili kwamba tumesimama wapi na vipi kama Zanzibar katika kutoa msimamo ambao unaoeleweka katika process hii ili hatimaye wananchi waridhike kwamba Baraza hili Mhe.Spika, serikali itasimamia maslahi yao.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, nikushukuru tena na kama nilivyosema yale ya awali yalikuwa ni ya kamati na haya ni yangu binafsi ninaamini yatapata majibu yote kwa umoja wakati ukifika.
Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa muda huu niweze kuchangia wizara hizi mbili za Utumishi na Wizara ya Katiba na Sheria.

Mhe. Spika, kwanza niwapongeze sana mawaziri kwa hotuba yao nzuri zilizowasilishwa na kutaja maeneo mazuri sana. Lakini hasa niunge mkono hotuba ya mwenyekiti aliyowasilisha hivi sasa hapo na baadhi ya mambo ameyaona yenye kasoro na ameeleza kama nafsi yake.

Lakini mimi niseme moja tu Mhe. Spika, katika Wizara ya Utawala Bora. Siku moja Mhe. Spika, nilisema hapa kuwa kuna mfanyakazi ambaye na mpaka leo sijapata jibu, nilitarajia kwenye kitabu hiki labda au kwenye taarifa ya Mhe. Waziriatanambia kuwa yule kijana amesharejeshwa kazini, sio lazima katika Wizara ile ya Afya, lakini hata wizara nyengine. Lakini sikupata jibu, labda Mhe. Waziri amesahau na walisema kuwa wamekubali kupokea, pamoja na Mhe. Mwanasheria, walijaribu kukaa naye na kuweza kupunguza hata ile fedha ambayo aliitaka kwa mujibu wa utaratibu.

Mhe. Spika, mimi nawaasa sana serikali, inapoamua kumtia mtu hatiani kwanza iangalie utaratibu wa sheria. Kwa sababu baadae inakuwa yule mtu anaposhindwa, serikali inaona mzigo mzito wa kuweza kumlipa ile haki yake. Lakini wakati huo huo muda mwingi sana wanamuweka ndani au wanamsimamisha. Aidha, wanamlipa nusu posho au hawamlipi kabisa, serikali pale inaona raha kabisa. Lakini baadae inapokuwa sasa raha ya kuona yule mfanyakazi, serikali inaona shida ya kumlipa.

Mhe. Spika, suala hili nimelisema sana, mwananchi yule ameitumikia serikali hii kwa muda mrefu, leo tunakuja kumnyima haki yake. Mhe. Spika, tutasema nini mbele ya haki. Mimi naomba tena Mhe. Waziri ni mtu mtiifu sana, lakini sijui ni sababu gani ya kuwa yule kijana wetu hawezi kurudishwa, inasikitisha

sana Mhe. Spika. Mhe. Spika, huyu mtu anapigwa mpira kama ule mpira wa uwanjani. Wallahi akienda Wizara ya Afya anapigwa mpira, kaja huku Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wamesema wanampokea, lakini hatima yake haikujulikana wapi.

Hebu naomba sana Mhe. Waziri yule mtu ana familia, ana watoto na kila kitu, basi tumfikirieni jamani, sio tuone ule mwanzo tu serikali kumtia hatiani na sasa hivi mahakama imeshageuka nayo, au hii mahakama ya wafanyakazi tuifute kama hatuiwezi, tuiondowe. Kwa sababu ni chombo tumekitunga hapa kwa mujibu wa sheria zetu. Lakini leo maskini ya Mungu mnyonge mpaka leo hii ametumikia serikali na pengine ni Mwanamapinduzi kabisa katika kugomboa, lakini haki yake tunamnyima.

Suala hili Mhe. Spika, naomba sana, nimejaribu leo kutizama sana kwa unyonge na upole, namuombea jamani huyu mtu. Tumfikirie na aweze kupewa maslahi yake. Aidha, aendelee kazini au mpeni maslahi yake afanye biashara zake ili aweze kujiendeleza. Naomba sana Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, suala hili Mhe. Ismail Jussa Ladhu kasema hapa, kwamba kuna watu watendaji aidha, wale wanachukua jamaa zao kuwatia, basi hata na sisi Waheshimiwa hatupewi nafasi na sisi tuna watu wetu vile vile. Suala hili Mhe. Spika, nataka niliseme sana na sisi tuna jopo la watu wetu kwenye majimbo yetu na wao wanataka kazi, tena ni wasomi wazuri tu, lakini tunashindwa Jimbo la Kitope sisi na Kikwajuni wapi.

Mhe. Spika, nakuambia tunashindwa kabisa, hatupewi nafasi Mheshimiwa, wanakwenda kuchukua nafasi za watendaji wadogo kabisa. Kama alivyosema Mheshimiwa mwenzangu hapa, wanachagua tu watu ambao hawana sifa. Mimi katika Jimbo la Kitope ninao watu kibao ambao wana sifa hizo, lakini sipati nafasi na hili nalisemea siku zote, hebu tupewe nafasi na sisi Waheshimiwa kwa nini tusipewe nafasi na ni haki yetu. Tunawasimamia wananchi, lakini wanakuja kwetu sisi wanatuambia, Mheshimiwa leo nimeshasikia matangazo na kuna watu kibao tumewasikia. Nakwenda mimi, lakini nikienda kule sionekani kama ni Mheshimiwa, angalau nione ule umuhimu wa kuweza kuambiwa Mheshimiwa kaja, niambiwe kwamba lete vyeti vya watu wako, siambiwi ng'oo Mhe. Spika. Kubwa naambiwa nafasi moja ina watu zaidi ya 100, nimeshaondolewa pale nitasema nini mimi.

Kwa hivyo, nasema Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kwa makusudi afanye hilo zoezi la Waheshimiwa wote wapewe nafasi katika majimbo ya wananchi wao ili waweze kupata kazi. Kazi zipo Mhe. Spika, tena kweli kweli lakini bado tumezing'ang'ania hatuwezi kuzitoa, sijui kwa sababu gani.

Lakini la pili nimshukuru Mhe. Waziri kuhusu suala la Chuo. Amejitahidi kwa kiasi kikubwa sana, chuo cha kisasa, kinatoa fani nzuri *Alhamdulillah Rabilaalamina*. Lakini ulinzi, naomba sana suala la ulinzi litiliwe maanani kabisa, kwa sababu siku hizi vibaka wako wengi. Unamuweka mtu pale na kirungu atawezaje, watu wanakwenda 10 na wana mapanga yao. Hilo nakuomba sana Mhe. Spika, ulinzi uimarishwe ili kuweza kuwasaidia wale wapiga virungu. Sio kwamba waondoshwe, na wao waajiriwe hivyo hivyo, lakini waongezeke na watu wengine wenye silaha za moto, ili kusaidia ulinzi uwe mzuri zaidi. Kwa hilo mimi nakushukuru sana Waziri wangu jitahidi, kwa upande huo mimi sina maneno mengi, nakwenda katika Wizara ya Katiba na Sheria.

Vile vile Mhe. Spika, nilijaribu kuangalia katika ripoti yake Mhe. Abubakar, kuna mambo mengine binadamu hata kamati nayo binadamu, tunasahau tunaweza kusaidiana, ndio maana tukasema kuwa tuna wajibu wa kuchangia.

Mhe. Spika, niseme kwanza katika mahakama chakavu, Mfenesini nayo sijaiona humu, hata choo haina, choo chake kibovu kabisa. Namuomba Mhe. Waziri aweze kuliona suala hili na kuweza kulipatia ufanisi mzuri, hasa kutokana na kuwa sasa hivi kituo kile kimekuwa kama cha mkoa, ni cha mkoa hasa, sio kama ni cha mkoa, ni cha mkoa hasa. Kwa hivyo, nacho akipe heshima na taadhima kama majengo mengine uliyoyasimamia Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban hapa Mwera na yeye atupe historia yake ya kutuwekea yale majengo katika mikoa yetu.

Pia niseme Mhe. Spika, niwatetee majaji wangu. Siku moja niliona jambo ambalo hata mimi halikunifurahisha. Siku ambayo tulipewa vitambulisho na Mhe. Rais, kwa kweli pale nilihuzunika sana. Wale majaji wakuu walikuwa wanapigwa mpira kutokana na *protocol* sijui ikoje, mara wamepelekwa hapa, mara wamepelekwa huku na hatimaye wameondoka. Kwa kweli mimi naomba sana na wao hebu tuwaheshimu na tuwape kipaumbele kile cha sheria na heshima na wao kama ni wakubwa. Mhe. Spika, ilikuwa ni aibu tosha siku ile kusema kweli na ni jambo la kusikitisha. Sijui hawa wenzetu wa wizara husika sijui wanawawekaje. Ndio maana tukasema kwamba hebu tuangalieni huko katika utumishi wetu ambapo unalingana vipi na watu kama hawa. Mimi mwenyewe nimeona kwa macho yangu, lakini sikuwa na sauti pale ya kusema kwamba njooni huku, kwa sababu mimi mwenyewe ndio Mwakilishi, hivyo nilishindwa kwa sababu sio mpangaji, wako watu wanaopanga kwa mujibu wa sheria zetu. Lakini haikupendeza Mhe. Spika, hata kidogo. Tuliwasumbua na mwisho waliondoka kiaina, mimi niliona waliondoka kiaina na wao hawakuondoka kwa hasira. Nalo hili tulifikirie ili na wao wapewe heshima kubwa kutokana na ngazi zao walizokuwanazo.

Vile vile Mhe. Spika, nilisema sana kuhusu hawa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo habari ya maposho yao. Mhe. Spika, nilisema sana kuhusu habari hii, tuwajali kwa sababu na wao wana vyeti vizuri na wao, wana Diploma, wengine Digrii ni sawa sawa na mahakama nyengine za mkoa na kuendelea huko mbele, nilisema sana Mhe. Spika, lakini nashangaa sana utaratibu huu mpaka leo bado haujafikiriwa.

Mhe. Spika, suala hili nalisema siku zote kwamba kwa nini tunachelewa ni sababu gani, ni sababu ambazo tukiuliza hatuwezi kupata jawabu, sijui ni sababu gani. Tutaendelea na bajeti nyengine na nyengine, bado tutang'ang'ania hapa hapa. Kwa hivyo, mimi naomba hili suala tuwafikirie na wao, tuondoe msongamano wa kuwafanyisha hawa wakala rushwa, hawali rushwa lakini utawasababisha ni binadamu na wao wanachanganyikiwa wakiondoka nyumbani hali inakuwa ngumu ya maisha na sisi tunaelewa hali ya maisha ya Zanzibar iko ngumu kidogo. Kwa hivyo, ni lazima tuone ni jinsi gani ambavyo tunaweza kuwasaidia na wao, tukawafikiria kwa wakati ili kuweza kuendesha maisha yao.

Lakini Mhe. Spika, tulipitisha sheria hapa ya kuwataka majaji wa kusaidia kesi kuzipunguza katika mahakama za ardhi, tukasema kwenye mikoa tutawapeleka. Lakini ile sheria sijui niseme, ndio sheria kwa sababu chombo hiki kina wajibu wa kutunga sheria, lakini mpaka leo tunawapa tabu wale watu wawili tu, tunawasumbua. Kuna mwanamama pale na kuna baba pale, tunawasumbua kusema kweli ni kazi nzito. Hili mnalijua wazi suala la migogoro ya ardhi, mnayajua matatizo yake yalivyo na wingi wake. Kwa hivyo, tulisema zamani jamani tatizo liko wapi. Tunao majaji walikwenda kusoma nchi mbali mbali na mpaka leo hawajapandishwa vile vyeo ambavyo vinastahiki kutokana na masomo yao, sijui tatizo liko wapi Mhe. Spika. Ndio maana tukasema tatizo letu sisi hapa tunachelewa sijui kwa sababu gani. Lakini mimi sioni ni vitu ambavyo viko *simple* na sheria yetu, kwa nini tunashindwa kuwaajiri watu kama hawa. Ukienda huko unaambiwa tume ya mahakama haijakaa, au tume ya mahakama imekaa lakini hawajakubaliana na hao watu. Hawajakubaliana vipi na hao watu wana vyeti vyao.

Kwa hivyo, mimi naomba suala hili Mhe. Spika, kwa sababu sasa hivi wenzetu tunawapa mzigo mzito, yule mama wakati wowote binadamu anaweza kuwa mjamzito, kesi zitaendelea kurundikana na yule baba na yeye naye anaweza ni binadamu naye akatokezea kuumwa au akatokezea na matatizo mengine, kesi zitaendelea kulala. Kwa hivyo, mimi naomba Mhe. Spika, hili suala lifikiriwe sasa hivi, ili tukija kwenye bajeti tujibiwe pale kuwa tayari wameshapelekwa hao watu.

Vile vile Mhe. Spika, niende katika suala la Watathmini. Watathmini hawa sijawasikia kabisa hawa wazee wetu tuwafikirieni maposho yao. Kwanza posho lenyewe dogo, halafu la pili nayo yanachelewa kwa muda kuwapa. Kwa hivyo, Mhe. Spika, naomba na hawa wazee wetu tuwafikirie wanakaa sehemu mbali mbali, wanakaa mashamba, hata wakija mjini wenyewe na hilo posho lenyewe halikuja kwa wakati basi utamkuta yule mtu amerundika madeni ambayo hayastahiki kuweza kurundika. Kwa hivyo, nalo hili naomba Mhe. Spika, ili kuweza kuwaondoshea wazee wetu matatizo ya kupita na kukopa kopa au kuombaomba, nao tuwape kwa wakati ambao unawaruhusu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi leo hasa katika masuala ya sheria, kwa kuwa sijavaa miwani naona Mhe. Spika, niwashukuru sana mawaziri wetu wawili hawa na hasa Mwenyekiti, aliyeleta ripoti yake kuwa ni nzuri sana na naiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Mimi Mhe. Spika, naomba kukaa kitako, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Makame Mshimba Mbarouk tunakushukuru. Nafikiria muda uliobaki ni mchache mno hatutoweza kuendelea na mchangiaji mwengine. Kuna tangazo moja na baada ya hapo tupate kwenda kupumzika.

Waheshimiwa Wajumbe, nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa wanamichezo wote, tunajulishwa taarifa ya mechi kati ya timu ya Baraza la Wawakilishi na timu ya KMKM. Mchezo huo utafanyika keshokutwa siku ya Jumapili, wakati wa saa 10 jioni katika uwanja wa nje wa Amani. Mchezo huo ni miongoni mwa mashindano ya Mei Mosi ambayo yanaanza hapo kesho, lakini mchezo wenyewe ni siku ya Jumapili, lakini mtiririko wa michezo ya Mei Mosi inaanza kesho kwa mujibu wa taarifa hii.

Kwa hivyo, shime wachezaji na wapenzi wa timu yetu tuhudhurie kwa wingi ili kuwapa nguvu wachezaji wetu na hatimaye tuweze kushinda katika mechi hiyo, siku ya Jumapili saa 10 jioni, kwenye uwanja wa nje wa Amani.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya taarifa ya tangazo hilo, sasa nichukue nafasi hii kwanza kuwashukuru sana kwa mashirikiano makubwa ambayo mmenipa katika kuendesha shughuli zetu.

Pili, sasa ni wakati muafaka niakhirishe kikao hiki hadi siku ya Jumatatu ya tarehe 15/04/2013 saa 3:00 barabara za asubuhi.

(Saa 1:36 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 15/04/2013 saa 3:00 asubuhi)